ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake

18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani

39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake

40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi

41. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake

42. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo

43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo

44. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake

45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Jimbo la Mtoni

46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje

47. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe

48. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini

49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi - Jimbo la Mtopepo

50. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

51. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

53. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

55. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali- Jimbo la Uzini

57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

67. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Nne - Tarehe 12 Disemba, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 na Kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na Masuala Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 na Kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na Masuala Mengine Yanayohusiana na Hayo. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 96

Uhaba wa Maeneo ya Kuegeshea Vyombo

Mhe. Nassor Salim Ali: (Kny. Mhe. Suleiman Sarahan Said) - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuleta maendeleo kwa wananchi wake na nchi kwa ujumla. Katika Mji wa Chake Chake, Baraza la Mji linaendesha *operation* maalum ya kutoruhusu magari kuegesha pembezoni mwa barabara na hata maeneo muhimu ya huduma za jamii kama benki, maeneo ya kukatia tiketi za ndege na kadhalika, wakati wananchi wakitaka huduma katika maeneo hayo ambapo maeneo yaliyotengwa kwa maegesho hayapo au yapo mbali sana na huduma hizo.

(a) Je, serikali haioni kuwa inaleta usumbufu kwa wanaotaka huduma na baadhi ya wakati huhatarisha usalama na mali zao.

(b) Je, serikali ina mpango gani wa kuweka maeneo ya maegesho ya kudumu katika Mji wa Chake Chake.

(c) Je, wizara haioni kutokuruhusu maegesho kunaipotezea serikali mapato.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 96 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, Baraza la Mji wa Chake Chake kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya, limeanzisha utaratibu wa kuondosha gari zinazoegeshwa pembezoni mwa barabara na maeneo yasiyoruhusiwa, kwa lengo la kupunguza msongamano na kuepusha ajali zisizokuwa za lazima. Katika kufanikisha zoezi hilo, Baraza limetayarisha maeneo maalum kwa muda *(temporary)* ya kuegesha gari hizo, ikiwa ni pamoja na eneo la Tibirinzi, Madungu *flat*, eneo la Miembeni kwa kushushia abiria na maegesho ya gari za *taxi* na eneo la benki kwa ajili ya wateja wa *PBZ*. Hali hiyo imeleta ufanisi na kuimarisha huduma ya usafiri katika Mji wa Chake Chake pamoja na kuwaondolea usumbufu wananchi.

(b) Mhe. Naibu Spika, serikali imepanga kuliendeleza eneo la Tibirinzi liliopo karibu na soko kwa ajili ya maegesho ya kudumu katika Mji wa Chake Chake, ambapo kazi za utafiti na uandaaji wa michoro ya eneo hilo itafanyika. Kwa sasa eneo hilo lina urefu wa mita 100 na upana wa mita 60 na tunatarajia kuongeza upana wa mita 10. Vilevile, serikali kupitia Baraza la Mji Chake Chake linaendelea na mpango wa kutafuta ufadhili kwa ajili ya kujengewa stendi ya kudumu ya Chanjaani kwa ajili ya gari za abiria na binafsi.

(c) Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa kuegesha gari katika maeneo maalum na kutoruhusu uegeshaji wa gari pembezoni mwa barabara, ni hatua mojawapo za uimarishaji usalama katika barabara na kuongeza mapato ya serikali yatokanayo na ada ya uegeshaji wa gari katika maeneo yaliyokusudiwa. Kama tutaendelea kuruhusu uegeshaji wa gari katika maeneo yasiyokubalika ni dhahiri kuwa tutaendelea kupoteza mapato yatokanayo na ada ya maegesho ya gari katika maeneo yasiyoruhusiwa na pia kupelekea uwezekano wa kutokezea ajali za mara kwa mara.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, mbali na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, kwanza nimpongeze kwa majibu yake kwa ufasaha. Lakini pamoja na majibu hayo naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake amesema kwamba serikali kupitia Baraza la Mji wa Chake Chake inaendelea na mpango wa kutafuta ufadhili kwa ajili ya kujengewa stendi ya kudumu ya Chanjaani.

Je, serikali haioni kwamba ipo haja kutenga fedha katika bajeti inayokuja kuanza kazi ya kuijenga stendi hii ya Chanjaani, ili kuondoa usumbufu huu unaowakabili wananchi wetu katika jiji la Chake Chake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa majibu ya ziada kwa Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli ushauri wa Mhe. Mwakilishi serikali kuona kwamba kuna umuhimu wa kutenga bajeti maalum ambazo zitaweza kusaidia katika ufanisi wa utekelezaji wa stendi hiyo kama azma ya serikali ambavyo imekusudiwa, ni jambo moja la msingi sana na serikali imekuwa ikifanya juhudi hizo za makusudi. Utaratibu ni kwamba zimekuwa zikifanyika juhudi hizo za makusudi katika kukabiliana sio katika stendi hiyo tu ya Chake Chake/Chanjaani bali na kwengineko. Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba ushauri huo tumeuchukua na hilo ni jambo ambalo serikali inaendelea kulifanya na tutazingatia tuone kwamba kwa kipindi cha mwaka wa bajeti unaokuja tutaangalia ni nini ambacho kitaweza kufanyika zaidi katika kuona jambo hili linafanikiwa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo tu la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri yanayoonesha utekelezaji mzuri wa maegesho yetu. Lakini Mhe. Naibu Waziri kwa ujumla *parking* zote ziliomo kwenye Manispaa za Unguja na Pemba pamoja na Halmashauri zake hazipo vizuri katika utekelezaji na kuziratibu katika kutoa huduma hasa na tozo.

(a) Je, ni lini wizara yake itaweka utaratibu mzuri wa maegesho katika manispaa zake.

(b) Katika eneo la ukusanyaji wa mapato kuna utaratibu gani uliopangwa na wizara wa uboresha hii huduma ya kutoa tozo, ili kuepusha upotevu wa mapato yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa majibu ya ziada kwa Mhe. Mwakilishi wa kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri kwamba katika sehemu zetu za kutoa huduma za maegesho kama ambavyo Mhe. Mwakilishi amesema bado hazipo vizuri. Lakini naomba nitoe majibu yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, hali hii tumeshaibaini na ndio maana Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa imekuwa ikiangalia namna kuona kwamba tunaongeza ufanisi katika usimamizi juu ya utoaji wa huduma katika maeneo hayo, ili usimamizi wetu huo uweze kuonesha tija wananchi wapate huduma kama vile ambavyo zimekusudiwa na serikali.

Lakini pamoja na hayo, sasa hivi kazi kubwa ambayo inafanyika katika Ofisi ya Rais kwa kupitia hizo Halmashauri na Manispaa zetu, tumeona ni maeneo ambayo kwa kweli mikakati imeanza kufanyika katika kuona jambo hilo linafanikiwa usumbufu unaondoka kwa wananchi wetu. Hivi sasa kama tunavyoona katika maeneo ya Kijangwani pia zile ni juhudi ambazo zinafanyika katika kuona kwamba tatizo hili linaondoka. Nimpe matumaini Mhe. Mwakilishi hili jambo litafanikiwa na muda sio mrefu.

Mhe. Naibu Spika, vilevile suala la kuongeza ubora wa ukusanyaji wa mapato naomba niseme nalo pia nithibitishe kwamba tumekuwa tukipoteza fedha nyingi, kutokana na hali ya kukusanya kwa kutumia huu mfumo ambao tunakwenda nao wa mikononi kwa kuandika risiti na mambo

mengine. Kwa sasa ni kwamba hali hiyo tumeshaibaini, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tumeongeza wigo mpana zaidi katika kuona tunatoa usimamizi wa ziada kuona fedha hizi hazipotei. Lakini si hilo tu, vile vile tumekuwa tukitafuta namna ya kuona hatupotezi mapato, sasa hivi tunatarajia katika kipindi hichi cha karibuni Mwenyezi Mungu akijaalia tunaweza kufanya tukaingia katika mfumo wa ukusanyaji kwa njia ya *electronic,* ili kuona kwamba hatupotezi hizo fedha kama ambavyo tumekuwa tukipoteza siku zote. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri lakini nataka kumuuliza kwamba katika Manispaa ya Chake Chake tuna *block* pale ya kuweza kuchangia magari yote yanayoingia mjini. Lakini watu wale ambao naweza kutoa mfano kama vi-*carry* ni vigari ambavyo vinatafuta riziki pale mjini. Tumeondoa magari ya ng'ombe, ili kuweza vigari vile visaidie watu katika kutoa biashara. Lakini hakuna eneo hata moja walilotengewa zaidi ya kufukuzana na wale watia vyuma ambayo ni matatizo yanayojitokeza.

Sasa Mhe. Naibu Waziri, una mpango gani wa vi-*carry* kuviweka katika maeneo ambayo watu wataondoa usumbufu na wakati huo huo ujue kwamba watu wale wameshalipa kodi, kwa hivyo hawahitajiki kusumbuka. Sasa una mpango gani wa kuweza kuwawekea mazingira mazuri katika mji wa Chake Chake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, katika Mji wa Chake Chake naomba nikiri kwamba tuna changamoto kubwa. Kutokana na jiografia ya mji wenyewe wa Chake Chake tumekuwa tukitafuta namna mbalimbali za kuona kwamba utoaji wa huduma, tunauzingatia sana katika masuala mazima ya *parking* za magari na mambo mengine yanayofanana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, juhudi za kitaalam zinaendelea katika kutafuta namna bora ya kuona kwamba ni maeneo yepi ambayo yanaweza yakafaa labda kwa vi-*carry* au na magari mengine, ili kuona kwamba huduma hizo zinafanyika sambamba na lile zoezi la ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Naibu Spika, tunataka tufanye juhudi hiyo kwa makusudi, ili kwasababu hii tija yake tunaijua vizuri lakini tumekuwa na changamoto hiyo. Sio vi-*carry* tu, hata boda boda nazo tumekuwa na changamoto kubwa kwasababu msongamano umekuwa mkubwa.

Kwa hivyo, ninachokuomba tu Mhe. Mwakilishi tupe mashirikiano ya dhati ili kutafuta namna na eneo gani ambalo kwa kweli ni rasmi tuweze kushirikiana pamoja na Baraza la Mji Chake Chake, kuona kwamba tunaondoa usumbufu huo ambao umeanza kujitokeza ili kusudi wananchi wetu wapate huduma kama vile dhamira ya serikali ambavyo imekusudia.

Nam. 99

Utanuzi wa Barabara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:

Serikali inastahili pongezi katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake na miji kama Chake Chake na miji mingine. Katika mji wa Chake Chake ipo Ofisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, lakini katika ofisi hiyo ipo njia moja nyembamba inayotumika kwenda kwenye ofisi hiyo ambayo ni muhimu, kwani Mhe. Makamu huitumia kwa shughuli za serikali na baadhi ya wageni, hatahivyo barabara hiyo sio salama sana.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara nyengine ya kutokea kuliko kutumika barabara hiyo hiyo moja.

(b) Je, upo mpango wa kuitanua barabara hiyo kwani ni hatari kwa hivi sasa, ili iweze kupata barabara mbili ya kwenda na kurudi.

(c) Je, kuna mpango gani wa kiusalama au alama maalum za kuonesha kuwa barabara hiyo ni nyembamba na upande mwengine ni bonde, ili kumpa tahadhari dereva na kuwekwa uhalisia wa barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 99 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba njia inayoelekea Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutoka Hospitali ya Chake Chake ni nyembamba lakini hali hii inatokana na jiografia ya eneo hilo ambalo lina milima na mabonde pembezoni mwake. Hata hivyo, Ofisi yetu kupitia Baraza la Mji wa Chake Chake inaangalia uwezekano wa kutayarisha barabara nyengine kupitia katika soko la Tibirinzi endapo hali ya mazingira itaruhusu ujenzi katika eneo hilo.

(b) Mhe. Naibu Spika, kwa sasa mazungumzo yanaendelea baina ya Baraza la Mji Chake Chake na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kuangalia uwezekano wa kuitanua barabara hiyo kwa kuzingatia athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza kulingana na jiografia ya eneo husika endapo barabara hiyo itatanuliwa.

(c) Mhe. Naibu Spika, kazi za uwekaji wa alama za barabarani ni endelevu. Hivyo, hatua za haraka zitachukuliwa kuhakikisha alama hizo zinawekwa, ili kutoa tahadhari kwa madereva wa vyombo vya moto wanaotumia barabara hiyo.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana na nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini nataka nimwambie Mhe. Naibu Waziri kwamba Mji wa Chake Chake sasa hivi unakua kwa kasi sana. Unapokwenda asubuhi mpaka kwenye saa kumi jioni msongamano wa magari umekuwa mkubwa sana. Sasa tatizo linajitokeza kwamba ofisi yako ya Manispaa imekuwa inatembea na mavyuma kila maeneo, imekuwa mtu akisimama pahala katika barabara hata kama gari bado zinasubiri anakuja kumfungia vyuma pale pale. Sasa

mimi ningeona katika suala la kwanza, suala la vyuma pale mji wa Chake Chake ukasimamisha mara moja mpaka hali halisi ikawa inaendana na lile tukio.

Lakini la pili, ni kwamba tayari kama hali ya barabara ile inaonekana kuwa ni nyembamba na haiwezi kurudisha, ipo barabara ambayo inaweza ikatokezea sokoni pale sasa hivi bila ya madhara yoyote. Haijajengwa ile barabara wala haijafanywa chochote.

Je, Mhe. Naibu Waziri, una mpango gani wa haraka kuidhibiti ile barabara ya kutokea katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kabla watu hawajajenga halafu ikawa *compensation* na mambo mengine yakaanza kuendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Mwakilishi kwa namna bora ambavyo amekuwa akiwatumikia wananchi wa Jimbo la Chake Chake katika suala zima la utetezi. Hii ni dhahiri kwamba Mheshimiwa anajituma. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, kuhusu kusitisha huduma mpaka pale ambapo huo utaratibu aliousema alioshauri kwamba ukawe sawa. Naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi tukubaliane kwamba suala jengine katika Baraza la Mji Chake Chake tunahitaji kupata mapato, na lazima tukiri kwamba msongamano katika Mji wa Chake Chake bado ni changamoto kutokana na jiografia, kama nilivyoeleza katika swali la msingi, kwamba jiografia ya Chake Chake kama tunavyoifahamu.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo sisi ushauri ambao Mhe. Mjumbe ameutoa basi tutaufanyia kazi, ili kuona kwamba tuko tayari kushirikiana naye katika kuona ushauri ule alioutoa tuweze kuufanyia kazi. Lakini bado turudi pale pale kwamba changamoto tuliyokuwa nayo ni kubwa na inahitaji umakini wa hali ya juu, ili kuona kwamba tunafanikisha mipango ya serikali, kwasababu lengo la serikali sio kuwatesa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kwamba ni lini utaratibu tunaweza tukachukua hatua juu ya kufanikisha upatikanaji wa hiyo huduma ya kujenga barabara. Pia nirejee Mhe. Naibu Spika, kwamba tuko tayari kuanza wakati wowote pale ambapo itakuwa hali inaruhusu. Kwahivyo, ninachokuomba tu tuendelee kushirikiana katika kusaidiana pamoja na wataalamu wengine, ili tuone kwamba suala hili kama dhamira ya serikali ilivyo ni kutatua kero za wananchi, tuweze kutatua kero kwa mujibu na hali ambavyo inaruhusu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi tena ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri na mwanana katika kuwatumikia wananchi.

Mhe. Naibu Waziri kama alivyokiri katika maelezo yako kuwa wizara yako inaendelea kuwa na jukumu la kujenga zile barabara ndogo ndogo za ndani yaani *feeder roads* Unguja na Pemba, zilizokuwepo ndani ya Manispaa na Halmashauri husika. Nilitaka kujua kwa sababu bajeti yako

ipo inayopita hapa, lakini ipo inayopitishwa na mabaraza ya madiwani. Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotengwa kwa ujumla katika utekelezaji wa ujenzi wa barabara hizi za ndani kwa kupitia hizo manispaa zako ambazo jukumu la msingi kwa wizara yako. Lakini ni barabara zipi ambazo mpaka sasa zimefanikiwa kujengwa na kiasi gani cha fedha kimetumika. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa majibu ya ziada kwa Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Mhe. Mwakilishi alitaka kujua ni fedha kiasi gani ambazo tumezitenga kwenye bajeti hii katika kuona kwamba tunaweza tukakabiliana na ujenzi wa barabara za ndani katika visiwa vya Unguja na Pemba kwa ujumla.

Vilevile, alitaka kujua kwamba katika zile bajeti ambazo tunazielekeza kwenye Halmashauri. Naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali hili la mwisho, kwamba hadi sasa hivi sina takwimu halisi ambazo zinaonesha ni kiwango gani Halmashauri zetu au Manispaa zetu zimeweza kutoa ufafanuzi. Lakini kwa majibu ya ziada naomba tu nimpishe Mhe. Waziri aweze kutoa majibu zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Kwanza kwa mwaka katika utekelezaji wa ujenzi wa barabara za ndani ambazo zinatekelezwa na Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri, bajeti yetu ni bilioni 1.5 kwa mwaka, kati ya hizo bilioni 1.35 ni kwa ajili ya ujenzi wa barabara na milioni 150 ni kwa ajili ya uendeshaji na ufuatiliaji. Lakini toka tumeanza mpango huu wa ujenzi wa barabara za ndani ambazo zinashughulikiwa na ofisi yetu, kiasi cha shilingi bilioni 4.5 zimeshatumika ukijumuisha bilioni 4.15 ambazo zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara na milioni 450 zimetumika kwa ajili ya shughuli za uendeshaji. Ahsante sana.

Nam. 104

Mgongano wa Sheria za Dini na Serikali kuhusu Mtoto

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi katika kuboresha sheria na kuweka misingi mizuri ya kufuata na kuheshimu sheria za dini. Hatahivyo, bado inaonesha sheria za nchi zinahusiana na haki za watoto na sheria za dini ya Kiislamu kutokubaliana kwa uwazi kwa mfano sheria ya dini mtoto akipata ukubwa kwa umri wowote ule mtoto anatakiwa kuolewa. Wakati mwengine baba mzazi hasikii haoni kwa kisingizio cha sheria za dini, mtoto aolewe. Na wakati huo huo mtoto huyo ukija kwenye sheria za nchi zinamlinda asiolewe, ama kwa kisingizio cha sheria za umri mdogo au hajamaliza masomo sasa ndio inakuwa tatizo la kukosana kwa familia.

(a) Je, kutokana na mgongano huo wa sheria, serikali husimama kwa sheria zipi za dini au serikali kumlinda mtoto.

(b) Je, kama mtoto wa kike anataka kuolewa au kuozeshwa na baba au walii wake na mtoto hataki pengine kwa maslahi mazuri, lakini mtoto hataki ni sheria ipi itamlinda mtoto au baba kwa maslahi yao.

(c) Je, kwanini sheria za nchi hutumika kiamri na kusitisha sheria za dini na miongozo yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 104 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, Katiba ya Zanzibar ni miongoni mwa katiba bora sana kuwahi kutokea katika dunia, masuala mengi na ya msingi yameelezewa katika katiba yetu, kwa mfano kifungu cha 19 cha Katiba ya Zanzibar kinatoa uhuru wa mtu kuamini dini au imani aipendayo mwenyewe. Kwa msingi huo suala la kuamini ni suala la mtu binafsi na serikali haiingilii uhuru wa kuabudu na kuamini kwa mtu yeyote.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, katika suala hili napenda ifahamike kwamba sheria za nchi na zile za dini hazina mgongano, tatizo kubwa linalojitokeza ni utofauti wa ufahamu baina ya watu wenyewe. Pale endapo mtoto atakataa kuolewa kwa sababu za masomo, serikali itasimamia sheria za nchi kwa maslahi ya mtoto kielimu. Kufanya hivyo kwa serikali ni kuendana na sheria za dini, kwani hata sheria za dini zinasisitiza umuhimu wa elimu kwanza juu ya chochote kile. Ndio maana kifungu cha 19 cha Sheria ya Elimu namba 6/1982 kinatoa ufafanuzi mzuri juu ya umri wa mtoto kutakiwa kumaliza skuli.

Vilevile, kifungu cha 20 cha sheria hiyo hiyo kinatoa wajibu kwa mzazi au mlezi wa mtoto kuhakikisha mtoto anahudhuria masomo yake katika skuli aliyosajiliwa mpaka amalize elimu yake ya msingi, na mtoto husika hatoolewa hadi atakapomaliza elimu yake ya msingi. Pia, katika Sheria za dini Mtume Muhammad (*S.A.W)* hakupewa utume mpaka alipopewa elimu. Hii inaonesha kuwa suala la elimu katika imani yeyote ni jambo la lazima kwani hakuna chochote kitakachofanyika vizuri bila ya elimu'.

(b) Mhe. Naibu Spika, suala la ndoa ni furaha na upendo na mambo haya hayapatikani bila ya kupatikana ridhaa ya mwenye kuolewa (mtoto) na walii wake. Hivyo, basi pale ambapo mtoto amekataa kuolewa na ana sababu za msingi (maslahi mazuri) kama suala linavyouliza.

Kwa mfano, mtoto anaetaka kuolewa ni mcha mungu (tabia njema) ila mwanaume anaetaka kumuoa ana tabia mbaya kama vile mlevi, mwizi, mpigaji au aswi wa aina yeyote hata kama umri wa kuolewa umeshafika, mtoto huyo anayo haki ya kukataa na hapa sheria zote za dini na za nchi zitamuunga mkono na kumlinda katika maamuzi yake

hayo. Sheria ya mtoto Namb 6/2011 imemlinda vyema mtoto katika Kifungu cha 12 (1) (2)kwa kumtaka mzazi au mtu mwenye dhamana ya mtoto kuhakikisha mtoto anapata haki zote. Mfano, haki ya kuishi, utu, heshima, elimu nk. Pia Mzazi au mtu mwenye dhamana ya mtoto kisheria atakuwa na jukumu la kuhakikisha anasimamia maslahi bora ya mtoto wakati wote. *(Makofi)*

(c) Mhe. Naibu Spika, sheria za nchi hazitumii amri bali zinatoa miongozo mizuri kwa maslahi ya wananchi na ndio maana hata pale watu wanapolazimika kupelekwa katika vyombo vya sheria za nchi, basi mwisho hutafutwa wataalamu wa sheria za dini kwa ajili ya kulimaliza suala hilo. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake ya ufafanuzi mazuri sana**.** Lakini na mimi kidogo nina swali moja la nyongeza ili kwa faida ya wananchi ambao wana matatizo kama haya.

Mhe. Naibu Spika, dini ina misingi yake ambayo imetoa kwa ajili ya mtoto kuolewa, ingawa kuna mazingira mengi ambayo Mhe. Naibu Waziri ametoa ufafanuzi, lakini yote haya hayakuwekwa bayana sana katika kuolewa, lakini cha msingi kinachojitokeza ni kwamba mtoto kwa mzazi hakui, hata akifikia miaka 18 ambayo tunasema ni umri wa mtu mzima kwa upande wa serikali, lakini bado kwa baba yake anahitaji uwalii na kila kitu.

Je, tatizo linalojitokeza wanafunzi wetu au watoto wetu wanafikia umri wa miaka 18 au kuanzia miaka 19 ameshavuka kiwango, lakini yeye kama ulivyosema bado ana hamu ya kusoma au ya kuendelea. Lakini kidini kuanzia miaka ambayo atapata ukubwa wake tayari anahitaji kuolewa na wazazi wameshakubaliana na mambo yote ya kuolewa, lakini bado mtoto inamsimamia sheria. Sasa nilikuwa nauliza hapa baba ana nguvu gani, mtoto ana nguvu gani na serikali inampendelea nani kati ya hapa, kwasababu umri wa kuolewa tayari na baba walii wameshakubaliana. Tatizo lilijitokeza ni kwamba mume sio mlevi, wala sio mwizi na wala hana tatizo lakini yeye hataki kuolewa, hapa inakuaje mnatusaidiaje serikali hilo suala.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala linazungumza kwamba elimu ilikuwa ni muhimu. Mhe. Naibu Spika, watu wengi walioolewa nyuma walikuwa wala hawakuwa na elimu, wengine waliolewa tu na mpaka sasa hivi bado kuna watu ambao wengine hawajafikishwa shule katika mazingira ya shamba, lakini bado serikali ukimuozesha mtoto zaidi ya miaka 12 au hajafika miaka 18 bado serikali inamchukulia kama mtoto huyu amedhalilishwa inakuaje serikali hebu tusaidie maelezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika jibu mama, suala la dini halina mjadala kama vitabu vyetu vitukufu vinavyoonesha suala hilo kwamba upo umuhimu huo wa umri unahusika kwa mfano katika dini ya Kiislamu mara tu pale mtu anapokuwa kuolewa au kuozeshwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini tuelewe tu kwamba dini hiyo hiyo au dini hizo hizo zinasisitiza umuhimu wa elimu. Nirejee kusema kwamba pale ambapo patakuwa pana maslahi ya mtoto kielimu basi serikali itasimama kwa hilo ili kuhakikisha kwamba yule mtoto anapata elimu.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri mara nyingi tunashuhudia mitaani kuna mizozo baina ya mama na baba hususan pale wanapoachana, na wazee kama hawa hukataa kabisaa kuwaozesha au kutoa idhini ndio inabidi watoto wale kuozeshwa Mahakamani.

Je, ni hatua gani zinazochukuliwa za kinidhamu kupewa wazee kama wale. Pia huoni kama ni udhalilishaji wanaofanya wa kuwanyima haki zao za kisheria.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, ni kweli baadhi ya wazee huwa wanakataa kuwaozesha watoto wao wale watu ambao wamewapenda. Mara nyingi wazee huwa wanakataa kwa sababu za kimsingi.

Kwa mfano, kama mzee ameona kwamba mwanawe anataka kuolewa na mtu ambaye, kama nilivyoeleza katika jibu langu mama kwamba tabia yake ni mbaya, ni mlevi na mpigaji. Kwahivyo, mzee pale ana haki ya kusema kwamba mtoto wangu sitoweza kumpeleka kwa mtu mwenye tabia kama ile. Kwahiyo, mzee katika hali kama hiyo ni vyema kufanya hivyo kwa sababu ana upendo mkubwa na mwanawe, kwa sababu mwanawe hataki apate tabu kule anakokwenda. Kwa maana hiyo, suala hilo liko vyema katika hali kama hiyo, kuwa pale ambapo mzee anapoona kwamba mwanawe atakwenda kupata matatizo, basi sio tatizo mzee mwenyewe kukataa hilo. Nashukuru Mhe. Naibu Spika.

Nam. 46

Msamaha wa Kodi Katika Bidhaa za Mitumba

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Wizara ya Fedha inatoa msamaha wa kodi kwa wafanyabiashara ambao huingiza nguo zilizotumika (mitumba), ambayo mengine husafirishwa kwenye nchi nyengine kama Rwanda, Uganda, Congo na kadhalika.

(a) Je, ni kiasi gani cha kodi ambacho Wizara ya Fedha hutoa msamaha huo kwa wafanyabiashara wanaoingiza mitumba na baadaye kuisafirisha nchi nyengine.

(b) Je, upo utaratibu wa kubainisha kwamba wafanyabiashara hao hawafanyi udanganyifu kwa kuuza nchini nguo za mitumba ambazo tayari zimeshapatiwa msamaha wa kodi.

(c) Je, kuna hatua gani za kisheria ambazo zinastahiki kuchukuliwa kwa mfanyabiashara mwenye kuingiza mitumba ambaye baada ya kupatiwa msamaha wa kodi akauza nguo hizo hapa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali namba 46 lenye vipengele (a), (b) na (c) la Mhe. Mwakilishi naomba nitowe maelezo mafupi kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhamira ya kutanua shughuli za kiuchumi nchini, kwa makusudi serikali iliruhusu na kuanzisha shughuli za biashara ya mpito kwa maana ya (*transit trade)* kupitia maeneo ya Bandari Huru (*Freeport*), ambazo kama ilivyo kwa shughuli nyengine za uwekezaji, zinasimamiwa na Mamlaka ya Vitega Uchumi, *ZIPA*. Kwa mujibu wa sheria ya uwekezaji huu unastahiki kupata vivutio maalum, ikiwemo vya kutolipa baadhi ya kodi, ambavyo vimeorodheshwa kwenye Jaduweli la Sheria ya Uwekezaji, Sheria namba 11 ya mwaka 2004. Msamaha anaousema Mheshimiwa Mwakilishi, unaangukia katika vivutio hivyo na sio kwa Wafanyabiashara walio nje ya eneo la Bandari Huru.

Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swalila Mhe. Mwakilishi namba 46 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Bidhaa zinazoingizwa kwa utaratibu wa biashara chini ya Bandari Huru husamehewa kodi zote za uingizaji kwa maana ya (Ushuru wa forodha, Kodi ya Ongezeko la Thamani na Ushuru wa Bidhaa). Wawekezaji wanatakiwa kuzisafirisha tena bidhaa hizo nje ya nchi bila ya kuzilipa Ushuru na Kodi hizo. Hata hivyo, wawekezaji hao wanaruhusiwa kuuza hadi asilimia 20 ya bidhaa zao katika soko la ndani, lakini asilimia hiyo 20 hupaswa kulipiwa kodi zote zote zinazostahili.

(b) Utaratibu uliopo wa kubainisha udanganyifu ni wa usimamizi wa maofisa wa *ZIPA* na wale wa *TRA* ambao wapo katika eneo la Bandari Huru. Aidha, bidhaa kukaguliwa zinapoingia nchini na zinapotaka kusafirishwa na kuwekewa kumbukumbu. Aidha, kama ilivyo kwa maeneo mengine, usimamizi wa bidhaa hizi pia hufanyiwa ukaguzi;

(c) Hatua za kisheria zinazomstahikia mwekezaji anayeingiza nguo za mitumba, kwa utaratibu wa Bandari Huru na baadaye akaziuza nchini bila ya kulipia kodi, ni kulipishwa kodi yote inayostahiki ambayo aliikwepwa, lakini vilevile, hutozwa faini ya dola za Kimarekani 10,000 au pia bidhaa zake zote zinaweza kutaifishwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana. Nashukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa ruhusa ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri yenye ufafanuzi wa kina ambayo yametupa uelewa wa kuelewa pengine sisi tulikuwa tuna, nina hofu kwamba pana mitumba pengine naona mabeli yanaingia pengine tukawa tuna wasi wasi, lakini nilitaka niulize Je, wapo baadhi ya wawakezaji wazalendo ambao wanafanya biashara hii ya kuingiza hiyo bidhaa na baadaye kuipeleka nje.

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi: Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Kwa kumbukumbu tulizonazo Mhe. Naibu Spika, ni kampuni mbili ndizo zinazohusika na biashara ya mitumba hapa nchini, kampuni ya kwanza inaitwa Hakuna Matata, kampuni hii

ilisajiliwa kupitia usajili wa biashara inayofanywa katika bandari huru *(free port).* Vile vile, kuna kampuni nyengine inaitwa kampuni ya Savana ambayo kampuni hii ilisajiliwa na *ZIPA* na kuwekeza katika maeneo huru ya kiuchumi *(free economic zone)* pale Amani, kampuni hizi zote zilikuwa zinafanya kazi vizuri.

Lakini kampuni ya Hakuna Matata kutokana na kwamba walishindwa kutekeleza masharti ya uwekezaji kupitia bandari huru ya kwamba walikuwa hawafanyi sasa hii *transit free,* na kwa maana walikuwa wanaleta bidhaa zao na kuuza katika soko la ndani, kampuni hii imekuwa ikilipishwa kodi zote. Lakini kwa kampuni ya Hakuna Matata, kampuni hii ilikuwa inafanya vizuri na kwamba ilikuwa inauza ndani katika soko la ndani ile asilimia 20% inayoruhusiwa kisheria asilimia 80% ilikuwa inauzwa katika nchi za jirani na kwa namna hiyo basi ilikuwa ikitozwa kodi ile asilimia 20% tu.

Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba nilieleze Baraza lako kwamba hivi sasa tunafanya *assessment* ya kina, kwasababu zipo tuhuma za kwamba kampuni hii ya Savana haifanyi kama ilivyopaswa kufanya, kwa maana ya kwamba kuuza nje bidhaa zake asilimia 80% na 20% kuuza katika soko la ndani, sasa tunaifanyia *assessment* ya kina, ili kujua ukweli wake. Ikiwa sasa haifanyi kama inavyotakiwa kufanya kisheria nayo itabidi iondolewe katika usajili wa *ZIPA.*

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, mimi pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa dhamira njema ambayo anaendelea kutoa misamaha kwa yale maeneo tuliyomuwekea kisheria. Lakini pamoja na kufahamu kuwa Mhe. Waziri kwa uwezo wa msamaha wa kodi amepewa Waziri wa Fedha kisheria.

(a) Je, ni kiasi gani cha msamaha kilichowekwa kwa kila mwaka wa fedha kama kuna *ceilling* ambayo kawekewa Waziri wa Fedha au hajawekewa kabisa nilikuwa nataka kujua.

(b) Ni kiasi gani cha msamaha wa kodi kwa ujumla katika maeneo yote kilichotoka kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 hadi sasa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Ni kweli kabisa Waziri wa Fedha amepewa mamlaka ya kisheria ya kusamehe kodi na nimhakikishie kwamba kazi hiyo tunaifanya kwa umakini mkubwa na ushahidi wa hilo Mhe. Naibu Spika, ni kwamba katika mwaka 2015/2016 tulisamehe kodi yenye thamani ya shilingi bilioni 22, lakini mwaka 2016/2017 tumesamehe kodi ya shilingi bilioni 15.99. Kwahivyo, kuna upugufu wa asilimia 30% na tunaendelea na kasi hiyo hiyo, ili kuhakikisha kwamba kodi tunayoisamehe ni kwa ile miradi inayostahiki, miradi ya kijamii, taasisi za serikali lakini na wawekezaji walioruhusiwa kisheria.

Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 takwimu hiyo bado hatujaikamilisha lakini *trend* yetu ni kupunguza kama alivyosema tumepunguza kwa asilimia 30% katika kipindi cha mwaka 2015/na 2017.

Nam. 82

Ukosefu wa Huduma za *PBZ* Micheweni

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:

Serikali inastahili pongezi kwa kushirikiana na Benki ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)* kwa kuwaondolea wananchi usumbufu kwa kuwajengea benki katika miji na baadhi ya Wilaya kuwepo huduma hii karibuni wilaya zote Unguja na Pemba. Kwa kuwa bado kuna wilaya nyengine huduma hii haijapatikana na ni muhimu.

(a) Je, ni sababu zipi katika Wilaya ya Micheweni kutokuwepo kwa huduma hii japo tawi hadi leo.

(b) Je, serikali haioni kutokuwepo huduma hii kunarudisha nyuma maendeleo ya wananchi.

(c) Je, serikali haioni inawapa mzigo mzito wananchi wa Micheweni kufuata huduma hii Chake Chake na Wete kwa masafa marefu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 lenye vipengele (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:

Ni kweli kwamba serikali imekuwa ikichukua juhudi za kuimarisha upatikanaji wa huduma za fedha nchini hususan huduma za kibenki, lengo ni kumfikishia kila mwananchi huduma hizo. Benki yetu ya Watu wa Zanzibar *(PBZ)* ndio inayoongoza kwa utoaji wa huduma na kuwafikia wananchi walio wengi hapa Zanzibar.

Hata hivyo, kwenye ngazi ya Wilaya sio sahihi kwamba tayari huduma hizo zipo Wilaya zote za Unguja na Pemba isipokuwa Wilaya ya Micheweni. Usahihi ni kwamba kwa upande wa Pemba, tayari huduma hizo zipo katika Miji ya Mkoani, Wete na Chake Chake wakati kwa Unguja, huduma zipo katika Mji wa Zanzibar pekee. Ukiacha tawi la Mwanakwerekwe, *PBZ* haina matawi mengine zaidi ya Wilaya ya Mjini kwa hapa Unguja hivyo Wilaya zote za Mikoa ya Kaskazini na Kusini Unguja nazo hazina matawi ya Benki.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu kama ifuatavyo:

(a) Kama ilivyo kwa Wilaya za Kati, Kusini na Kaskazini "A" na "B" kwa Unguja, sababu kuu iliyoifanya *PBZ* kutokuwa na tawi kwa sasa katika Wilaya ya Micheweni ni uwezo wake mdogo kimtaji, hali ya kiuchumi na kibiashara kwa Wilaya hizo na ukaribu na urahisi wa kufikika matawi ya Benki katika Wilaya za karibu.

(b) Serikali inaelewa umuhimu wa huduma za fedha kwa maendeleo ya kiuchumi. Kwa upande wa Wilaya ya Micheweni, azma ya sasa ni kuanzia na angalau huduma za *ATM* na wakala wa benki, ili kuwasogezea wananchi huduma hizo muhimu.

(c) Kama nilivyokwisha kueleza, tatizo la kufuata huduma za Benki nje ya Wilaya sio la Wilaya ya Micheweni pekee na kwamba *PBZ* inachukua hatua maalum ya kusogeza huduma za msingi ndani ya Wilaya zisizokuwa na matawi. Tunaamini kuwa muda sio mrefu wananchi wa Micheweni nao watafaidika na ukaribu wa huduma za *ATM* na wakala wa benki kama nilivyoeleza.

Lakini zipo huduma nyengine ambazo zinatolewa za *Mobile Bank* kwa maana popote ulipo unawza uka- *access* huduma za fedha kupitia *Mobile Bank*, lakini vile vile masuala ya *Internet Bank* nayo yapo katika utaratibu mzuri hivi sasa.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameisemea serikali juu ya hali halisi ilivyo. Lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Waziri kwa kuwa wananchi kupitia Benki zetu za *PBZ* na *NMB* mara nyingi huduma hizi huchukuliwa wananchi kuweza kupata mahitaji yao, na kwa kuwa tumeshuhudia sasa wananchi huenda kulipia kwenye mabenki kwa ajili ya kupata mahitaji.

a) Je. huduma hii kwa Wilaya ya Micheweni lini itaanza.

b) Mara nyingi hupokea jawabu kama hizo kesho keshokutwa sasa kwa kupitia kauli hii kwa kweli wakati mwengine tunakuwa na masikitiko. Sasa je, ni lini wananchi wa Micheweni na wao watakuwemo katika hii huduma, ili waweze kupata yale mahitaji yao kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakari swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kama nilivyosema ni kwamba Benki ya Watu wa Zanzibar hivi sasa inaongeza huduma zake za *ATM* katika maeneo mbali mbali na tunakwenda awamu kwa awamu na hivi karibuni tumeshuhudia maeneo mengi mapya ambayo yamewekewa *ATM* ikiwemo *ATM* iliyofungwa katika eneo letu la Baraza la Wawakilishi.

Sasa nimjulishe tu Mhe. Ali Khamis Bakari asiwe na wasi wasi *ATM* itapelekwa pia katika eneo la Micheweni. Lakini pia huduma hizi tuwashawishi wananchi wetu waanze kutumia huduma za *Mobile* Bank, wakitumia ana simu yake ya Mkononi anaweza sasa kutumia huduma hii ya kuweza kutoa fedha zake kwenye account yake na kuzihaulisha katika mitandao mbali mbali M Pesa, Tigo Pesa, Ezy Pesa anaweza kutumia huduma hiyo akiwa kwenye kiganja chake cha mkono, pamoja na huduma hiyo *ATM* pia nimuahidi na wakala wa benki itakuwepo katika eneo la Micheweni si muda mrefu kuanzia sasa hivi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuuliza suala dogo la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri kwanza niipongeze sana *PBZ* kwa kuweka *ATM* kila nyanja na kila sehemu kwa Unguja na Pemba kwa kuwawezesha wananchi ili kupata huduma kiurahisi zaidi, lakini Mhe. Waziri katika jimbo langu Wesha Bandarini kuna ongezeko kubwa la watu hususan ikiwepo na hoteli ile ya *Misali Sunset*.

Je, ni lini kutawekwa *ATM* kule katika eneo la Wesha bandarini ili kuwaharakishia wananchi wa Ndagoni na Wesha kupata huduma hiyo, kiurahisi bila ya kwenda Chake Chake kutokana na masafa marefu yaliyokuwepo kule.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo.

Lengo la Benki ya Watu wa Zanzibar ni kuhakikisha kwamba huduma za kibenki zinawafikia wananchi wote ndio lengo, nilisema huko nyuma Benki ya Watu wa Zanzibar ilikuwa na matawi katika maeneo mbalimbali, lakini matawi yale kutokana na shughuli za kibiashara katika maeneo hayo matawi yale yalifungwa, kwasababu benki hii inafanya kazi zake kibiashara ni lazima ipate faida. Sasa eneo lolote ambalo shughuli za kibiashara zitaimarika, basi hicho ni kichocheo tosha kabisa kwa benki kufungua tawi au huduma zake nyengine zozote.

Sasa kama eneo hili la Wesha Bandarini lina wateja wengine na kwasababu shughuli za benki hii ni shughuli za kibiashara, basi tumelisikia hilo tunalipokea na benki itafanya tathmini yake na ikiona kuna haja ya kuweka *ATM* katika eneo hilo, haitosita kufanya hivyo. Kwahivyo, ningemuoba Mhe. Mjumbe atulie watu wa benki watafika katika maeneo yote hayo kwasababu tulisema *ATM* zitawekwa katika maeneo yote yenye mvuto wa kibiashara awamu kwa awamu na muda ukifika katika eneo hili la Wesha Bandarini nalo litawekewa *ATM*.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, minong'ono imezidi hatuelewani humu ndani, naomba sana mpunguze minong'ono. Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Nam. 35

Matokeo ya Sera Mpya ya Elimu

Mhe. Miraji Khamis Mussa - Aliuliza:

Wizara ya Elimu iliacha kutumia Sera ya *Zanzibar Education Master Plan (ZEMAP)* na kutumia sera mpya ya *Zanzibar Education Development Plan (ZEDP)* ambayo tunaendelea nayo hadi sasa.

(a) Je, ni sababu zipi ukiachilia mbali umri wa kuanza na kumaliza skuli, zilizopelekea kutumia sera hii mpya, wakati ambapo ubora wa elimu umeshuka *(Quality of Education)* kwa kiwango kikubwa sana.

(b) Baada ya kutumia sera mpya, kuna utafiti uliofanywa na Wizara na umetoa matokeo gani, na kama kulikuwa na changamoto, hatua zipi zilichukuliwa na Wizara kuboresha matokeo hayo.

(c) Kuna programu ngapi zilifanyika za kuwajengea uwezo walimu na kuwawezesha kuikabili sera mpya, na walimu wangapi Unguja na wangapi Pemba waliopatiwa mafunzo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Zanzibar Education Master Plan (ZEMAP) ni Mpango Mkuu wa Elimu wa muda wa miaka kumi uliotekelezwa kuanzia mwaka 1996 hadi mwaka 2006. Baada ya mpango huo kumaliza muda wake, wizara iliufanyia tathmini na baadae iliandaa Mpango mwengine uliokidhi matakwa ya Sera ya Elimu ya mwaka 2006 na *MKUZA I*. Mpango huo uliitwa *Zanzibar Education Development Plan (ZEDP)* wa mwaka 2008 hadi 2016. Mpango huo hivi sasa umemaliza muda wake na umefanyiwa tathmini. Hivyo *ZEMAP* na *ZEDP* sio sera bali ni Mipango na Mikakati ya Maendeleo ya Elimu ya Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Sera za Nchi. Mipango ya Elimu inaandaliwa kwa kila kipindi ili kulingana na mahitaji ya nchi na wakati wa kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Baada ya maelezo hayo sasa najibu kama ifuatavyo:-

(a) Sera ya Elimu ya mwaka 2006 iliandaliwa kwa sababu zifuatazo:-

(i) Kulingana na kuowanisha na utekelezaji wa malengo ya Kitaifa na Kimataifa kama vile MKUZA II, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020, Malengo ya Elimu kwa Wote na Malengo ya Milenia *(MDGs).*

(ii) Kukabiliana na changamoto za ushindani wa soko la ajira la kimataifa na katika Jumuiya za kikanda kama vile Jumuiya ya Nchi za Afrika ya Mashariki, ambapo elimu imekuwa na nafasi pana ya kuandaa vijana na ajira.

(iii) Kukabiliana na changamoto za janga la maradhi ya UKIMWI, ambalo sera iliyopita ilikuwa haiyongozi katika jitihada za kukabiliana na maradhi hayo.

(iv) Kuimarisha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kama ni vyanzo muhimu ya kufundishia na kujifunzia na kuwapatia vijana fursa ya kujiajiri au kuajiri katika soko kubwa la *TEHAMA*.

Mbali ya umri wa kuanza na kumaliza skuli, Sera ya Elimu ya mwaka 2006, iliagiza kuimarishwa kwa mafunzo ya ualimu kwa kuviweka Vyuo vya Uwalimu chini ya uongozi na usimamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, ili kuimarisha ubora wa elimu ya walimu.

(b) Kama nilivyotangulia kueleza, tafiti mbalimbali zilifanyika kutathmini utekelzaji wa Sera ya Elimu kupitia Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Elimu Zanzibar *(ZEDP).* Tafiti hizo

ni kama vile tathmini ya Utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Elimu wa Zanzibar (*ZEDP I*), uchambuzi wa hali halisi ya Elimu ya Zanzibar *(Zanzibar Education Situation Analysis),* tafiti kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya elimu kwa wote (*EFA 2015),* utafiti kuhusu ajira na mgawanyo wa walimu katika ngazi ya sekondari pamoja na tathmini ya kupima uwezo wa wanafunzi wa msingi katika kujuwa kusoma kuandika na kuhesabu *(SACMEQ).* Tafiti zote hizo zimeonesha mafanikio makubwa ya kielimu kwa upande wa uandikishaji na mafunzo kwa walimu. Pia, kasoro zilijionesha katika kuinua ubora wa elimu hasa katika kipengele cha ufaulu wa wanafunzi.

Kuhusu tathmini ya Sera ya Elimu, wizara imeunda kikundi kazi cha maafisa wa wizara, mashirika yasio ya kiserikali na wataalamu wastaafu ili kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ya mwaka 2006 na kupendekeza mabadiliko yake. Kikundi kazi hicho kitakutana na wadau mbalimbali wa elimu, ili kupata mawazo yao ya namna ya kuimarisha Sera ya Elimu ya mwaka 2006.

(c) Katika kuhakikisha kuwa walimu wana uwezo wa kukabili utekelezaji wa Sera mpya ya Elimu, Wizara iliendesha *programs* mbalimbali na endelevu za mafunzo kwa walimu. *Programs* hizo ni kama hizi zifuatazo:-

(i) Programu ya uwasilishaji wa Sera ya Elimu kwa walimu ambayo ilifanyika kwa walimu wote wa Unguja na Pemba, wakiwemo walimu wakuu, wasaidizi walimu wakuu pamoja na walimu wanaosomesha skuli za binafsi. Uwasilishaji huo, uliambatana na usambazaji wa sera hizo katika skuli zote za Unguja na Pemba.

(ii) Programu ya Mafunzo ya walimu ambapo jumla ya walimu 422 wa skuli za maandalizi (262 Unguja na 160 Pemba) walipatiwa mafunzo juu ya mbinu za ufundishaji katika ngazi ya elimu ya maandalizi. Aidha, walimu 3,510 (2,148 Unguja na 1,362 Pemba) wa skuli za msingi darasa la kwanza hadi la sita walipatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mitaala mipya iliyoanzishwa kuendana na mfumo mpya wa elimu ya msingi ya miaka 6.

Vilevile, mafunzo yalitolewa kwa walimu wote wa wanaosomesha madarasa ya tano na sita juu ya matumizi ya Lugha ya Kingereza katika kufundishia. Pia programu za mafunzo ya sayansi zilitolewa kwa walimu wote wa sekondari kwa Unguja na Pemba.

(iii) Programu ya Mafunzo ya walimu kuhusu matumizi ya viwango vya kujifunza kwa wanafunzi *(achievement standards),* ambapo jumla ya walimu 10,997 kati ya hao (7,380 Unguja na 3,617 Pemba) walipatiwa mafunzo. Ahsante

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, lakini pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake marefu sana yenye changamoto ndani yake. Pamoja na hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza suali dogo tu lenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa wanafunzi wanaomaliza darasa la sita wengi wao hawana uwezo wa kufikiri kimantiki kama ilivyotarajiwa. Ni lini wizara itafanya mapitio ya sera hii ikiwezekana wizara ifanye maamuzi sahihi ya kurudisha mfumo wa zamani.

(b) Katika nchi za Afrika Mashariki zenye hali nzuri ya watu wake katika soko la ajira moja wapo ni Kenya ambapo haina mfumo wa elimu uliosawa kama wetu. Je, ni vigezo gani vilivyotumika kuona kwamba mfumo wa elimu tulionao na unaotumika hivi sasa utatuvusha katika changamoto za ushindani wa soko la ajira kama ambavyo nilivyokunukuu katika majibu yako. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Naibu Spika, nimetanguliza kusema hivi sasa Wizara ya Elimu imeunda Kikundi Kazi, kwa ajili ya kuifanyia mapitio Sera ya Elimu ya mwaka 2006. Wizara imelazimika kuunda kikundi hichi kutokana na maoni mbalimbali ambayo yanatolewa na wadau. Kwa hivyo, tusubiri matokeo ya utafiti huu ndiyo yatakayotuonesha njia sahihi kama njia tunayofanya tuko sahihi au tumekosea. Pale ambapo tutakapoona tumekosea basi utaratibu wa kawaida utatumika, ili kuona kama tunakwenda sawa.

Lakini, kwa maoni ya wizara ni kwamba mfumo tuliyouwekwa kwa kweli ni mfumo bora kielimu na ndiyo unaofuatwa na nchi nyingi kabisa duniani. Suala muhimu ni kuweza kuimarisha ubora wa elimu, siyo lazima kurejesha mfumo wa miaka saba, minane katika elimu ya msingi, ulazima ni kuweza kutoa elimu bora na hii ndiyo changamoto ambayo wizara tunakabiliana nayo hivi sasa.

(b) Kuhusu vigezo ambavyo tulitumia katika kuweka mfumo huwo, kwanza nataka ieleweke kwamba mfumo huu ulitokana na mawazo ya wadau mbali mbali kwa Zanzibar,wananchi tofauti waliulizwa kuhusu mfumo huu. Mfumo huu sio suala la maamuzi ya wizara na serikali hapana, umetokana na *data* zilizokusanywa kwa wananchi mbalimbali ambao waliona kwamba mfumo huu unaweza kuwa njia moja sahihi ya kutupeleka mbele katika sehemu ya elimu.

Lakini pia ulitokana na tafiti nyengine zilizofanywa nje ya Zanzibar, nje ya Tanzania, ili kuona mifumo kama hii inafanya kazi kwa kiasi gani. Imani yetu kwamba mfumo huu unaubora wake na zile changamoto ambazo zinajitokeza tutazipatia ufumbuzi kadri hali itakavyowezekana. Lakini kubwa zaidi tunajaribu kuyafanyia mapitia matamko mbalimbali ya sera hii. Ahsante sana.

Nam. 88

Mpango wa Kuyapima Maeneo kwa Ajili ya Malisho ya Mifugo

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:

Katika hotuba ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli ya ufunguzi wa Uwanja wa Ndege huko Kagera, Bukoba alisema kuwa atahakikisha kuwa mifugo anaisajili yote na kulipima eneo maalum, kwa ajili ya mifugo hiyo na sio tu kuzurura ovyo na iwe na eneo maalum la malisho. Kwakuwa Zanzibar suala hili bado ni kero kwa jamii na mifugo ipo kila eneo na kupelekea usumbufu kwa baadhi ya sehemu.

(a) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango gani wa kuyapima maeneo maalum, kwa ajili ya malisho ya mifugo.

(b) Je, lini serikali itatoa elimu juu ya suala la uwekaji wa eneo la malisho hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 88 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, hadi sasa hapana maeneo maalum ambayo yanatumika kwa kulishia mifugo pekee kutokana na udogo wa visiwa vyetu. Hatahivyo, wafugaji wanashauriwa kufuga idadi ndogo ya mifugo yenye tija kwa njia ya kutumia mabanda *(Zero grazing).*

(b) Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara inaendelea kuhamasisha wafugaji wafuge kisasa ikiwa ni pamoja na kutoa taaluma ya upandaji wa majani ya malisho katika maeneo wanayofugia ambayo yanamilikiwa na mfugaji mwenyewe. Vilevile, taaluma ya uhifadhi na utumiaji wa masalia ya mpunga baada ya kuvunwa inatolewa kwa lengo la kutumiwa majani hayo makavu wakati wa kiangazi ambapo majani mabichi yanakuwa adimu. Serikali inatoa wito kwa wakulima kutokuyachoma moto masalia ya mpunga, ili yatumiwe kwa chakula cha mifugo wakati wote**.** Ahsante.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize suali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a. Ni wafugaji wa maeneo gani katika visiwa vya Unguja na Pemba ambao wizara yako imewapatia huwo ushauri.

b. Ufugaji wa kisasa kwa wakulima wengi katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba unahitaji gharama. Je, wizara yako imejipanga vipi kuwasaidi wakulima au wafugaji wadogo wadogo, ili kuingia katika mfumo huwo wa ufugaji wa kisasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi majibu yake ya nyongeza kama ifuatavyo.

Ni wafugaji wa maeneo tofauti wakiwemo Machui kwa Kaskazini na kwa Pemba ni maeneo tofauti yapo ambao tumewapa maelezo hayo. Vile vile Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba tunashauri wafuge mifugo hii kwa *zero grazing* sio kwamba labda kuna mbegu maalum, hata yule ng'ombe ambaye ni wa *local* tunashauri kwamba umuingize kwenye banda uwe

unamtayarishia chakula chake na maji yake, ili aweze kutoa maziwa zaidi na kilo ziongezeka zaidi, unapomuachia ngombe akenda akazunguka na kutafuta chakula ile peke yake inampelekea ng'ombe kupungua kwa uzito na maziwa vile vile kupungua kama uzalishaji.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa majibu mazuri sana aliyoyatoa naomba niongezee kutokana na masuali mawili ya nyongeza.

(a) Mhe. Naibu Spika, kwanza tulikuwa tuna mpango wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe mpango huu unawasaidia wafugaji wasiopungua 2000. Kwahivyo, kila *group* moja la watu 30 wanapewa ng'ombe na wanafuga ng'ombe na moja katika taaluma wanazopata ni taaluma za kuweza kupanda majani na kufanya *zero grazing.* Huu ni mpango wa serikali na ulikuwa unaendelea kwa bahati mbaya sasa hivi umemalizika lakini tunaanza kuufanyia mpango mpya ili kuweza kuwapa taaluma wafugaji.

(b) Mhe. Naibu Spika, pili tumetumia vyombo vyetu vya habari na vichapisho mbalimbali kwa kuwaelimisha wananchi kwamba suala la kuchunga ng'ombe kwa utaratibu ule wa zamani hauwezi kusaidia katika visiwa vyetu. Naukiona sasa hivi tumeanza na ugomvi baina ya wakulima na wafugaji, kwa sababu wafugaji wengi wanafugia kwenye mashamba ya wakulima kuweza kulishia mifugo yao.

Kwa hiyo, tumetoa taaluma hizo kwa kupitia vipindi mbali mbali na tunaomba kutumia fursa hii kuwaomba sana wafugaji waheshimu na watumie mabakia ya mpunga, ili yasaidie sana katika kulisha ng'ombe na waendelee katika kutoa utaratibu wakulima wa *zero grazing,* ili kupunguza matumizi makubwa ya ardhi ambayo hatunayo sasa hivi.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kuzingatia umuhimu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imeundwa rasmi kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanatafuta mifugo mingi, ili kuweka katika nchi yetu ili kuondoa kero la ukosefu wa kitoweo. Lakini, kwa bahati katika jibu lilojibiwa hapa tumeambiwa kwamba wafugaji wanashauriwa waweke ng'ombe kidogo tu kwa kuwa hatuna maeneo ya kuhifadhi au kulisha wanyama hao.

Je, hivyo wizara imezingatia kitu gani juu ya kusema kwamba wafugaji wetu wawe na ng'ombe kidogo kwa kuwa maeneo ya kulisha hatuna. Kuna utaratibu gani wa kutafuta maeneo maalum kuhakikisha kwamba katika zoni hii wakulima mbalimbali watakuwa wanyama wao wanafunga kwa ajili ya malisho, ili tuhakikishe kwamba ng'ombe wanaongezeka katika nchi yetu na kuondoa shida ya kuagizia ng'ombe kutoka Bara.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Waheshimiwa Wajumbe, tujue kwamba hapa visiwani kwetu tofauti na Bara, Bara wana eneo kubwa na wanaweza kulitumia wanavyotaka. Lakini kwa hapa sisi visiwani eneo letu ni dogo, eneo hilo hilo tunataka kulima, eneo hilo hilo tunataka kuchimba mchanga, eneo hilo hilo tunataka tutengewe kwa ajili ya kufuga. Kutokana na hali hiyo, ndio maana kama Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi tukashauri uwepo ufugaji wa aina hii, sio kama hatutaki kujitosheleza na nyama au hatutaki kuwa na mifugo mingi. Tunahitaji kuwa mifugo mingi lakini tunashauri hivi, ili tuweze kupata wale ng'ombe kuwa na uzito zaidi kuweza kupata nyama na kuweza kupata lita nyingi za maziwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Nam. 92

Ujenzi wa Mabwawa Ndani ya Hifadhi ya Misitu kwa Ajili ya Wanyama

Mhe. Ali Khamis Bakari - Aliuliza:

Serikali inastahili pongezi kwa kusimamia vyema suala zima la utalii na pia kusimamia vyema maeneo ya hifadhi kwa kutunza misitu na kuwalinda wanyama pori waliomo ili wasitoweke. Na kwakuwa wanyama hao hutumia rasilimali zilizomo ndani ya msitu wakati wa ukame tumeona maji hukauka na maziwa yote hutoweka.

Je, serikali ina mpango gani wa kujenga mabwawa maalum katika sehemu za msitu, ili wanyama waweze kupata maji.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 92 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni kweli wanyama wanaoishi porini hutegemea maji kwa namna moja ama nyengine katika maisha yao. Hatahivyo, wapo baadhi ya wanyamapori hunywa maji kuondoa kiu hasa wakati wa jua na joto kali. Wapo baadhi ya wanyama pori wengine hutumia maji yaliyotuama au yanayotiririka kwa mawindo na wengine ni kama sehemu ya makaazi yao au kupumzika na kupunguza joto katika miili yao.

Mhe. Naibu Spika, si wanyamapori wa aina zote wanaohitaji maji ya kunywa moja kwa moja ili waweze kuishi, isipokuwa hupata maji kutoka katika majani au matunda ya miti, mfano wa wanyama hawa ni Paa, Kimapunju, Komba na Popo. Aidha, wanyamapori wanaokula nyama ndio wanaohitajia kunywa maji zaidi kulinganisha na wanaokula majani au matunda, mfano Chui, Cheche, Ushundwi, Kitu na Ngawa.

Mhe. Naibu Spika, Wizara yangu haina ushahidi unaothibitisha upotevu wa wanyama pori kutokana na ukosefu maji. Hatahivyo, wizara italifanyia utafiti ili kuchukua hatua zinazofaa.

Mhe. Naibu Spika, wizara imeupokea ushauri huu, na inazingatia faida nyingi zitakazopatikana iwapo ujenzi wa mabwawa utafanyika kwani utasaidia watalii kuwaona baadhi ya wanyamapori

wanaopendelea kunywa maji katika maeneo ya mabwawa, hususan nyakati za kiangazi. Mabwawa haya yatasaidia sana shughuli za utafiti na ugunduzi wa baadhi ya wanyama ambao si rahisi kuwaona katika hali ya kawaida. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize suali moja la nyongeza. Ni lini utafiti huwo utafanywa kwa kuwa ni dhahiri kuwa kuna athari inayoendelea kupotea kwa baadhi ya wanyama pori hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu swali lake Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Kama nilivyosema utafiti ufatanywa, ila siwezi kukwambia tarehe ngapi, wala siwezi kukwambia lini, kwa sababu unapofanya utafiti ni gharama na kama hujakipangia bajet kitu kama hichi huwezi kukifanya. Kwa hivyo naomba Mhe. Mwakilishi awe na subra utafiti utafanywa na badala yake majibu yake tutawaletea hapa Barazani. Ahsante sana.

Nam. 72

Gharama za Matibabu kwa Wagonjwa Wanaopelekwa India

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa Wizara ya Afya inawapeleka wagonjwa wa maradhi mbalimbali nchini India kwa ajili ya matibabu, jambo ambalo linagharimu serikali fedha nyingi sana. Wagonjwa wanaopata huduma hii sio hata nusu ya wagonjwa ambao wanaomba na ambao kweli wanastahiki kupatiwa fursa hiyo ya kwenda kwenye tiba nchini India.

a) Je, wizara ina mpango mbadala wa kuwaleta nchini madaktari bingwa kutoka India kuja kutibu hapa Zanzibar, ili kupunguza gharama na wagonjwa wengi watapata kutibiwa kulikoni kutumia fedha nyingi kuwasafirisha na kuwatibu wagonjwa wachache.

b) Je, wizara inafanya utafiti wa hesabu, kwa ajili ya kugundua njia rahisi kati ya kuwasafirisha wagonjwa na kuwaleta madaktari hapa nchini kwetu.

c) Je, kwa kipindi cha 2016/2017 wizara iliwasafirisha wagonjwa wangapi na wizara ilitumia kiasi gani cha fedha, ili kuwahudumia safari na matibabu ya nje wagonjwa wetu.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu:

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote kuwepo hapa tukiwa na afya njema na wazima.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 72 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza kwa pamoja na baadaye kidogo nitaomba nitoe ufafanuzi wa ziada kutokana na jibu lililoandikwa katika majibu yaliyowasilishwa.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya kila mwaka inaratibu kambi mbali za wataalamu wa Afya kutoka nchi mbalimbali ikiwemo, China, Marekani, Saudia Arabia, Israel, India, Pakistan, Norway na nchi nyengine nyingi. Kambi hizi zinatibu wagonjwa wengi wenye matatizo mbalimbali na kwa kiasi kikubwa inapunguza mzigo mkubwa sana kwa kusafirisha wagojwa nje ya nchi. Aidha, tathmini halisi ya wagonjwa tayari imeshafanyika kwa vile maradhi hutokea ya aina nyingi tafauti na mengine hutokea kutokana na tabia zetu za kutokwenda kupima afya zetu kila baada ya miezi sita, wataalamu wanatwambia tukifika miaka 40 unatakiwa kila baada ya miezi sita tunatakiwa kila baada ya miezi sita tuwe tunakwenda kupima afya zetu, kama vile gari inavyopelekwa gereji kwenda kufanyiwa *service* na kubadilishwa *oil* na mambo mengine.

Kwa mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya shilingi bilioni 6.95 zilitumika kuwasafirisha wagonjwa jumla ya 270 kwenda nje ya Tanzania kupatiwa matibabu, hii siyo India tu na nchi nyengine mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako nitaomba kidogo nitoe ufafanuzi wa ziada kutokana na jibu fupi lililokuwa limeandikwa.

Tayari wizara kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali imeleta madaktari hapa nchini kutoka nchi tafauti kuja kufanya kambi ambazo zimeweza kusaidia sehemu kubwa sana ya kutoa matibabu. Kwa mwaka huu jumla ya madaktari 140 wamekuja Zanzibar kutoka nchi tafauti na kutibu maradhi mbali mbali. Nitatoa mifano michache tu ya kambi hizi ambazo zilifanyika hivi karibuni, kambi ya macho, pua, koo na masikio zilifanyika Mnazi Mmoja ambao wagonjwa 144 waliyokuwa wasafirishwe kenda nje ya nchi waliweza kupata tiba.

Mnamo Mwezi wa Oktoba kisiwani Pemba madaktari 32 walitokea nchini Saudia Arabia, ambapo waliweza kuwafanyia *operation.* Akina mama wenye maradhi ya kike ikiwemo na saratani ya shingo ya kizazi, akina mama 283 ni kambi kubwa kabisa ambayo ilifanyika kisiwani Pemba, walifanyiwa *operation* ambao wengine waliweza kutolewa mayoma na *fibroids* zilizofikia kilo 2.8 haijawahi kutokezea hata hao madaktari wenyewe kidogo walishangaa. Kwakweli, baadhi yao walikuwa wakiyafuga yale maradhi na kukaa nayo kwa kipindi kirefu sana bila ya kujitokeza kwenda hospitali, lakini madaktari hao walipokuja waliweza kupata huduma hizo.

Mhe. Naibu Spika, zilifanyika *operation* 78 za saratani ya shingo ya kizazi na kuweza kuokoa maisha ya watu huko kisiwani Pemba. Mnamo mwezi wa Juni 2017 timu ya madaktari bingwa kutoka *Health Bergen Hockland University* ya Norway walifika Zanzibar na Pemba na kufanya *operation* za maradhi mbalimbali hususan maradhi ya akina mama pamoja na kutupatia vifaa na dawa ambazo walizibakisha. *(Makofi)*

Naomba niseme kwamba gharama kubwa tumeweza kuokoa kwa kambi hizi moja kwa moja. Kwa mfano, tiba ya saratani kwa kutumia miyonzi ni ghali sana hiyo yaiwezi kufanyika Zanzibar na sio kuwa madaktari tu bali na vile vifaa vyenyewe vinahitajika. Nitatoa mfano mdogo sana kwa mashine ya *MRI* iliyonunuliwa kwa pale Mnazi Mmoja mashine ile gharama zake jumla ni bilioni 2.5 mashine moja, ambayo sasa hivi tunaitumia na inatusaidia sana, ili kuokoa kabisa tusipeleke wagonjwa nje basi panahitajika mashine zaidi ya 20 nyengine mbali mbali zenye gharama kama hizo.

Naomba Mhe. Naibu Spika niseme kwamba wagonjwa wengi wanaosafirishwa kwenda nje, ni wale ambao tiba zao ziameshindikana kabisa hapa Zanzibar kupitia kambi mbalimbali, na wagonjwa hao hupitishwa kwa sheria maalum iliyokuwa chini ya Sheria ya Baraza la Madaktari la Zanzibar, ambao hupelekwa kwenye Bodi Maalum ya Madaktari Bingwa wote hukaa kwa pamoja na husema kwamba mgonjwa huyu ameshindikana kupatiwa matibabu hapa Zanzibar.

Hatupeleki nje ya nchi tu bali wagonjwa wengine huwa tunawapeleka Muhimbili wengine tunawaapeleka *MOHAS* Hospitali ya Chuo Kikuu cha Muhimbili, Jakaya Mrisho Kikwete *Heart Institute* yaani Taasisi ya Maradhi ya Moyo ya Jakaya Mrisho Kikwete iliyopo huko Dar-es-Salaam, *Ocean Road Cancer Institute* - Taasisi ya Saratani iliyoko *Ocean Road* pamoja na baadhi ya Hospitali *KCMC* kule Moshi.

Ufafanuzi wa kipengele cha (b) wizara tayari ilishafanya utafiti mkubwa tokea mwaka 1992 pale Dkt. Ali Mohamed Shein hivi sasa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipokuwa kiongozi wa wizara hii ya afya, yeye ndiye alilofanya utafiti huo wa mwanzo na kuandika waraka rasmi ambao hadi leo hii ndio waraka wake tunautumia. *(Makofi)*

Wizara kupitia uongozi wakati huo wa Dkt. Ali Mohamed Shein, iliweza kubuni njia mbadala za kupunguza gharama za kuwapeleka wagonjwa nje kwa kuanzishwa vitengo vipya mbalimbali vya kutibu maradhi makubwa, ambapo hapo awali wagonjwa hawa wote walikuwa wakipelekwa nje ya nchi. Mafanikio hayo ya Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar tokea wakati huo ndio waliopelekea kwa vitengo vipya kuanzishwa hapa Zanzibar vikiwemo vitengo vya *NEURO* yaani Kitengo kile cha Mishipa ya Fahamu, Vichwa Maji, Saratani ya Ubongo ambayo tunaifanya hivi sasa Zanzibar hatupeleki tena wagonjwa nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, vyote hivyo vimeanzishwa chini ya uongozi wake moja kwa moja, kwa Kitengo cha Mishipa ya Fahamu hadi leo nimeangalia leo asubuhi tumeweza kuokoa jumla ya shilingi bilioni 6,000,000,000/= za kitanzania tokea kitengo hicho kianzishwe, Kitengo cha *NEURO* kile kilichokuwepo pale Mnazi Mmoja ambacho kinashirikiana na wenzetu kutoa *Spain*.

Serikali pia iliweza kuanzisha Kitengo cha Dialysis ambacho kina mashine tano zinazofanya kazi.....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Afya, jibu lako limekuwa refu mno unaonekana umalizie...

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante. Kwa hiyo, utafiti huo uliweza kupelekea kuokoa hadi leo jumla ya shilingi bilioni 10,000,000,000 zimeweza kuokolewa. Kutokana na hali hiyo, hivi sasa ndio maana orodha imepungua hapo awali tulikuwa tukipeleka zaidi ya wagonjwa elfu moja kwa mwaka kwenda nchini India na kwengineko, lakini hivi sasa tumeweza kupunguza hadi kufikia wagonjwa 270 naomba kuwasilisha Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri ambayo yametoa ufafanuzi imetoa mwelekeo. Lakini naomba kuuliza kwa kuwa

wizara ilitumia shilingi bilioni 6,953,972,810/= kwa kuwasafirisha wagonjwa 270 kupata tiba nje ya nchi.

(a) Je, wengi wa wagonjwa waliopelekwa kutibiwa walikuwa wanasumbuliwa na maradhi gani hasa hata ikapelekea kwamba 270 wapelekwe nje ya nchi na nchi gani hizo walizopelekwa.

(b) Ni nini muelekeo na wito wa wizara kuhusiana na wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi kwa ajili ya kutibiwa ambao kwenye hayo maradhi mengi yaliyogunduliwa. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika naomba hili swali la pili alirudie kidogo sijalipata.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nilitaka kujua wito wa wizara kwa wale wagonjwa wengi ambao wanasumbuliwa na yale maradhi, maana yake kama watu wa moyo, pengine wana utaratibu, wana maelekezo, ili kupunguza hayo maradhi kwa wizara. Wizara wito wao ni upi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Maradhi matatu makuu yalioongoza kwa kupeleka wagonjwa India kwanza kabisa ni maradhi ya moyo wale ambao wanafanyiwa *operation* ya moyo pamoja na kufanyiwa *stanting* au kutiwa *post marker* na kusafisha mishipa ambayo imefanya *blockage* imekwama damu hayo ndio ya kwanza kabisa.

Pili, ni maradhi ya saratani ambayo yanaongoza na la tatu ni maradhi ya figo hasa wale wanaohitaji kubadilishwa figo na kuwekwa figo jengine, hilo bado hatujaweza kulifanya hapa kwetu hiyo inabidi anakwenda India.

Wito kwanza kuna utaratibu maalum wa kupelekwa wagonjwa, mgonjwa lazima anapelekwa na daktari wake ambaye aliyeshindwa kwenda kwenye bodi hawezi kwenda moja kwa moja mgonjwa kwenye bodi, lazima awe ameshaonana na daktari wa kwake kwanza halafu daktari bingwa, halafu ndio anapelekwa kwenye bodi, na utaratibu wa kusafirisha mgonjwa ndio unaofuata.

Mhe. Naibu Spika, wito kwetu sote la kwanza kabisa ni kufanya kitu kinaitwa *check up* kuangalia afya zetu. Wataalam wanatwambia unapofikia miaka 40, naamini wengi wamefikia miaka hii, ni wachache ambao hawajafikia miaka 40, unatakiwa angalau mara mbili kwa mwaka uende kufanya *check up*. Lakini kuna ile *check up* ya kawaida ya kila mwezi mfano kuangalia *pressure* yako, kuangalia *cholesterol level*, kuangalia sukari na kadhalika, ili kuweza kugundua mapema.

Mara nyingi hata India wamekuwa wakilalamika wakituandikia barua kadhaa, mara nyingi tukipeleka wagonjwa wetu kule nchini India wanakuwa nusu wafu yaani, mtu ameshaathirika tunampeleka nusu maiti.

Wanatuambia wagonjwa tukiweza kuwawahisha kwenda mapema, basi tutaweza kuokoa maisha ya wengi zaidi, na hili linawezekana kwa wananchi kujitokeza pale tunapoweka kambi zetu za kupima afya.

Lakini la pili kubadilisha tabia zamani tunakumbuka wazee wetu sehemu ndogo ama kubwa anakwenda kwa baiskeli au kwa miguu, sasa hivi sisi sehemu ndogo kabisa tunakwenda kwa gari kitako cha humu ndani kukaa kirefu, kikubwa, viti vyenyewe ndio hivyo tena, maradhi ya migongo mingi sana na viungo ...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Afya, kuna maswali mengine yanakuja.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, wito ndio huo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye ufasaha zaidi. Vile vile niipongeze serikali kwa kuwajali wananchi wake kwa kuweza kuwapeleka matitabu na kuweza kutumia fedha kama hizi za serikali.

Katika majibu yake amesema kwamba katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 jumla ya fedha bilioni 6.8 zimetumika na kwenda katika nje ya nchi ya Tanzania kwa matibabu. Je, ni nchi gani na gani waliosafirishwa wagonjwa hao na kwenda kwenye matibabu katika wagonjwa hao 270.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Nchi waliopelekwa wagonjwa wengi 266 walipelekwa nchini India ambao tuna mikataba na hospitali tatu nchini India, hao wachache waliobakia walipelekwa nchini South Africa na wawili nchini Kenya Nairobi. Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini ametaja hapa *figure* mbali mbali zilizo-*save* katika kupeleka wagonjwa nje, ni matumaini yangu moja ni Kitengo cha *NEURO*.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri Kitengo cha *NEURO* kama sikosei ni kitengo kinachofadhiliwa na wazungu kutoka nadhani *Denmark* kama sikosei au *Sweden* na wazungu hawa wameshachoka kwa sababu wamekuwa wanaambiwa uongo katika kupewa msaada mbali mbali, kwa mfano nyumba, hata *visa* na mambo mengine wanatumia pesa zao nyingi.

Kwa kweli wazungu hao wanataka *withdraw project* yao ya *NEURO* hapa Zanzibar, kwa sababu mfano Uganda juzi wamepewa nyumba na kila kitu, hapa wameomba kwa muda wa miezi sita mpaka mwaka hawajapewa *visa* wala pa kukaa yaani, hawajapewa chochote na wanaisaidia nchi katika kutibu maradhi mbali mbali ya *NEURO* na mabilioni chungu nzima.

Swali langu. Je, wazungu hawa anawatambua na ana mchango gani wa kuweza kuwasaidia kwa sababu wameshachoka na wameshasema wana *withdraw project* yao wanadanganywa. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi.

1. Ni kweli tuna mkataba wa mashirikiano baina yetu sisi pale *NED* yaani *Neuro Surgical Education Development Institute* ile ni taasisi kama zilivyokuwa nyengine za *MOI* na JK ambayo iko pale Mnazi Mmoja. Tunao mkataba wa mashirikiano na wao na nchi yenyewe ni *Spain*. Mhe. Naibu Spika, ninaomba pia nimueleze kwamba katika mkataba huo wao tumekubaliana kuna sehemu ya ufadhili wanatoa wao lakini sehemu nyengine ya ufadhili tunatoa sisi. Kwa mfano, jukumu la maji, umeme, mishahara ya wafanyakazi wale wote kutoka hapa Zanzibar wa Wizara ya Afya tunalipa sisi pamoja na gharama nyengine za uendeshaji, gharama za vifaa na mashine za ku-*test* pamoja na *operation* wanalipa wao.

2. Barua yao ya *visa* hivi karibuni nime-*sign* na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto atakuwa shahidi kwa sababu huwa zinapitia pia kwake kupatiwa kibali cha kazi.

3. Mashirikiano yetu yapo karibu sana, naomba niseme taarifa hivi kwamba wanataka kuvunja mkataba si kweli kwani hivi juzi tu tumepata *accreditation* ya hali ya juu kabisa yaani, kituo kile kutambulikana katika Afrika ya Mashariki na Kati kwa kutoa mafunzo na kufanya *operation*. Kwa hiyo, kitu hicho sasa hivi kimekuwa sio cha Zanzibar tu isipokuwa kimekuwa kinatambulikana Afrika Mashariki na Kati na watu mbali mbali wanakuja kutoka Mombasa, Nairobi, Dar-es-Salaam kupata matibabu pale na wanafunzi wao kupata mafunzo pale.

Kwa hiyo, mkataba wetu Mhe. Naibu Spika, naomba nimjibu Mhe. Mjumbe unaendelea vizuri na vitu vyote hivyo wanavyohitaji masuala ya *visa* na kadhalika wizara inashughulikia na tayari hivi sasa wameshapata. Sasa kama kuna yeyote bado analalamika tafadhali aje kuniona. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, muda wa maswali na majibu umemalizika, lakini tuna maswali mengine saba, hivyo ningemuomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atengue kanuni ya muda, ili tuongeze nusu saa kwa ajili ya kama tutaweza kumaliza maswali haya ya leo. Mheshimiwa karibu.

KUONGEZA MUDA WA MASWALI

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa bado maswali yemebakia na muda wa maswali umemalizika. Kwa hiyo, ningeomba Baraza lako tukufu liweke Kanuni kando ya muda wa maswali, ili tuweze kumaliza maswali yaliyo mbele yetu. Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja, wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Nam.33

Kurudisha Huduma ya Maji Bure kwa Wananchi

Mhe. Bahati Khamis Kombo - Aliuliza:

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, hivi karibuni alitangaza elimu bure, matibabu kwa wananchi wake, ili kurudisha ule mfumo wa Marehemu Mzee Abeid Amani Karume uliokuwepo zamani.

Kwa kuwa wananchi walikuwa wakitumia mambo matatu katika kufaidika na matunda ya Mapinduzi ikiwemo elimu, matibabu na maji bure.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi maji yakawa bure.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 33 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia wizara yangu inatekeleza sheria ya maji namba 4 ya 2006 iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi ambayo imeamua kuwa wananchi wachangie huduma ya maji ili iwe endelevu. Suala hili lipo kwa mujibu wa sheria ambayo imepitishwa na Baraza hili, hivyo namuomba Mhe. Mwakilishi akubaliane na maelekezo hayo ya Baraza la Wawakilishi. Ahsante.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza kabisa, nililiambia Baraza lako tukufu kwamba sipingani na sheria namba 4 ya mwaka 2006 iliyotungwa na Baraza letu tukufu. Je, Mhe. Waziri atawasaidia vipi wananchi ambao hawapati maji kwa muda mrefu na wanaendelea kulipa fedha hizi. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza waliokuwa hawapati maji hawachangishwi na kama wapo maji hapa tutani lakini wanachangishwa basi tuonane, ili tujue tuli-*settle* lakini namna ya kupata maji, kwa sababu serikali inakusudia kuhakikisha kwamba wananchi wake wote wanapata maji na ni jukumu letu.

Kwa hiyo, tuone ni eneo gani, tuone na mpango gani unaweza kufanyika kwa ajili ya kupata maji hawa wananchi wake. Ahsante sana.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi napenda kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Katika jibu lake mama amesema Wizara inatekeleza sheria ya maji namba 4 ya mwaka 2006 ambayo imetungwa kwenye Baraza la Wawakilishi. Nataka kumuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo.

Lengo la kutungwa sheria hii ni kuimarisha huduma ya maji safi na salama mjini na vijijini, lakini tunashuhudia kwamba miundo mbinu ya maji inazidi kuwa mibovu siku hadi siku. Je, tokea kuanzishwa kwa sheria hii ni miaka kumi sasa, ni kiasi gani cha fedha ambacho kilichopatikana katika kuchangisha wananchi wetu, lakini pia fedha hizo zimetumika katika mambo gani. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kweli kwmba baadhi ya miundombinu ni mibovu na ndio maana ikawa kuna miradi mingi iliyolenga kutatua hilo tatizo. Lakini kwa upande wa kiasi gani kimechangishwa tangu kuanzishwa naomba nimjibu kwa maandishi. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wangu wa Kwale Miburani tangu kuumbwa dunia maji ya mfereji hawajawahi kuyapata. Je, Mhe. Waziri ni lini wananchi wangu wa Kwale Miburani watapata maji, ili kufaidi matunda ya Mapinduzi ya Serikali yao hii ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Makame Ali swalii lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwanza, nisikitike kumwambia kwamba kama angenambia juzi wakati tuko Pemba pamoja kwenye jimbo lake tungepata nafasi ya kwenda hilo eneo. Lakini niseme basi atuvumilie kwanza tuone eneo, tukutane na wataalam wetu tujue tunafanya nini, hapa siwezi kumpa jawabu kama tutafanya vipi ili apate maji, kwa sababu hilo eneo lenyewe bado silijui. Ahsante sana.

Nam. 57

Fedha za Maendeleo kwa Mamlaka ya Maji Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa katika hotuba yake ya Bajeti Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira alisema kwamba kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo, serikali inasimamia usambazaji wa maji vijijini na kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji.

a) Je, ni kwa sababu gani wizara haijatoa fedha kwa Mamlaka ya Maji Pemba kwa muda wa miaka miwili.

b) Je, serikali haioni kwamba kama haikutoa fedha za maendeleo kwa Mamlaka ya Maji Pemba kunasababisha kuyumba kwa mamlaka na kusababisha baadhi ya wananchi wa mjini kukosa maji na kupelekea usumbufu mkubwa.

c) Je, ni lini serikali itapeleka fedha za maendeleo kwa Mamlaka ya Maji Pemba, ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kutoa huduma hiyo kwa wananchi ambao ni haki yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba ifahamike kwamba wizara yangu huwa inaipatia fedha za Maendeleo Mamlaka ya Maji Afisi Kuu Unguja, na baadaye Afisi Kuu hufanya mgao wa fedha hizo kwa Afisi ya Mamlaka ya Maji Pemba, kwa mujibu wa mahitaji na kiwango cha fedha kilichopatikana. Katika kipindi cha utekelezaji wa mwaka wa fedha uliopita (2016/2017) Afisi ya Pemba ilipatiwa fedha za Miradi ya Maendeleo jumla ya shilingi milioni 58 kwa kazi za ulipaji fidia na ujenzi wa miundombinu ya maji.

Mhe. Naibu Spika, serikali inaendelea kuipatia wizara yangu fedha za miradi ya maendeleo kupitia maombi ya bajeti 2017/2018 awamu kwa awamu, kwa kufuata utaratibu wa upatikanaji wa fedha hizo, ambapo hadi kufikia Oktoba jumla ya shilingi 81 milioni zimepatikana kwa kazi za miradi ya maendeleo kwa upande wa Mamlaka ya Maji Tawi la Pemba. Ahsante sana.

Nam. 26

Ununuzi wa Karafuu kwa Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*)

Mhe. Mussa Foum Mussa - Aliuliza:

Shirika la Biashara la Taifa – *ZSTC* katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/2018 lilitarajia kununua karafuu zote, kwa msimu mzima kutoka kwa wakulima wa Unguja na Pemba, pamoja na kutoa mikopo kwa wakulima na pia kuwakatia bima ya kuanguka mikarafuu.

(a) Je, shirika lilikisia kununua tani ngapi hapo mwanzo na sasa limenunua tani ngapi.

(b) Je, ni kiasi gani cha mikopo kilichotolewa.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kumjibu swali Mhe. Mwakilishi naomba nitoe maelezo mafupi halafu nitajibu swali lake.

Mhe. Naibu Spika, swali lake Mhe. Mwakilishi alikuwa anataka kujua tani ngapi tumeweza kukisia na tumeweza kununua kutoka Pemba na Unguja.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba sisi tupo katika biashara, na katika biashara hii ya karafuu tumegundua mambo mawili makubwa ambayo yanatusababisha sisi kama wizara tusiweze kutangaza tani ngapi tumeweza kununua na tani ngapi tumekisia.

Kwanza, tuna watu wengi ambao tunashindana katika soko hili na tumegundua kwamba wenzetu wote hawatangazi kwa uhakika kiasi gani wamevuna au wamekisikia na ngapi zimo katika maghala, hiyo inakuwa kama ni silaha ya biashara hii ya karafuu. Na sisi hapo nyuma tulikuwa tumefanya makosa tukitangaza lakini tumeona kwamba mara kwa mara kati kati tunakuwa tunapigwa na wenzetu wanaoshindana na sisi kwenye biashara hii ya karafuu. Kwa hiyo, mwaka huu hatutangazi kiasi gani tumepanga, tumekisia na kiasi gani tunazo na kiasi gani tumeuza.

Mhe. Naibu Spika, la pili, pia walanguzi hawa wanaofanya ulanguzi na kuuza karafuu za magendo wakitupiga pia katika suala hili kwasababu tunapokuwa tunakisia, basi wanaiba karafuu nyingi na matokeo yake utakuta tunapewa zile ambazo tumekisia kuonekana ndio hali halisi ilivyo.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha 2017/2018 serikali hadi kufikia hadi kufika 28/11/2017 Shirika limeshanunua karafuu zenye thamani shilingi bilioni 97.405. Vilevile, kwa upande wa Unguja karafuu zenye thamani ya shilingi bilioni 1.998 na kwa upande wa Pemba karafuu zenye thamani ya bilioni 95.707.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa utoaji mikopo shirika katika kipindi cha 2017/2018 ilikopesha wakulima 111 kati ya hao 37 kutoka Unguja na 74 kutoka Pemba. Kiasi cha fedha zilizokopeshwa kwa wakulima ni shilingi milioni 191 wamefanikiwa kulipa kiasi cha shiilngi milioni 1.7 na kilichobaki ni shilingi milioni 139.3. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri kwakuwa kipindi cha uchumaji wa karafuu watu wengi hupata athari ya kuanguka.

a) Je, ni watu wangapi Pemba na Unguja walioanguka mikarafuu kwa mara hii. Na je, mtawalipa haki yao ya kuanguka.

b) Kuna usemi kwamba vijana wengi walioanguka mikarafuu kwa mwaka huu walio chini ya miaka 18 hawatolipwa fidia hii. Je, suala hilo ni kweli na ikiwa ni kweli ni kwasababu gani.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mhe. Mwakilishi. Mpaka hivi karibuni idadi niliyokuwa nayo ya watu walioanguka

kwa mikarafuu ni 39 na wamelipwa wote kasoro watu 5, lakini hesabu hiyo inafanyiwa kazi na nitakuletea baadae kwa maandishi baada ya kukamilisha msimu na kujua wangapi wote walioanguka na wangapi ambao wamelipwa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu swali la pili la nyongeza sina taarifa kwamba walioanguka wengi ni watoto chini ya miaka 15, lakini ni kweli kwamba mtoto aliyekuwa hajafikia miaka 18 akianguka kwenye mkarafuu Shirika la Bima la *ZSTC* hatuwezi kumlipa mtoto chini ya miaka 18 kwa sababu sheria za bima haziruhusu.

Mhe. Naibu Spika, vilevile wakati tunatoa tangazo na kufungua msimu huu tuliwatahadharisha sana wazee na wazazi na kuwaambia kwamba wasiwaruhusu watoto wao waliokuwa chini ya miaka 18 kwenda kupanda kwenye mikarafuu, kwasababu wakipanda kwenye mikarafuu hawatokuja kupewa fidia yoyote pindipo watakapokuja kuanguka.

Sasa kama mzazi hakusikia tumesema na tumetumia kamati zetu za *Task Force* na tumewaandikia masheha kuwakataza watoto waliokuwa chini ya miaka 18 wasiende kupanda mikarafuu. Kwahivyo, kama kapanda mikarafuu hakutusikiliza wasia wetu na maelekezo yetu, hivyo nina masikitiko sana kwamba hawa hawatoweza kupata fidia. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 47

Gharama za Kutangaza Utalii Nje ya Nchi

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa kwenye programu ya kuendeleza utalii nje ya nchi, wizara ilitia gharama za ujenzi wa mabanda ya maonesho nchini Dubai na Ujerumani kwa lengo la kuitangaza nchi yetu kwenye soko la utalii na kutangaza bidhaa na huduma za utalii wa Zanzibar.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha ambazo zilitumika kwenye ujenzi wa mabanda hayo.

(b) Je, faida gani ambayo tumeipata kwa kuitangaza bidhaa na utalii wetu nje.

(c) Je, baada ya kuutangaza utalii, ni watalii wangapi waliongezeka na watalii wangapi tunategemea kuwapata kwa mwaka huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, jumla ya dola za Kimarekani 118,951.84 zilitumika kwa ajili ya kugharamia Maonesho ya Utalii yaliyofanyika nchini Ujerumani mwezi wa Machi, 2017 na Dubai mwaka wa Mei, 2017. Kati ya fedha hizo Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ilichangia jumla dola 66,000 kwa ajili ya ununuzi wa eneo (mita za mraba 44

kwa Maonesho ya Ujerumani na mita za mraba 63 kwa Maonesha ya Dubai) na sekta binafsi ilichangia dola za Kimarekani 52,951.84 kwa ajili ya ujenzi wa mabanda hayo.

(b) Mhe. Naibu Spika, kupitia ushiriki wa maonesho ya Ujerumani na Dubai, Zanzibar imepata faida nyingi ikiwemo taarifa zinazohusu Utalii wa Zanzibar kufahamika zaidi katika soko la Ujerumani, Dubai na nchi zilizokaribu na masoko hayo. Kupitia maonesho hayo Zanzibar imeweza kupokea ndege za Utalii (*charter flights*) kutoka nchini Latvia na Urusi. Vilevile, Zanzibar imepokea mwandishi wa habari kutoka Ufaransa ambayo ameweza kutengeneza *documentary* ya Utalii kwa lugha ya Kifaransa na Kiingereza ambayo itarushwa hewani kupitia televisheni za Ufaransa na mitandao ya kijamii.

(c) Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi hutumia njia tofauti kutangaza bidhaa na huduma za Utalii zilizopo Zanzibar. Kupitia jitihada hizo za utangazaji, inakadiriwa kuwa hadi ifikapo tarehe 31 Disemba, 2017 jumla ya wageni 457,027 wanatarajiwa kutembelea Zanzibar. Aidha, hadi Septemba, 2017 jumla ya wageni 302,529 wametembelea Zanzibar ambayo ni sawa na asilimia 67 ya makadirio ya mwaka. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu yako mazuri sana yenye mwelekeo mzuri ya kutuongezea watalii na kukuza pato la taifa lakini nilikuwa na swali dogo la nyongeza. Nilikuwa nataka kujua kwamba inaonekana kwenye majibu kuna sekta binafsi ambazo zilichangia katika gharama za ujenzi kwa matangazo ya biashara ya utalii huko nje.

Je, nilitaka kujua katika hizo sekta binafsi ni sekta gani binafsi ambazo zimeshiriki katika kuchangia hizo dola za Kimarekani 52,951 na faida ambazo imezipata hizo sekta binafsi. Bila shaka wametoa pesa kwa kutegemea faida, ni faida gani zilizopata kampuni hizo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Mwakilishi. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna taasisi nyingi za binafsi ambazo zimechangia maonesho haya, sekta hizi ni kama hivi ifuatavyo:

Kuna ZATO, *ZATI, MELIA, PALUMBO, ORAL RESOURCE* na kadhalika.

Nam. 50

Athari ya Matumizi ya *Smart Phone* kwa Vijana Wadogo

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwa kuwa baadhi ya vijana wetu wameshasahau kabisa maadili ya asili ya Kizanzibari na badala yake kufuata maadili ya nchi za kimagharibi kunakosababishwa na utandawazi, hasa kwa vijana wetu wa rika la chini.

(a) Je, serikali haioni kwamba kuendelea kuachia matumizi ya simu za mikononi kwa vijana wadogo, kunaongeza kasi ya vijana hao kufanya michepuko jambo ambalo ni athari kubwa kwao.

(b) Je, ni lini serikali itafikiria kutunga Sheria au Kanuni ya kuwadhibiti vijana wadogo wenye umri wa miaka 10 hadi 17 kutotumia "*Smart Phone*", kwa ajili ya kuwalinda na changamoto zinazosababishwa na utandawazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 50 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Matumizi ya simu za mkononi ikiwemo simu aina ya "*smart phone*" yanalinganishwa sawa na matumizi ya kompyuta kwa mujibu wa mpango wa Milenia (*MDGs – Millennium Development Goals*) wa matumizi wa vifaa vya kikompyuta duniani ambavyo unahamasisha utumiaji wa kompyuta kwa watoto katika mambo ya kitaaluma, kutokana na kauli mbiu ya mpango huo inayosema *One Laptop per Child* (*OLPC*) yaani kompyuta moja kwa mtoto mmoja.

One Laptop per Child (*OLPC*) ni mpango maalum ulioanzishwa duniani, ili kuwasaidia watoto katika mambo ya kitaaluma na elimu kwa ujumla wa nchi inazoendelea kwa mfano Zanzibar. Mpango huu unampatia fursa mtoto ya kupata kutumia na kujifunza kompyuta wakati angali mdogo ambapo itamjengea uwezo wa kujiamini, kujielezea pamoja na kupata habari tofauti duniani.

Aidha, kwa hapa kwetu Zanzibar wanafunzi wa skuli za msingi wanaanza kusomeshwa elimu ya TEHAMA wanapofika darasa la tano (5). Pia, wanafunzi hao wanatakiwa kulifanyia mtihani wa Taifa wa kumaliza Elimu ya Msingi somo la TEHAMA wanapofika darasa la sita (6). Kwa kuzingatia kwamba umri wa kuanza masomo ya skuli ya msingi (Darasa la kwanza) ni miaka sita (6), mtoto anapofika darasa la sita anakuwa na umri wa miaka kumi (12).

(b) Kwa kuzingatia maelezo tuliyoyatoa huko juu watoto kuanzia umri wa miaka saba (7) hawawezi kuzuiwa kutumia vifaa hivyo, ili kuepusha kuwakosesha haki zao za kielimu. Katika kuzuia matumizi yasiyokuwa na maadili kwa vifaa hivyo Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 (*Cyber Crime Act, 2015*) inapiga marufuku matumizi mabaya ya vifaa hivyo, sio tu kwa watoto bali hata kwa watu wazima.

Vilevile, sheria hizo zinakataza kwa mtoto chini ya miaka kumi na nane (18) kumiliki laini ya simu (*SIM Card*) kwa maana kwamba kampuni na simu hazitakiwi kabisa kusajili laini kwa mtoto yeyote aliyekuwa na umri wa mwaka mmoja hadi miaka kumi na saba kwa mujibu wa sheria. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na pamoja na dhamira nzuri ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwapatia mpango bora wa elimu kwa kuwaruhusu kutumia…

Mhe. Naibu Spika: Uliza swali …

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, ndio naijenga hoja nimuulize swali…

Mhe. Naibu Spika: Uliza swali muda hatuna Mhe. Mjumbe.

Mhe. Omar Seif Abeid: (a) Sasa je, kwa utaratibu huu au kwa hii sheria huoni kwamba wapo baadhi ya vijana walio chini ya miaka 18 ambao wanamiliki hizo kadi za simu.

b) Hatuoni kwamba kuendelea na utaratibu huo wa kutowadhibiti vijana wetu pia kutaleta athari hiyo ambayo tutakuja kujutia hapo baadaye. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa taratibu na Kanuni zetu mtu yeyote ambaye anataka kusajili *sim card* lazima aende na kitambulisho chake ambacho kitamuonesha kwamba huyu ni tayari kijana aliyetimiza miaka 18. Na sote tunajua kwamba vitambulisho vingi Zanzibar vinatolewa vijana wakiwa na umri wa miaka 18. Kwa hiyo, iwapo mtoto yeyote anasajiliwa hapo itakuwa amesajiliwa kinyume na sheria na hatua kali huchukuliwa kwa mtoto yule na yule aliyemsajili.

Kuhusu swali lake la pili, maadili binadamu tunafundishwa na wazee wetu na mazingira yetu na pamoja na skuli ambazo tunakuwa tunasoma. Kwahiyo, nina imani kubwa sana tunapowafunza watoto wetu maadili mema sina shaka kabisa kwamba watatumia vizuri hizi kompyuta na *sim card* zao katika kujiendeleza zaidi kielimu, ndio kusudio zaidi lilowekwa kutumia hizi kompyuta na simu kwa vijana wetu ambao wako masomo ya sekondari. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Nam. 58

Mapato kwa Shirika la Bandari Zanzibar

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa Shirika la Bandari kwa mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia Machi, 2017, tayari lilikuwa limeshakusanya jumla ya shilingi 20,979,844,866 kati ya shilingi 29,895,185,265.61 kutokana na vianzio vyake vya mapato. Hatahivyo, shirika lilitumia shilingi 5,548,394,801 ambazo ni sawa na 51% tu za fedha iliyotengwa kwa ajili ya kazi za maendeleo.

(a) Je, miradi gani ya maendeleo ilipangwa kutekelezwa na Shirika la Bandari Zanzibar na utekelezaji wake umefikia hatua gani.

(b) Je, kwa kipindi cha Aprili/Juni, 2017 Shirika la Bandari lilikusanya shilingi ngapi, kwa ajili ya kufikia lengo la ukusanyaji walilojipangia kwa mwaka huu wa fedha.

(c) Je, kuna tafauti ya kiasi cha makusanyo kwa Shirika la Bandari kwa 2015/2016 na mwaka 2016/2017.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 shirika lilipanga kutekeleza miradi ya maendeleo 15 ikiwemo miradi 11 inayoendelea kutoka mwaka uliomalizika (2015/2016) na miradi minne (4) mipya. Katika utekelezaji wa miradi hiyo shirika lilitekeleza miradi 13 kati ya miradi 15, ambapo miradi tisa (9) ilikamilika na miradi minne (4) inaendelea katika mwaka wa fedha 2017/2018.

(b) Mhe. Spika, kwa kipindi cha Aprili – Juni, 2017 shirika limekusanya shilingi 6,899,128,362.28 ambapo ni sawa na asilimia 92 ya makadirio ya kipindi hicho.

(c) Shirika katika mwaka wa fedha 2015/2016 lilikusanya shilingi 28,403,268,241.51 na mwaka 2016/2017 lilikusanya shilingi 27.8. Hivyo, mapato hayo yalipungua kwa asilimia 2 sawa shilingi. 524,295,012.86. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini napenda nijue ni miradi gani ya maendeleo ambayo imekamilika na ni ipi ambayo haijakamilika, na gharama za miradi hiyo ilikuwa ni kiasi gani, na fedha zilizogharamika kutumia kuendesha miradi hiyo ni fedha zilizotokana na makusanyo ya Shirika la Bandari au ni baadhi ya pesa zilitoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe. Nilianza kujibu suala hili tokea jana tumewaambia kwamba, tulikuwa na miradi ya vifaa ambapo ilitugharimu takriban shilingi 11 bilioni na yote tumelipa kwa mujibu ilivyotakiwa kupitia *Peoples' Bank.* Vile vile miradi minne ambayo hatujaikamilisha ni Mradi wa TEHAMA, Mradi wa Ulinzi na Usalama, Mradi wa Mkokotoni na vilevile kuna mradi mwengine ambao tunaita Mradi wa Kuongoza Meli.

Kwa hivyo, mpaka sasa hivi tunahitajika kutumia katika mwaka huu wa fedha shilingi bilioni kumi, ili kukamilisha miradi hiyo na miradi mingine mipya ambayo nimeielezea jana katika kumjibu maswali. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Nam. 107

Ujenzi wa Daraja kutoka Kisiwa cha Shamiani kwenda Mpene Mwambe

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kuwaletea wananchi wake maendeleo. Lakini katika jimbo la Kiwani kuna sehemu ya Mwambe kipo Kisiwa kinaitwa Shamiani, kisiwa hicho kimepakana na maneno ya Mpene, Mwambe na usafiri wao ni wa kuvuka kwa madau na ngarawa. Pia, lipo eneo la Mpene, Mwambe na Kisiwa cha Shamiani kimepakana kwa masafa ya mita ishirini au thalathini na kuweza kwenda na kurudi kwa kutumia usafiri wa barabarani, kama eneo hilo litaunganishwa kwa daraja kuwapatia maendeleo ya haraka wananchi katika kisiwa hicho cha Shamiani.

(a) Je, serikali ina mpango gani wa kulijenga daraja hilo.

(b) Je, serikali haioni umuhimu wa kuona kama litajengwa daraja hilo kisiwa hicho kitapata maendeleo ya haraka ikiwemo utalii.

(c) Je, eneo hilo limeshafanyiwa utafiti wa uwezekano wa kujengwa daraja hilo au bado.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 107 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, kwa hivi sasa serikali haijaweka mpango wa kulijenga daraja hilo.

(b) Serikali inajua umuhimu wa utalii katika kukuza uchumi wa taifa na kuimarisha miundombinu ya barabara ni sehemu ya kuharakisha maendeleo ya wananchi wake. Hivyo basi, pale ambapo kutahitajika kuimarisha miundombinu hiyo haitasita kufanya hivyo kwa mujibu wa bajeti na upatikanaji wa fedha.

(c) Serikali haijafanya utafiti wa uwezekano wa kujengwa daraja eneo hilo analolisema Mhe. Mwakilishi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi nimshukuru waziri kwa majibu yake, ingawa ni ya kukatisha tamaa. Lakini nataka nimwambie Mhe. Naibu Waziri kwamba, kwasababu Mhe. Rais anafanya jitihada zake zote kuvirahisisha visiwa, ili kuwa karibu pamoja na nchi kwa maeneo ya kutumia maboti na kununua boti za kisasa na kila jambo. Lakini kisiwa kile cha Shamiani ni sehemu ndogo tu ambayo inaweza ikatuunganisha.

Je, Mhe. Waziri ni lini atafanya utafiti, ili tuweze eneo lile kupunguza hizo gharama za kusafirisha na pia ili tuweze kuunganisha pale tuna watu zaidi ya 1,000 kwenda mbele ambao wanatumia kisiwa kile na ambao kiusalama pamoja na maendeleo yao yatapatikana.

Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo. Kama nilivyosema jambo la utafiti linataka kufanyiwa uchambuzi wa kina, lakini pia kama nilivyosema mimi karibuni nilikuwa maeneo yale ya Mwambe na Waheshimiwa wenzangu wawili hapa na tuliona ile sehemu ni mbali kidogo kama anavyosema yeye na kunahitajika gharama. Kwa hiyo, ushauri

wake tutauchukua na tutafanya utafiti, iwapo hali itaruhusu kwamba kweli kuna uwezekano wa kufanya hiyo kazi na serikali inayo fedha tutafanya, lakini ni kazi ambayo inataka utafiti kwanza.

Sasa kama alivyosema kwamba sisi tunajali usalama ndio maana katika mwaka huu wa bajeti tumetenga fedha maalum takriban shilingi milioni 800 kwa ajili ya kununua boti za kusaidia wananchi wetu wa visiwa kuwavusha kwa salama na amani. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe...

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, nimesimama mimi, nyinyi mkae nina taarifa nataka kutoa. Kwahiyo, naomba sana mukae muniachie nitoe taarifa halafu tutaendelea na miongozo.

Waheshimiwa Wajumbe, nafahamu vizuri sana kwamba ratiba yetu leo ilikuwa baada ya maswali na majibu kutakuwa na semina inayohusiana na masuala ya mswada wa uchaguzi. Na kwa bahati nzuri vile vile kuna wajumbe wanne ambao tayari wameniletea *note* hapa kwamba kidogo wanaomba muda wa dakika kumi kumi kwa ajili ya kutoa taarifa ambazo zinahusiana na humu ndani ya Baraza.

Hivyo, wajumbe hao nafikiri ndio maana wamesimama haraka haraka ni Mhe. Mohamed Said Mohamed na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Lakini vile vile nina Waheshimiwa Mawaziri ambao ni Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ana taarifa na yeye kuhusiana na michango ya jana ambayo tulielekeza ipatikane pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye na yeye vile vile anataka kutoa taarifa inayohusiana na vifo vya Wanajeshi wetu wa Jeshi la Wananchi la Tanzania.

Kwa hiyo, nitaanza kwanza kumpa nafasi Mhe. Mohamed Said Mohamed halafu atafuata Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa imani yako na kwa kuona hoja yangu ambayo ipo. Hoja yangu ilikuwa juu ya kukosekana kwa kifungu cha katiba cha 18 cha Katiba ya Zanzibar, uhalali wa kupata habari kwa wananchi. *ZBC TV* na *Radio* tangu jana jioni ukizingatia na hivi asubuhi ilikuwa haipatikani na wananchi walikuwa wanataka kulitizama Baraza lao tukufu. Sasa hatujui kwa mara ile tuliambiwa wanaingia kwenye dijitali, lakini mara hii wameambiwa sijui watatuambia nini. Sasa nilikuwa nikuombe tu, sitaki kusimamisha shughuli za Baraza lakini nilikuwa nataka serikali ijue au kama inatoa tamko, ili wananchi wetu wajue jinsi gani kwa nini wanakosa habari na kinavunjwa kifungu cha 18 cha Katiba ya Zanzibar. Nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru Mhe. Mjumbe, serikali ipo imeshalisikia na inaweza ikalitolea maelezo. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillah Rahmani Rahiim*. Kwanza tumshukuru Mhe. Spika pamoja na wewe Mhe. Naibu Spika na watendaji wote kwa kuweza kunipatia nafasi

hii pamoja na kuikubali jana hoja maalum ya Mhe. Nassor Ali Salim kuhusiana na suala la *Zanzibar Heroes*.

Mhe. Naibu Spika, nimesimama hapa jana kumejitokeza kitu baada ya kuchangia sisi wajumbe wachache kwenye suala hilo. Kuna mwandishi wa habari mmoja anaitwa Salma Hamoud Said nimeingia na simu leo nimeomba kwasababu ya ushahidi baada ya kuzungumza maneno ambayo tumeyazungumza humu ndani hasa mimi. Kwa kweli, mwanahabari huyu amelidhalilisha Baraza la Wawakilishi, wajumbe wote pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, baada ya ku-*post* uongo ambao ameutaka yeye na kipande ambacho kakitaka yeye alichokiingiza kimoja. Pia na ku-*edit* video kwa kipande kile kuwapa watu anaowataka yeye.

Kwa maana hiyo, nimetukanwa mimi na kanidhalilisha ambaye ni Mjumbe wa Baraza la wawakilishi tumetukanwa wawakilishi sote pamoja na serikali nzima. Alichokiandika kwenye ujumbe wake katika ukurasa wa *facebook*, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi leo wamesema eti wachangishane kila mmoja shilingi 25,000, ili watakaporudi wachezaji wa *Zanzibar Heroes* wale pilau na kupiga picha pamoja.

Mimi nilitarajia mbali na kuiomba serikali lakini wao wenyewe kwa sauti moja wasamehe posho zao za kikao cha leo, ili zipelekwe Nairobi na sio mpaka warudi, *in short* ahadi ya pilau imetukera.

Kwa kweli, katika mchango wangu wa jana nilizungumza mambo karibu *point* tano, na ndio kawaida yetu tunapochangia tunakwenda kwa *point* hatukurupuki kama alivyoandika yeye kwenye *facebook*. Nilizungumza *point* ya mwanzo nilimuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na serikali iweze kwenda na Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ikiwa yeye kaweza kutokana na majukumu yake atakwenda, ikiwa hawezi amwakilishe japo waziri wake aende akawape angalau motisha. Hili ni jambo la mwanzo nililolizungumza jana. *(Makofi)*

Pili, nikazungumza kwamba suala la kurudi basi waje warudishwe kwa chombo cha ndege *instead of* basi ambalo lilitumika mwanzo, na serikali imeliridhia hilo suala. Lakini la tatu nikazungumza kama mimi kushauri wajumbe wenzangu kwamba hii nchi nzima, dunia nzima, viongozi wote Marais, Mawaziri Wakuu, wanapotaka wachezaji wao ikiwa timu ya mipira, *volleyball, netball, golf* na mambo mengine; wanaposhinda au kufanya vizuri kwa njia yoyote ile huwa wanaalika kama Ikulu kula nao, kupiga nao picha pamoja, kuzungumza maneno mazuri na sio kwamba tumewaita sisi kula nao biriani kwamba wana shida na biriani. Sisi tunafanya hivyo kwa uzalendo mkubwa tunawapenda na ndio maana tunataka tuje tukae nao viongozi wote tushereheke nao pamoja. Kwa hili wakishinda, wasishinde tutakuja kula nao, narudia tena tutakuja kula nao pamoja. *(Makofi)*

Vile vile, nilizungumza *point* nyengine mbali ya fedha hizi za chakula ambazo amezizua yeye kwamba ndio tumesema zipelekwe Nairobi shilingi 25,000; hizi zilikuwa ni za chakula lakini tumetoa fedha zote jumla ni shilingi 10,875,000/-. Wawakilishi tumeridhiana kwa sote na serikali imefurahika na suala hili na tumetoa kwa uzalendo wetu na imani yetu shilingi 10,875,000/-. Sasa cha kushangaza mwandishi huyu wa habari, Salma Said kaandika vitu ambavyo havina maana, vimetudhalilisha, katukanwa kuanzia Mhe. Rais ndani ya *comment* zile.

Mhe. Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katukanwa ndani, viongozi wote na mimi binafsi juu kaweka picha yangu.

Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kuzungumza kwamba jambo hili limeleta athari kubwa. Mwandishi huyu wa habari kwa rikodi zake zilizokuwepo nyuma kwamba yeye ni fisadi kwanza wa Chama cha Mapinduzi, halafu mnafiki, mfitinishaji, muongo, hafai kuwa katika jamii. Mimi ningeomba Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo amchukulie hatua kwa mujibu wa sheria kutokana na wizara yake suala la habari linamhusu. *(Makofi)*

Vile vile Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwenye suala la *TCRA* mtandao wake wa *facebook* ahakikishe anaufungisha kutokana na huyu kwamba kazowea. Kama mnakumbuka kipindi cha nyuma mwanamke huyu ambaye ni mmoja tu anataka kuharibu na wanawake wenziwe ambaye ni muongo.

Mhe. Naibu Spika, jambo la kushangaza kwamba ndani ya Mamlaka hii ya Baraza la Wawakilishi viongozi wetu wa juu tunao wanatuheshimu. Leo tunae Makamu wa Rais humu ndani kakaa kimya utafikiri hayumo, lakini si kama hawezi kuzungumza lakini bado anaheshimu Baraza hili tukufu. Lakini cha kushangaza panya yule mmoja anataka kuingilia ukumbi huu.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ahakikishe mtandao huu wa *facebook* unafungwa na isitoshe kwa mujibu wa sheria za Baraza la Wawakilishi na Kinga, Fursa za Wajumbe ukurasa wa 120, Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe, kwanza kuchunguza na kuyatolea maamuzi masuala yote yanayohusiana na Kinga, Fursa, Mamlaka na Madaraka ya Wajumbe na pia Mamlaka ya Madaraka ya Spika, Mhe. Naibu Spika, na wenyeviti wa Baraza ambayo yanapelekwa mbele ya kamati na Spika au Mjumbe yeyote wa Baraza.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa kuwa huyu mtu kadhalilisha Baraza, kanidhalilisha na mimi, katukanisha na viongozi wa serikali iwe mtu wa mwanzo kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia wizara hizi mbili kumchukulia hatua mtu huyu pamoja na Kamati ya Maadili ya Baraza la Wawakilishi, niombe kiti chako kimuite kimhoji halafu kitoe maamuzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini tukiacha hilo mimi mwenyewe binafsi kama mjumbe aliyenidhalilisha, nahakikisha nitakaa na wanasheria wangu nitamshtaki na nitamdai fidia ya shilingi milioni mia mbili kwa kuniadhirisha kwenye mitandao ya *facebook*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mtu kama huyu hafai hata kualikwa tena kwenye Baraza la Wawakilishi kuja kuchukua habari. Hivi juzi kwa taarifa alikuwepo kuna waandishi wa habari wengi sana wanakuja humu ndani ambao sio wafanyakazi wa *ZBC* na wengineo wana heshima zao, wanatoa habari za ukweli, hawana fitina.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Mhe. Naibu Spika, huyu kuna kipindi alizua uongo kwamba katekwa, huyu kwa uongo wake inaonekana dhahiri hakutekwa na ni mnafiki. Watu kama hawa tunataka Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo apewe ruhusa

alizungumze hili suala na hili litakuwa ndio mwanzo na mwisho kwa mtu yeyote katika nchi hii kucheza na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuingilia mhimili wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo nalilaani suala hili na ninamlaani na yeye kwa uongo wake. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-lafit Yussuf nafikiri umefahamika vizuri sana. Sasa nimpe nafasi kwanza Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo na yeye ana taarifa ndogo, baada ya hapo nitampisha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana, awali ya yote niweze kumshukuru Mwenyezi Mungu *(S.W)* mwingi wa rehema na mwenye nguvu zaidi kushinda viumbe vyote.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nizungumze machache yanayohusiana na masuala yetu ya Baraza. Lakini kabla ya kuzungumza haya ningeomba kwa ruhusa yako nizungumze kidogo tu kwamba, kutokana na mjumbe aliyesimama muda mchache uliopita na kuwasilisha taarifa yake au hoja yake.

Nataka nilijulishe Baraza lako tukufu kwamba, tunaamini wazi na tunaelewa kwamba tasnia ya habari ina maadili yake na habari kwa urefu wake ina kanuni, sheria na taratibu zake ambazo zinapaswa kufuatwa. Kwa kupitia vyombo ambavyo vinasimamiwa na Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, ikiwemo Kamisheni ya Utangazaji, Bodi ya Matangazo na Vijarida zote hivi sasa uongozi wake umekamilika na sisi tunalichukua suala hilo ambalo limeelezwa na mjumbe, tutalifanyia uchunguzi wake na tutalifanyia kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ni mara nyingi inatokezea waandishi kwenda kiyume na maadili, ni jambo ambalo hatulipendelei litokee kwa waandishi wetu. Lakini endapo waandishi wamekwenda kinyume na wanavunja maadili ya tasnia hii, basi hatua za kisheria zitachukuliwa. Namhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba endapo patakuwa na makosa yaliyofanyika taasisi zetu hazitasita kuchukua sheria, ikiwezekana kuonekana kwamba hafai kuwemo katika tasnia hii ya habari kwa upotoshaji kwa wananchi wa Zanzibar, na kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar, basi tutachukua hatua hata za kupokonya kile kibali ambapo jambo hilo liachwe kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo sasa nizungumze dhamira ambayo ilinipasa na mimi niombe muda mchache kuzungumzia taarifa yetu.

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa kwamba jana tulitoa taarifa juu ya timu yetu ya *Zanzibar Heroes* ambayo ipo kule nchini Kenya na hii leo ikiwa inasafiri kuelekea Kisumu kwa kucheza nusu fainali.

Mhe. Naibu Spika, jana Baraza lako tukufu lilijawa na hamasa na limepata moyo wa kuwapa ari wachezaji wetu wa Timu ya *Zanzibar Heroes* kwa kuweza kuwachangia michango yao adhimu kabisa. Napenda kulieleza Baraza lako tukufu kwamba katika michango yote iliyochangiwa Timu yetu ya Taifa, Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi wamekuwa ndio wa kwanza

kutoa mchango mkubwa kuliko taasisi yoyote. Ni wazi kwamba mchango unaochangiwa sio kama vile ulivyopotoshwa na waandishi wa habari, kila mjumbe aliweza kuchangia au anaendelea kuchangia jumla ya shilingi 125,000/- na hii itafanya jumla ya michango kufikia shilingi 10,873,000/-. Huu ni mchango mkubwa ambao tumeupata katika taasisi yako Mhe. Naibu Spika, kuliko taasisi zote. *(Makofi)*

Pia nazishukuru taasisi nyengine ikiwemo *PBZ* ambayo ilikuwa ndio inafuatia kwa mchango mkubwa imetupatia shilingi 10,000,000/- nazo nataka niziweke hadharani, lakini vile vile namshukuru sana Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ambaye na yeye amechangia mchango mkubwa sana kupitia Shirika letu la *ZSTC*. Pamoja na mashirika mengine yaliyotajwa jana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa namna hiyo, na michango hii tutakayoipata nataka nikuhakikishie kwamba mchango wa Baraza la Wawakilishi utawafika wahusika kabla hawajacheza nusu fainali. Taratibu za kuwapelekea mipango hiyo na jana nimezungumza na kocha nimemueleza azma ya Baraza, nimemueleza nia iliyofikiwa na Baraza na ameniambia nilete salamu zetu kwamba na wao watafanya jitihada zao zote, ili na wao wapate nafasi ya kuingia Barazani huenda ikawa ni chachu ya kuja kuwa na wao wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nataka nikushukuru na wewe binafsi kwa jitihada zako na kwa muda uliotupa ili kuweka wazi suala hili. Nataka niwashukuru wachangiaji waliochangia jana akiwemo Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf kwa mchango wake na kuweza kuweka kima hiki cha kuweza sisi kuchangia. Vile vile, nimshukuru Mhe. Spika wa Baraza hili la Wawakilishi kwa kuweka taratibu za kuhakikisha kwamba michango yetu inafika mapema iwezekanavyo na sisi tupo makini na yale yote ambayo yalikuwa yanaonekana yatawapa ari, motisha ya wachezaji wetu, ili kuzisuuza nyoyo zetu Wazanzibari, basi yatakuwa yamefikia na natumaini timu ile nayo itaongeza ari ya kuweza kuhakikisha kwamba nyoyo zetu zinapata burudani.

Mhe. Naibu Spika, naomba kukujulisha kwamba, jana tumesikika kupitia vyombo vya habari na taarifa zile zote zimepitia kutoka vyombo vyetu vya habari zikiwemo *television* za *ZBC*, inawezekana kwamba kulikuwa kuna baadhi ya sehemu umeme umezimwa, kulikuwa na marekebisho mengine inawezekana kwamba sehemu nyengine zikawa hazikuweza kupata zile taarifa.

Lakini pongezi nyingi sana zimepokewa kutoka Baraza la Wawakilishi na mimi pongezi hizo nataka nizilete kwenu na kwa Wajumbe wote kwa ujumla kwa moyo wao waliouonesha. Mhe. Naibu Spika, nataka kukuhakikishia kwa mchango huu na kwa michango mingine inayoendelea kutolewa basi *Zanzibar Heroes* watarudi na ndege kwa hali yoyote iwe wamepata kombe, iwe hawakupata kombe tutafanya jitihada. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, hili ni jukumu la serikali, serikali ndio inasafirisha timu ya taifa. Nataka kutoa tahadhari kumekuwa na matapeli baada ya taarifa tulizozitoa jana, baada ya matangazo tuliyoyatoa jana kwamba sisi tumeanza michango kwa hivyo wamejitokeza matapeli, ambao tayari wameanza kutoa namba za simu kwenye hiyo mitandao na mitandao hiyo ipo ya ndani, nje mpaka Ulaya. Kumekuwa na *account* zinaweza kutolewa sasa hivi, ili *Zanzibar Heroes*

ichangiwe kwasababu tu, inaonekana kama kwamba serikali imewatelekeza kuwapeleka wachezaji wetu.

Serikali imefanya jitihada zake zote Baraza la Wawakilishi limethibitisha juhudi zake kwa serikali. Kutokana na hili Mhe. Naibu Spika, nataka nikuhakikishie kwamba serikali haikuwa na ukosefu wa kuwapeleka wale wachezaji wetu kule. Wananchi wale kama ilivyozungumzwa jana kwa mara ya kwanza wameondoka wakiwa na furaha kuliko mara zote ambazo wanaondoka hapa kwetu. Kwa hivyo, *account* zinazotolewa nje namba za simu zinazotelewa nje kwa kuchangiwa na zinazoingizwa katika mitandao tafauti nataka nitoe tamko rasmi kwamba hizo ni simu ambazo hazikubaliki kupewa michango kwa ajili ya kuichangia timu yetu ya taifa *Zanzibar Heroes*. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, namba zitakazokubalika kuichangia *Zanzibar Heroes* ni *account* kutoka Baraza la Taifa la Michezo la Zanzibar liliopo chini ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo ambayo namba yake inatangazwa wazi. Kwa yule yoyote ambaye anataka kuchangia kwa kupitia ubinafsi basi *ZFA* kupitia *account* ya *ZFA* nayo *account* yao imetolewa wazi. Zaidi ya *account* hizo mbili Mhe. Naibu Spika, hakuna michango tuliyoipokea kwa kupitia simu wala hakuna michango tutakayopokea kwa kupitia njia nyengine yoyote za kuwafikishia wachezaji. *(Makofi)*

Kwa taarifa hii Mhe. Naibu Spika, naomba niwashukuru tena Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa miongozi yake aliyotupatia ya kuweza kutukubalia suala hili tulilete hapa Barazani. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika nashukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Sasa nitampisha Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa ajili ya kutoa taarifa kuhusiana na vifo vya wanajeshi wetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kuweka nchi yetu katika hali ya amani na utulivu.

Aidha, naomba kuchukua fursa hii kwa masikitiko makubwa kutoa pole kwa wanafamilia wote ambao wamepoteza ndugu na jamaa zao ambao ni wanajeshi waliofariki katika shambulio huko katika Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyoelewa kuwa mnamo tarehe 7/12/2017 kimoja kati ya Vikosi vya Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania vinavyolinda amani katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo katika Jimbo la Kivu Kaskazini, kilivamiwa na kikundi cha waasi nchini Congo kinachojulikana kwa jina la *Allied Democratic Forces (ADF).*

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tunalaani vikali shambulio hili lililofanywa na waasi wa *ADF* kwa vikosi vyetu vya kulinda amani ambavyo havipaswi kushambuliwa kwa mujibu wa sheria za Umoja wa Mataifa.

Shambulio hilo lililosababisha vifo vya wanajeshi 14. Wanajeshi tisa kutoka Zanzibar, wawili kutoka Arusha, wawili Dar es Salaam na mmoja Bukoba, na majeruhi wengine 44 walijeruhiwa kati ya hao wanne hali zao ni mbaya na matibabu yanaendelea. Aidha, mmoja mpaka sasa hajulikani alipo katika wanajeshi hao.

Mhe. Naibu Spika, kwa kawaida Jeshi la Wananchi wa Tanzania hupeleka walinda amani katika nchi mbali mbali kwa kuzingatia mpangilio wa vikosi vyake vilivyopo katika maeneo mbali mbali nchini. Kwa wakati huu ambapo tukio hili limetokea kikosi kutoka Zanzibar kilikuwa ndio chenye zamu ya kulinda amani katika eneo hilo, hivyo kusababisha idadi kubwa ya wanajeshi waliopoteza maisha kwa wakati mmoja kutoka Zanzibar. Katika tukio hili jumla ya wanajeshi 9 wanatoka Zanzibar waliofariki dunia.

Mhe. Naibu Spika, wanajeshi kutoka Zanzibar waliofariki dunia wanatoka katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Kusini Unguja:

1.	Sajent: Hassan Abdala Makame	-	Shehia ya Mpapa
2.	Koplo: Issa Mussa Juma	-	Shehia ya Ndijani Mseweni
3.	Private: Nassor Daud Iddi	-	Shehia ya Kitogani

Mkoa wa Kaskazini Unguja:

1.	Private: Ali Haji Ussi	-	Shehia ya Uyagu
2.	Private: Hamad Mzee Kamna	-	Shehia ya Pale
3.	Private: Juma Mosi Ali	-	Shehia ya Moga

Mkoa wa Mjini Magharibi:

1.	Private: Mwinchum Vuai Moh'd	-	Shehia ya Mitondooni
2.	Private: Iddi Abdalla Ali	-	Shehia ya Mpendae

Mkoa wa Kusini Pemba:

1.	Private: Hamad Haji Bakari	-	Shehia ya Mjimbini

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Umoja na Mataifa kwa umakini mkubwa inaendelea kuratibu matokeo yote ya kutoa matibabu kwa waliojeruhiwa kuendelea kumtafuta aliyepotea pamoja na kuzishughulikia maiti zote. Jana mnamo saa 6:30 mchana tarehe 11/12/2017 ndege iliyowabeba maiti hao iliondoka mjini Goma na kuwasili jijini Dar-es-Salam jana hiyo hiyo mnamo saa 10:00 jioni na kupokelewa rasmi na viongozi wa serikali hapo Dar es Salaam.

Mhe. Naibu Spika, kufuatia hali hiyo mnamo tarehe 14/12/2017 saa 3:00 asubuhi kutafanyika hafla maalum ya kitaifa ya kuiaga miili ya marehemu. Shughuli hii itafanyika katika Viwanja vya Jeshi Upanga jijini Dar es Salaam.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itawakilishwa na viongozi wafuatao:-

1. Mhe. Haji Omar Kheri
2. Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya
3. Mhe. Mihayo Juma N'hunga
4. Ndg. Ahmad Kassim - Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Aidha wafiwa wa wawakilishi wa askari wetu hao watajumuika katika shughuli za kuwaaga na kuwatambua ndugu zao wapendwa huko Dar-es-Salaam.

Mhe. Naibu Spika, mara baada ya shughuli hiyo maiti 8 zinazokuja kisiwa cha Unguja watasafirishwa moja kwa moja kuja Zanzibar na kupokelewa na viongozi mbali mbali wakiongozwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume. Maiti mmoja wa Mkoa wa Kusini Pemba na yeye atasafirishwa moja kwa moja kuelekea Uwanja wa Ndege wa Pemba na atapokelewa na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mapokezi hayo maiti hao watapelekwa moja kwa moja katika Viwanja vya Jeshi la Wananchi wa Tanzania viliopo Makao Makuu ya Jeshi hapa Zanzibar eneo la Migombani, ambapo patafanyika shughuli rasmi ya kiserikali ya kuwaaga wanajeshi hao ikiwemo shughuli ya ibada. Shughuli hii itaongozwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi.

Mara baada ya tukio hilo la ibada ya kuwaombea maiti wetu, Jeshi la Wananchi wa Tanzania likishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wanafamilia watasafirisha maiti hao kuelekea katika maeneo yao kwa ajili ya taratibu ya mazishi ambako huko pia viongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar watashiriki kikamilifu.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mara nyengine tena naomba kutoa pole kwa wananchi wote wa Zanzibar hasa wanafamilia wa mashujaa wetu hawa waliopoteza maisha yao wakiwa katika harakati za kulinda amani ya nchi na nchi za jirani.

Aidha, namuomba Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira wafiwa wote katika kipindi hichi kigumu. Vilevile nawaomba wananchi wote kuendelea kuwa watulivu na kuwaombea ndugu zetu hawa makaazi mema ya peponi. Amin.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya nakushukuru.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa taarifa yako.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kwanza nitoe tangazo la semina. Wakati tunaondoka hapa tunatakiwa tuelekee katika ukumbi wa juu kwa ajili ya kupata semina inayohusiana na Mswada wa Kufuta Sheria ya Uchaguzi. Baada ya hapo sasa nasitisha kikao hichi hadi saa 11:00 jioni. Ahsanteni.

(Saa 5:32 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

MWONGOZO

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa ruhusa ya kutoa mwongozo wako. Mhe. Naibu Spika, unajua toka jana tunakuwa tunajadili timu yetu ya Taifa ya *Zanzibar Heroes*. Kutokana na miongozo yako na Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameweza kuchangia takriban shilingi milioni 10.7. Kutokana na uzalendo wa mfanyabiashara mkubwa hapa Zanzibar ndugu yetu Abdulghafur Ismail kwa kuunga mkono Baraza la Wawakilishi ameweza kuchangia shilioni milioni 10 *cash* kwa ajili ya kuunga mkono Baraza la Wawakilishi. Mhe. Naibu Spika, juhudi zote hizi zinatokana na uzalendo wake, vile vile kwa juhudi ya ushajihishaji wa Mhe. Haroun Ali Suleiman. Kwa hiyo Mhe. Naibu Spika, naomba mwongozo ili nikukabidhi fedha hizi na kumkabidhi Waziri husika Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Mhe. Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru Mhe. Nassor Salim Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Kikwajuni. Nafikiri hilo suala halitaki mwongozo isipokuwa ni kumpongeza sana ambaye amekuwa mzalendo na kuweza kuchangia kiasi cha shilingi milioni 10 kwa ajili ya vijana wetu wa *Zanzibar Heroes. (Makofi)*

Mheshimiwa tunakushukuru na wewe vile vile kwa kupokea mchango huo na niseme tu, niwaombe vijana wangu sasa waupokee ili waweze kuuwasilisha katika meza yangu kwa ajili ya kuwasilisha kwa Mhe. Spika. Naomba uzipokee kwa niaba yangu huku juu kidogo mbali sana. Ahsante nakushukuru. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na hoja ya Serikali inayohusiana na Mswada wa Uchaguzi.

Hoja za Serikali

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 na Kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ametujaalia neema ya uhai na uzima, na tunamuomba atubariki ili kikao chetu hiki kifikie malengo yaliyokusudiwa.

Baada ya maelezo hayo ya shukrani kwa Mwenyezi Mungu, naomba sasa uniruhusu kumshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutukubalia kuwasilisha rasmi mswada huu wa sheria mbele ya Baraza lako hili tukufu.

Aidha, nimshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uongozi wake katika ofisi yetu. Pia Mhe. Naibu Spika, tukushukuru wewe na Mhe. Spika kwa kutuongoza vizuri katika Baraza letu hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, niruhusu nitoe shukrani za kipekee kwa Kamati yetu ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Omar Seif Abeid na Makamu Mwenyekiti wake Mhe. Panya Ali Abdalla. Kamati hii imekuwa siku zote dira katika utendaji wetu wa kazi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile uniruhusu niwashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa namna wanavyoshirikiana nasi na Serikali kwa jumla katika kufanya wajibu wetu wa kila siku.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 na Kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na masuala yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu imekuwa na historia ndefu kuhusu Uchaguzi wa Vyama Vingi vya Siasa hapa Zanzibar. Kwa mara ya kwanza uliendeshwa tarehe 22 Julai, 1957 ambao ulifuatiwa na chaguzi nyengine za vyama vingi vilivyoendeshwa tarehe 17 Januari, 1961 na tarehe 01 Juni, 1961. Na ikaendelea tarehe 08 hadi tarehe 11 Juni, 1963. Chaguzi zote hizo zilisimamiwa na Kamishna wa Uchaguzi *(Election Commissioner)* chini ya Sheria ya Baraza la Kutunga Sheria ya mwaka 1957 *(Legislative Council Election Decree, 1957).* Marekebisho yake ya mwaka 1961 na marekebisho mengine yalifanyika mwaka 1963 ya Sheria za Zanzibar, *chapter* 89.

Hivyo, katika miaka ya nyuma tumekuwa na utaratibu wa kufanya marekebisho ya sheria ili kukidhi mahitaji ya wakati na kurekebisha mapungufu yanayojitokeza. Kwa hiyo, imekuwa ni jambo la kawaida Mhe. Naibu Spika, kufanya marekebisho ya sheria pale yanapohitajika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964, Serikali ilitunga sheria ya Chama cha *Afro-Shirazi Party* ya mwaka 1965 *(The Afro-Shirazi Party Decree, 1965)* ambayo ilianzisha mfumo wa chama kimoja cha siasa. Chini ya sheria hiyo hakukuwa na uchaguzi wowote uliofanyika kwa kipindi cha miaka 17.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu wa kuchagua viongozi ulianzishwa tena mwaka 1980 kupitia Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1979, chini ya Katiba hiyo na Sheria ya Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar ya mwaka 1980 uliowezesha kufanyika uchaguzi tarehe 26 Oktoba, 1980 na tarehe 19 Aprili, 1984.

Mhe. Naibu Spika, Katiba ya Zanzibar iliyotungwa mwaka 1984, ilipelekea kutungwa kwa Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 ambayo iliweka utaratibu wa kusimamia uendeshaji wa jumla wa Uchaguzi wa Rais wa Zanzibar na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Chini ya Sheria hii ya Uchaguzi, Zanzibar iliendesha Chaguzi za Rais ya tarehe 13 Oktoba, 1985 na tarehe 21 Oktoba, 1990 chini ya mfumo wa chama kimoja.

Mhe. Naibu Spika, kufuatia mabadiliko ya Katiba ya mwaka 1992 kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa na mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho makubwa ili kukidhi haja ya kusimamia chaguzi katika mfumo wa siasa wa vyama vingi. Kupitia marekebisho ya pili ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 8 ya mwaka 1992, na baada ya marekebisho hayo chaguzi mbili za mwanzo za vyama vingi zilifanyika tarehe 22 Oktoba, 1995 na tarehe 29 Oktoba, 2000. Na baada ya hapo yalifanyika tena marekebisho makubwa ya Sheria ya Uchaguzi, na mara ya mwisho kufanyika ilikuwa mwaka 2004. Baada ya hapo, hakuna marekebisho zaidi yaliyofanyika.

Hivyo, baada ya kuonekana mapungufu mbali mbali, serikali imeamua kufanya marekebisho ili kuondoa mapungufu yaliyopo kwa kupata sheria bora inayoendana na wakati.

Muhtasari wa Sheria za Uchaguzi kuanzia mwaka 1984. Mhe. Naibu Spika, muhtasari wa Sheria za Uchaguzi ya mwaka 1984 tangu ilipotungwa imefanyiwa marekebisho mara 8 chini ya sheria za marekebisho zifuatazo:-

1. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 4 ya mwaka 1990.
2. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 8 ya mwaka 1992.
3. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 14 ya mwaka 1992.
4. Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali Nam. 5 ya mwaka 1995.
5. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 3 ya mwaka 2000.
6. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 3 ya mwaka 2001.
7. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 12 ya mwaka 2002.
8. Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uchaguzi Nam. 3 ya mwaka 2004.

Mhe. Naibu Spika, huo ni utaratibu unaotokea kila pale inapohitajika kufanya marekebisho hayo huchukua hatua za kufanya marekebisho.

Madhumuni ya Mswada huu. Mhe. Naibu Spika, madhumuni na sababu ya mswada huu ni kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 na kutunga Sheria Mpya ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mswada unaopendekezwa umekusudia kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa uchaguzi kwa kuondosha kasoro mbali mbali za sheria iliopo sasa. Mswada wa Sheria inayopendekezwa utasaidia mambo yafuatayo:-

1. Kuimarisha mfumo wa uandikishaji wapiga kura kwa kuweka bayana utaratibu wa uwekaji hadharani taarifa za wapiga kura, uhamisho wa taarifa za wapiga kura kutoka eneo moja kwenda jengine, matumizi ya daftari na uwekaji wake.

2. Mswada unakusudia kuweka maelezo ya kisheria ya kutosha yanayotofautisha baina ya Uchaguzi Mkuu, Uchaguzi Mdogo na Uchaguzi wa Marejeo. Na kuelezea kwa kina taratibu za kisheria juu ya uteuzi wa wagombea kwa nafasi zote ikijumuisha uteuzi wa Viti Maalum vya Wanawake katika Baraza la Wawakilishi na Mabaraza ya Serikali za Mitaa.

3. Mswada unakusudia kuweka maelekezo ya kisheria juu ya hatua za kuchukuliwa na Tume iwapo kutatokea jambo litakalosababisha kutokukamilika kwa uchaguzi, na kuipa Tume mamlaka ya kutolea maamuzi masuala mbali mbali ya kiuchaguzi ambayo hayakuelezwa moja kwa moja katika sheria.

4. Mswada unakusudia kuainisha makosa ya uchaguzi na kuainisha adhabu zinazoendana na makosa hayo, pamoja na kuweka utararibu wa usimamizi wa utoaji wa vibali kwa waangalizi wa uchaguzi na wajibu wao wakati wanapokuwa hapa nchini.

5. Mswada huu unapiga marufuku kwa mgombea, chama cha siasa, taasisi, au mtu mwengine yeyote kutangaza matokeo ya uchaguzi kwa njia yoyote ya mawasiliano kabla ya kutangazwa rasmi na Tume ya Uchaguzi.

   Pia mswada huu umeweka utaratibu mzuri wa kuweka mabango, *poster* na machapisho ya uchaguzi, na imeweka marufuku ya kuharibu machapisho hayo bila ya kufuata utaratibu uliowekwa na sheria.

Muundo wa Mswada. Mhe. Naibu Spika, mswada umegawika katika sura saba, na kila sura imebeba dhana inayojitegemea ili kuhakikisha msomaji anafahamu dhamira na madhumuni yaliyokusudiwa na sura hizi.

Sura ya kwanza, imeeleza utangulizi ambao unajumuisha jina fupi na kuanza kutumika na ufafanuzi wa baadhi ya maeneo ambayo yametumika katika mswada huu.

Sura ya pili, imeelezea daftari la kudumu la wapiga kura na uandikishaji wapiga kura. Sura hii inaainisha sifa za kuweza kuandikishwa kuwa mpiga kura na kufafanua taratibu za uandikishwaji wa daftari. Aidha, sura hii inafafanua taratibu za pingamizi na rufaa kwa mtu aliyekataliwa kuandikishwa na Msimamizi wa Kituo au Afisa Uandikishaji.

Sura ya tatu, inafafanua maana ya Uchaguzi Mkuu na aina nyengine za uchaguzi, na inaainisha sifa za watendaji wa uchaguzi na uajiri wao. Utoaji wa taarifa za uchaguzi na utayarishaji wa ratiba ya uchaguzi. Sura hii pia inafafanua utaratibu wa kampeni za uchaguzi, uteuzi wa wagombea, upigaji kura, kuhesabu kura, na kutangaza matokeo ya uchaguzi.

Sura ya nne, inahusiana na uangalizi wa uchaguzi na taratibu za utoaji vibali vya waangalizi. Sura hii inafafanua kwa uwazi sifa za waangalizi na uwezo wa Tume kusimamia shughuli za waangalizi. Sura hii pia inahusiana na utoaji wa elimu ya wapiga kura na taratibu zake.

Sura ya tano, inahusiana na migogoro na malalamiko ya uchaguzi. Mswada unafafanua kwa kina uwezo wa Tume kutatua migogoro ya kiuchaguzi inayotokea katika hatua mbali mbali za uchaguzi. Aidha, mswada unaelezea nafasi ya Mahkama Kuu katika kuendesha malalamiko ya Uchaguzi wa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Sura ya sita, inahusu makosa na adhabu zinazohusiana na uendeshaji wa uchaguzi. Mswada umeweka bayana makosa na adhabu yanayohusiana na uandikishaji, upigaji kura, kuhesabu kura, kutangaza matokeo, kampeni na uteuzi wa wagombea kwa mtu au taasisi yoyote itakayohusika.

Sura ya saba, inaelezea masharti ya fedha na mambo mengineyo yanayojumuisha utungaji wa kanuni, kufuta na kubakiza sheria, na mambo yaliyofanywa chini ya sheria inayofutwa.

Mhe. Naibu Spika, hitimisho. Kutungwa upya kwa Sheria ya Uchaguzi kuna umuhimu mkubwa katika kukuza demokrasia na ushirikishaji wa wahusika wa masuala ya uchaguzi. Sheria hii mpya itasaidia kuweka mfumo unaotambulika kisheria wa uendeshaji na usimamizi wa uchaguzi na shughuli zake, na hivyo kurahisisha utekelezaji wa kazi za Tume na kufikia malengo ya kuendesha uchaguzi wa wazi, uhuru na haki, na hivyo kutoa fursa kwa wananchi kutumia haki yao ya kidemokrasia kwa kuchagua viongozi wanaowataka.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu wa Sheria umeandaliwa kwa utaratibu mzuri na wepesi ili wananchi waweze kuifahamu vizuri sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kutoa hoja. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Amina Iddi Mabrouk (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa utukufu, mwenye rehma, kwa kutujaalia uzima na afya njema, na kuweza kutukutanisha tena katika Baraza hili la Tisa, kwa ajili ya lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wetu.

Aidha, nakushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam.11 ya mwaka 1984 na Kutunga Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya mwaka 2017 na masuala mengine yanayohusiana na hayo kama kanuni ya 84(7) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2016 inavyoelekeza.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru viongozi na wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na watendaji wa Tume ya Uchaguzi kwa mashirikiano yao makubwa waliyotupatia katika kuupitia na kuuchambua Mswada huu muhimu sana kwa Taifa letu. Sambamba na shukrani hizi, napenda kutumia fursa hii pia kuwapongeza sana Wadau mbali mbali waliojitokeza katika Kamati yetu na kuwasilisha maoni yao kwa lengo la kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi. Kwa kuthamini mchango wao kwa kutekeleza matakwa ya kanuni ya 83(6) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi (Toleo

la 2016) kama inavyoelekeza, ndio maana kila tunapokuwa na Mswada kwa idhini ya Baraza lako tukufu huwa tunawaalika Wadau mbali mbali ili waweze kutusaidia kuichambua Miswada hiyo kwa lengo la kupata maoni yao ili kufanya miswada hii iwe bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Mswada huu wa Sheria ya Uchaguzi ni muhimu sana kwani umekuja kuweka misingi bora ambayo inaenda sambamba na Katiba yetu ya Zanzibar. Hivyo basi, mswada huu umekusudia kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa chaguzi kwa kuondosha kasoro mbali mbali za kisheria zilizokuwepo katika Sheria ya sasa.

Mhe. Naibu Spika, aidha, azma ya mswada huu ni kuimarisha mfumo wa uandikishaji wa wapiga kura na uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura.Vile vile mswada huu umeweza kutofautisha baina ya Uchaguzi Mkuu na Uchaguzi Mdogo, pamoja na hayo umeweka utaratibu wa kisheria ambao unaweza kuchukuliwa na Tume endapo kutatokezea jambo ambalo litasababisha kutokamilika kwa Uchaguzi. Sambamba na hilo, jambo jengine ni kwamba mswada huo umeweza kufafanua zaidi kuhusiana na uchaguzi wa marudio pamoja kuainisha adhabu mbali mbali zinazohusiana na makosa ya uchaguzi na adhabu hizo zimewekwa kwa viwango vinavyohusiana na makosa yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilikaa tarehe 1 na 2 Novemba, 2017 kwa ajili ya kupitia mswada huo, baada ya mapitio Kamati ilibaini mapungufu kadhaa na kutoa ushauri ambao utaufanya mswada huu uwe bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na mapungufu hayo kamati iliagiza wataalamu wa sheria kutoka wa Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Baraza la Wawakilishi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wakae pamoja na kuzingatia maelekezo ya kamati na kufanya masahihisho katika mswada huo kama yalivyopendekezwa.

Mhe. Naibu Spika, aidha kamati iliagiza Tume ya Uchaguzi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuuchapisha upya mswada huo baada ya marekebisho yaliofanywa ambayo yaliyopendekezwa na kamati kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kulieleza Baraza lako tukufu kwamba licha ya mswada huo kuwa na masahihisho kadhaa, ambayo yalionekana ni mengi mno katika nakala ya awali na kupelekea hadi kuchapishwa upya nakala ya mswada huo, kwa kweli hakuna vifungu au maeneo ya kimantiki yaliyobadilika.

Mhe. Naibu Spika, baada ya marekebisho hayo mswada uliwasilishwa mbele ya kamati kwa mara ya pili, ambapo kamati ilipata fursa ya kuupitia tena na hatimae kuuridhia uletwe mbele ya Baraza lako tukufu kwa kujadiliwa.

Mhe. Naibu Spika, katika hatua za awali kamati ilibaini kasoro mbali mbali ambazo zilipelekea kuagiza wataalamu wa pande zote zilizohusika na mswada huu kuzifanyia kazi na hatimae kuchapisha tena mswada huo. Kasoro hizo ni tofauti ya tafsiri baina ya mswada wa Kingereza na Kiswahili, pamoja na baadhi ya vifungu vipya viliongezeka hivyo kupelekea kupanga upya nambari za vifungu vyote vya mswada huo.

Mhe. Naibu Spika, kamati imependekeza kuongeza kifungu kipya cha 2 kinachosomeka ‘’Kusomwa’’, ambapo kutokana na mapendekezo hayo yamepelekea Nakala ya Mswada kuwa na vifungu 145 badala ya 144 vya awali.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kamati ilipendekeza kufuta baadhi ya vifungu ambavyo vilionekana kwamba hakuna ulazima wa kuviweka, pamoja nakuagiza kuongezwa kwa tafsiri ya baadhi ya maneno yaliyokosekana katika mswada wa Kingereza.

Mhe. Naibu Spika, mbali ya marekebisho hayo yaliyofanywa na wataalamu kwa maelekezo ya kamati na hatimae kamati kuyaridhia, bado kamati ina maoni yafuatayo kwa dhamira ya kuimarisha mswada huo:

(i) Taasisi za kidini zisishirikishwe katika uangalizi wa Uchaguzi hivyo katika kifungu cha 100 cha mswada kamati inapendekeza kuongezwa “Kifungu Kidogo cha (5)”kitakachoweka bayana kuwa taasisi zilizotajwa hapo hazihusishi taaasisi zilizosajiliwa au zisizosajiliwa kwa madhumuni ya kusimamia au kutekeleza masuala ya kidini.

(ii) Kuhusu suala la malalamiko ya uchaguzi kamati inapendekeza kuwa “Kifungu cha 110” cha mswada kirekebishwe na kuondoa sharti la kwamba, mgogoro unaohusiana na uchaguzi wa Wawakilishi au Diwani kuamuliwa na Mahakama Kuu, na badala yake Tume ndio iwe yenye Mamlaka ya mwisho ya masuala yote yanayohusiana na malalamiko, na usiwekwe utaratibu wa kuhoji masuala hayo Mahakamani, kama ilivyo kwa upande wa uchaguzi wa Mhe. Rais ilivyo ainishwa katika katiba katika kifungu cha 34(7) na 119(13).

Mhe. Naibu Spika, pamoja na marekebisho hayo yaliyojitokeza katika nakala mpya ya mswada, kuna marekebisho mengine ya lugha na kimaandishi. Mfano katika kueleza sifa za mtu kuweza kuandikishwa katika jimbo, katika kifungu cha 12(2) kwa kufuta maneno ‘husikaikiwa ikiwa mume au mke’’ yaliyokuwepo mwishoni mwa kifungu kidogo hiki, na badala yake liongezwe neno ‘‘ikiwa’’ ili iwepo lugha nzuri inayoeleza sifa hizo. Aidha, kifungu cha 15(1) kamati ilishauri kirekebishwe kwa kuongeza maneno “katika shehia” baina ya neno “kura” na “kuwa, pia kwa kuongeza neno “hiyo” mwishoni mwa kifungu kidogo hicho.

Mhe. Naibu Spika, sambamba na hilo, kamati ilishauri kifungu cha 28(9) kinarekebishwa kwa kufuta nambari “14” iliopo baina ya neno “siku” na “tangu” na badala yake kuweka maneno “kumi na nne”.

Mhe. Naibu Spika, marekebisho mengine ambayo kamati imeyaona ni kwamba kila inapotajwa rejea ya Sheria ya Ofisi ya Tume ya Uchaguzi, ni vyema kusomeka ‘Sheria inayohusiana na Ofisi ya Tume ya Uchaguzi’

Mhe. Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii pia, kuwapongeza na kuwashukuru Wawakilishi wote katika Baraza lako tukufu, kwa kuendelea kuwawakilisha na kuwatumikia wananchi waliowachagua. Ni wazi kwamba wananchi wameonesha imani kubwa kwetu, nasi hatuna budi kurejesha imani kwao, kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote, kwa dhamira ya kutetea maendeleo ambayo ndio kiu yao kubwa. Kwa msingi huo basi, kila mmoja wetu akumbuke kuwa anadeni kwa aliyemchagua au aliyemteau kuwa Mjumbe wa Baraza hili. Hivyo,

basi kwa kuuchangia na hatiamye kuupitisha mswada huu tutakuwa tumewatendea haki wale tunaowawakilisha katika Baraza hili tukufu kwani ni mswaada wenye maslahi makubwa kwa Taifa zima.

Mhe. Naibu Spika, kazi ya kuupitia mswada huu tumeifanya kwa mashirikiano makubwa baina ya Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ambao ni wajumbe wenye kupenda kujituma na kufanya kazi kwa bidii ya hali ya juu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambue kwa kuwataja majina wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Omar Seif Abeid - Mwenyekiti
2. Mhe. Panya Ali Abdalla - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Mjumbe
4. Mhe. Ame Haji Ali - Mjumbe
5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu - Mjumbe
6. Mhe. Mussa Ali Mussa - Mjumbe
7. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Mjumbe

Aidha, kamati hii inafanyakazi na Makatibu wawili ambao wamekuwa wakitusaidia kwa kiasi kikubwa na kwa uweledi wa hali ya juu katika kutekeleza majukumu yetu ambayo yametupatia mafanikio makubwa. Makatibu wenyewe ni:-

1. Ndg. Karima Abdul-Wahab - Katibu
2. Ndg. Talib Enzi Talib - Katibu

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru tena wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha Maoni ya Kamati juu ya mswada huu ulio mbele yetu. Lakini pia kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa kunisikiliza kwa makini. Hivyo, nawaomba waupitie, waujadili, wauchangie kwa dhamira ya kuimarisha na hatimae kuupitisha mswada huu muhimu kwa ajili ya kukuza demokrasia na maendeleo katika nchi yetu, na hatimae kuwa sheria itakayotumika katika kuendesha shughuli zetu za uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi na kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa naunga mkono hoja hii. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tumeshasikia hotuba ya Mhe. Waziri pamoja na ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Sasa hivi naanza na michango ya wajumbe.

Mchangiaji wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Ali Suleiman Ali, baadae ajitayarishe Mhe. Juma Ali Khatib na atafuatia Mhe. Rashid Makame Shamsi. Mhe. Ali Suleiman karibu.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa na kuchangia Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya

Uchaguzi Nam. 11 ya mwaka 1984 na Kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na masuala mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, nakupongeza wewe kwa dhati kabisa kwa jioni ya leo kunipa nafasi na mimi kuchangia mswada huu muhimu sana katika nchi yetu, hasa tukizingatia kwamba demokrasia ni jambo la kwanza linalopigiwa kelele katika ulimwengu wetu. Lakini pia demokrasia inatakiwa lazima kutii sheria na taratibu zilizowekwa ili uende salama.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na wengineo. Lakini zaidi na mimi niipongeze Tume ya Uchaguzi kupitia watendaji wake wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na kuweza kutuletea mswada huu muhimu. Aidha, niipongeze Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora kwa kutuletea marekebisho mazuri ambapo kazi yetu imekuwa rahisi kuelekeza mambo muhimu katika mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakuwa na machache sana lakini vifungu vyangu hivyo vitanipa nafasi ya kujaza mambo mazuri ambayo yanaonekana katika mswada huu. Katika ukurasa wa 165 kifungu cha 12 "Sifa za Kuandikishwa.

Kifungu cha 12:

1. Mtu atakuwa na sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura ikiwa:-

    (a) Ni Mzanzibari amefikia umri wa miaka 18 na ataonesha kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, chini ya sheria zinazohusika na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.
    (b) Ana makaazi ya kudumu na amekuwa akiishi katika jimbo hilo katika kipindi cha miezi 36 mfululizo, yaani miaka mitatu na mfululizo kuwa huyo ni mkaazi halali ambaye anahusika, lakini na jina lake halimo katika daftari la jimbo jengine lolote lile."

Mhe. Naibu Spika, nafikiri hii ni sheria nzuri na mara nyingi huwa kuna malalamiko ya watu ambao wanakosa kupiga kura, lakini huwa kumbe anajikosesha kwa yeye mwenyewe kutokujitambua sheria iko wazi.

Mhe. Naibu Spika, leo kama mimi nahama hapa nakwenda pahala fulani, ina maana nilikokwenda pale nijiandikishe kama nimehama kule nimekuja hapa, kwa vielelezo vinavyokubaliwa na vielelezo vile vitakuwa ni ushahidi wangu tosha kwamba eneo lile nimeishi kwa muda unaotakiwa. Lakini vyenginevyo ukifanya lolote kwa nguvu zako ni kosa. Kwa hivyo, niseme tu napongeza kwa dhati hili la kuhakikisha kwamba haya yaliyopangwa ni muhimu na yana maana katika kuendeleza utaratibu ambao umewekwa kwa ajili ya uchaguzi wetu.

"2. Bila ya kujali maelekezo ya kifungu (1)(d) cha kifungu hiki, mtu atachukuliwa kuwa ana sifa za kuandikishwa katika jimbo."

Mhe. Naibu Spika, nisamehe sana ikiwa nitakuita Mwenyekiti. Naomba nirudie kidogo mheshimiwa.

…ana sifa za kuandikishwa katika jimbo husika ikiwa mume au mke.

(a) Ana ndoa na anaishi katika jimbo hilo mradi mwenza wake wa ndoa ni mkaazi wa kudumu wa eneo la uandikishaji;

(b) Anaishi katika jimbo kutokana na sababu za ajira;

(c) Ni mtegemezi wa mmoja wa watu wote ambao wameelezwa katika aya ya (a) mpaka (d).

3. Kwa madhumuni ya kifungu (2)(b) kwa kifungu hiki mtu atakuwa na sifa zinazotokana na misingi ya ajira, iwapo ni afisa ambaye amepata uhamisho wa kikazi, na inahusisha Wanajeshi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania JWTZ, Afisa Usalama wa Taifa, Jeshi la Polisi la Tanzania na Idara Maalum.

(b) Inaeleza vile vile ni mfanyakazi wa serikali au muajiriwa wa Shirika la Kimataifa ambaye amepata uhamisho kutokana na kazi zake;

(c) Ni mwanamke aliyeolewa au mwanamme aliyeoa na mtu ambaye ana sifa ya kikazi aliyehamishiwa katika eneo jengine, kutokana na uhamisho wa mume au mke wake."

Mhe. Naibu Spika, hayo yote ni sifa za mtu ambaye katika uandikishaji anakubaliwa bila ya matatizo yoyote.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika mambo haya yote kuna mambo katika kifungu cha 4 ambayo yanasema hivi:

Kifungu cha 4:

"Mtu ambaye kwa madhumuni ya sifa ya ukaazi hana sifa ya kuandikishwa katika jimbo analoishi sasa, anaweza kurejea katika jimbo la zamani na kuandikishwa kuwa mpiga kura na atakuwa na haki ya kuandikishwa katika jimbo hilo."

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme tu kwamba mswada huu ni mzuri na mswada huu umeondoa adha na umeondoa matatizo ambayo mtu anajitafutia mwenyewe. Kwa hivyo, niwaombe sana wananchi wetu ambao wanasikia au wanataka kujua mswada huu, wautafute na waujue ili twende vizuri katika demokrasia yetu ya uchaguzi. Kwa hivyo, napongeza sana kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 14 ukurasa wa 166 huo huo kinasema hivi:

Kifungu cha 14:

"Sheha kuwa wakala wa uandikishaji kwa wadhifa wake".

Mhe. Naibu Spika, mimi hili nalipongeza sana, napongeza kwa moyo wangu wote. Haiwezekani hata siku moja katika kituo cha uandikishaji Sheha akawa nje ya eneo, Sheha ni mhusika namba moja katika eneo lile, atamjua Shihata, atamjua na mwengineo. Kwa hivyo, sheha ni mdau wa kwanza. Mimi naipongeza sana Tume kwa kuliona hili kwamba Sheha ni mtu ambaye awe mwanzo katika kuhakikisha kwamba yupo karibu katika uandikishaji kwa wadhifa wake aliokuwa nao.

Pia niseme tu kwamba katika kutekeleza haya kutakuwa kuna mambo mengi ambayo yanahusiana na shughuli zao. Kwa mfano, katika jimbo langu au jimbo lolote Sheha ni mmoja, lakini Sheha ana Kamati ya Shehia wajumbe wake. Kwa hivyo kama nitakuwa nina vituo vinne au vitano, basi naamini Kamati yake Sheha kwa wale wajumbe wake, pia ni wadau ambao watamsaidia yeye na kuhakikisha kwamba kazi ile inakwenda vizuri bila ya kutokea matatizo. Kwa sababu kila mtu ana eneo lake na watu wa maeneo yale atakuwa huyu Msaidizi wa Sheha anawajua watu wale wanaoingia katika maeneo yale bila ya matatizo. Kwa hivyo, niseme kwamba hii ni hatua nzuri ambayo itatusaidia.

Jengine Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 167 kifungu cha 16. Watu wanaoruhusiwa katika kituo cha uandikishaji. Hii imeeleza wazi kwamba Afisa Uandikishaji, Karani Uandikishaji, Sheha, Wakala Uandikishaji, muombaji, mtu anayemsaidia muombaji mwenye mahitaji maalum, mwangalizi aliyeidhinishwa na maandishi na Tume, Mjumbe wa Tume, Mkurugenzi wa Uchaguzi, Askari Polisi au Afisa yeyote wa Usalama atakayekuwepo kituoni kwa ulinzi au mtu mwengine yeyote atakayeidhinishwa na Tume.

Mhe. Naibu Spika, huu ni utaratibu ambao bado ni mzuri na utaratibu huu utatusaidia kuondoa kasoro za hapa na pale. Mhe. Naibu Spika, katika kitu ambacho kinaelekeza kusimamia ni jambo muhimu sana na tukisimamia vyema utata na matatizo ya hapa na pale yataondoka. Kwa hivyo, naomba tu hili litekelezwe ili twende vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nataka kuchangia kwa haraka haraka kifungu cha 82. Kifungu hiki ni muhimu sana. Naomba nikinukuu kama kilivyo kinasema:

Kifungu cha 82:

"Kura ya Mapema".

Mhe. Naibu Spika, nataka hapa tuelewe wazi kwamba kupiga kura mapema ina mambo yake yafuatayo. Tume itaweka utaratibu utakaoruhusu upigaji wa kura wa mapema ambao utafanyika siku moja kabla ya siku ya upigaji kura au siku nyengine yoyote itakavyoamuliwa na Tume.

2. Upigaji kura wa mapema chini ya kifungu kidogo cha 1(1) cha kifungu hiki utatumika katika Uchaguzi Mkuu au Uchaguzi Mdogo wa Rais pekee na utahusisha:

(a) Wapiga kura wanaotekeleza majukumu ya uchaguzi kama Msimamizi wa Uchaguzi, Msaidizi Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Askari Polisi, Mjumbe au Mtendaji wa Tume.

(b) Mpiga kura ambae atahusika na kazi za ulinzi na usalama siku ya kupiga kura."

Mhe. Naibu Spika, hili ni muhimu tumeshuhudia inapofika wakati wa uchaguzi watu wetu au wananchi wengi wanakosa haki yao ya kupiga kura kutokana na kupangwa katika maeneo mbali mbali ya maeneo yao. Kwa hivyo, hili hata tukija katika mambo ya ulinzi na usalama nchi yoyote inategemea ulinzi na usalama, na mpiga kura anataka awe katika makaazi mazuri na kuhakikisha kwamba anakwenda kupiga kura anarejea kwake salama. Kwa hivyo, hili naiomba sana Tume ilifanyie kazi haraka watengeneze taratibu zao ili liondokane na shughuli ambayo itakwenda vizuri na kuwanufaisha wananchi wetu ambao wanafanya shughuli mbali na maeneo yao.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi nimesema tu mwanzo kwamba nitakuwa na mchango mdogo. Lakini la mwisho kabisa kabla hujanipigia kengele, naomba niseme tu ukurasa wa 208 kifungu cha 127 "Utangazaji wa Matokeo Kinyume na Sheria". Naomba ninukuu Mheshimiwa kwa ruhusa yako.

1. Ni marufuku kwa mgombea, chama cha siasa, taasisi au mtu mwengine yeyote, kutangaza matokeo ya uchaguzi kwa njia yoyote ya mawasiliano kabla ya kutangazwa rasmi na Tume"

Mhe. Naibu Spika, napongeza na ndivyo ilivyo Tume ndio yenye mamlaka na Tume ndio mwanzo na mwisho wanaotoa tangazo la matokeo ya uchaguzi.

2. Mgombea Chama cha Siasa, Taasisi au mtu mwengine yeyote atakayetangaza matokeo ya uchaguzi au kuitaka Tume kutangaza matokeo kabla ya kwisha kwa muda wa kutangaza matokeo uliopangwa, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atapata moja kati ya adhabu zifuatazo:

    (a) Ikiwa mgombea atatumikia kifungo kwa muda usiopungua miaka mitano na faini isiyopungua shilingi milioni hamsini…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Ali Suleiman Ali: La mwisho Mheshimiwa naomba radhi.

    (b) Ikiwa Chama cha Siasa au taasisi, adhabu isiyopungua shilingi milioni mia moja.

    (c) Ikiwa mtu mwengine, anatumikia kifungo kisichopungua miezi 18."

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono haya yote lakini naomba niongeze moja zaidi, ikiwa mgombeahuyu kagombea ngazi ya Urais. Namuomba sana Mhe. Waziri akifika lengo hilo kuthubutu kwenda kutangaza matokeo anakotaka yeye bila ya idhini afungiwe kugombea maisha yake katika nchi hii, asiwe mgombea wa chama chochote katika nchi hii kwa sababu analeta hatari na anahatarisha amani na utulivu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache narudia tena kusema tu kwamba naipongeza sana Tume yetu ya Uchaguzi kwa kutuletea mswada huu ambao madhumuni yake kuongeza demokrasia katika nchi yetu kwa kuleta amani na utulivu katika chaguzi zetu. Baada ya hayo naipongeza na naunga mkono kwa asilimia mia moja mimi na wananchi wangu wote wapenda amani wa Jimbo la Kijitoupele. Ahsante Mheshimiwa. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika. Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Juma Ali Khatib, atafuatia Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Mheshimiwa karibu.

Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na wenye afya njema na kukutana leo hapa kuzungumzia jambo muhimu lenye maslahi na nchi yetu na taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza natoa pongezi kwa Tume ya Uchaguzi kwa kazi kubwa wanayofanya ya kusimamia chaguzi zetu mbali mbali za Unguja na Pemba. Tume ya Uchaguzi tokea mwaka 1995 mimi nilibahatika kufanya nao kazi nikiwa mdau wao wa vyama vya siasa wamekuwa wakifanya kazi hii kwa nia nzuri na safi na mazingira magumu sana. Lakini kwa uzalendo wao wamekuwa wakifanya juhudi kubwa sana kuendesha chaguzi hizi kujitahidi kupunguza matatizo, pamoja na kwamba sisi baadhi ya vyama vya siasa tumekuwa kidogo tuna mambo yetu yale ya kisiasa ya msuguano suguano pale panapoundwa Tume za Maadili katika vyama vya siasa wakati wa uchaguzi, lakini baadhi ya wagombea tumekuwa tukivunja maadili ya uchaguzi na matokeo yake kuiweka Tume ya Uchaguzi katika wakati mgumu.

Mhe. Naibu Spika, suala hili limekuja wakati muafaka kwa sababu dunia inakwenda mbele na sisi nchi yetu inakwenda mbele, hatuwezi kila siku tukawa na sheria zile zile wakati mambo yanabadilika, wapiga kura wanaongezeka na demokrasia inakua sana. Napenda kutoa pongezi kwa Serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuendesha Serikali hii katika mfumo wa kidemokrasia yenye kujali mfumo wa vyama vya siasa. Jambo hili ni kuonesha kwamba kiongozi wetu Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein ni mtu anayetekeleza Katiba kwa vitendo na hili halitaki tochi, kwa sababu tunaona mara nyingi mambo mengi yanapotokezea haitoki amri isipokuwa kila kitu kinaletwa katika chombo hichi cha kutunga sheria na ndio maana leo tuko hapa tunajadili Sheria ya Tume ya Uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza nataka nizungumzie kuhusu mapitio na mipaka ya majimbo. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyowekwa kabla ya 2015 ya uchaguzi wakati wa kukata mipaka kwa majimbo, lakini kuna kasoro kadhaa wa kadhaa zilitokezea sisi kama wadau wa Tume ya uchaguzi tulipeleka malalamiko nyakati mbali mbali kwa Tume ya Uchaguzi kwamba hatukuridhika na jinsi majimbo ya uchaguzi yalivyokatwa. Kwa hivyo sasa ni wakati muafaka. Kwanza hoja yangu ni kwamba sasa ni zaidi ya miaka mitano tutakapoingia katika uchaguzi itakuwa idadi ya watu wameongezeka wapiga kura katika majimbo. Mhe. Naibu Spika, ukizingatia idadi yetu ya sensa ya watu tunaongezeka mwaka hadi mwaka, kwa hivyo sasa ni wakati muafaka tuangalie upya mipaka yetu ya majimbo ili kuweka usawa idadi ya wapiga kura.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii ni nzuri kwa sababu imeandaa utaratibu wa uandikishaji ambao kuna haki nyingi sana za kila mtu mwenye sifa za kuandikishwa ataweza kujiandikisha. Tumeona kwamba Sheha atakuwa ni wakala wa uandikishaji kwa sababu yeye ndio anayefahamu wale wapiga kura wanaokaa katika jimbo lake. Halafu isitoshe Mhe. Naibu Spika, Sheha ni kiongozi wa Serikali. Kwa hivyo, ili kuondoa utata na kuondoa msuguano hasa kwa sisi vyama vya siasa washabiki na wanachama wetu, ni vizuri Sheha kushirikishwa katika zoezi la uandikishaji.

Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia suala la mawakala katika zoezi la uandikishaji na wapiga kura kuna kasoro kadhaa wa kadhaa zilijitokeza katika baadhi ya chaguzi zetu. Kwa mfano uchaguzi wa mwaka 2015 hadi kufikia saa nne naa, kuna chama kimoja kilikuwa bado vitambulisho vyao mawakala hawajapewa, na sio kama hawakupewa, lakini ilifanyika *sabortage* kwa wale watu waliotaka kuitia doa Tume ya Uchaguzi kwa sababu suala hili haliko kwa wale watendaji wakuu, lipo kwa wale waliokabidhiwa. Kwa sababu vitambulisho vilitengenezwa vilikuwepo lakini alitokezea mtu mmoja akavificha kwa maslahi yake mwenyewe na chama chake. Kwa hivyo, jambo hili lilitia doa sana uchaguzi wake na hapo ndipo ilipoanza kasoro.

Mhe. Naibu Spika, tukienda suala hilo hilo la mawakala wagombea wa uwakilishi na madiwani wana mipaka, wakala wa mgombea wa uwakilishi mipaka yake ni katika lile jimbo husika. Lakini Mhe. Naibu Spika, wakala wa Mgombea wa Urais mipaka yake ni Unguja na Pemba. Sasa jambo la kusikitisha kwa masikitiko makubwa mimi nikiwa kama mgombea uchaguzi wa mwaka 2015 kutokana na sheria hazikuwa vizuri, basi mawakala wa chama chetu *TADEA* walitolewa kwenye vituo hususan kule Pemba wakapigwa karibu ya kuuwawa, tukapeleka kesi Polisi, tukapeleka malalamiko Tume ya Uchaguzi. Kwa hivyo, sisi kwa niaba ya chama chetu tunafurahi sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuleta mswada huu wa mabadiliko ya sheria hii. Ni jambo sahihi, ni jambo linalokwenda na wakati litatuondolea misuguano ya kisiasa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sisi sote ni wamoja lakini inapofikia wakati wa uchaguzi bilisi anatukumba tunakuta kwamba tunasuguana. Kwa hivyo, mimi naamini kwamba sheria hizi zitatuweka pazuri sana tutaondokana na yale matatizo yaliyokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, vile vile nataka kuzungumzia mambo mazuri yaliyokuwemo katika sheria hii na watu wanaoruhusiwa katika vituo vya uandikishaji. Sasa hivi kuna idadi maalum imetajwa katika sheria yetu hii wale watu watakaokuwemo katika kituo cha uandikishaji. Kwa hivyo, hili ni jambo zuri kwa sababu tulishuhudia hasa kule Pemba wakati wa uchaguzi uliopita ukiingia katika kituo cha kupigia kura utakuta kuna wale mawakala wanaojulikana na wasimamizi na wale waangalizi, lakini wengine hawana vitambulisho ukimuuliza anakwambia nina kazi maalum. Hapa ndipo tulipoanza sisi kuharibika uchaguzi wetu uliopita. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, sheria hii sasa naamini kwamba itatuweka pazuri na uchaguzi wa mwaka 2020 Mwenyezi Mungu akitujaalia wale watakaokuwa hai, basi naamini nchi yetu itaingia kwenye uchaguzi bila ya msuguano wa kisiasa na bila ya malumbano.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka kuzungumzia uamuzi wa Tume ya Uchaguzi juu ya rufaa. Hili ni jambo zuri sana kwa sababu mara nyingi zinapokuja rufaa zilikuwa kidogo hazipati mwelekeo mzuri, lakini sasa katika sheria hii kutakuwa na sheria nzuri sana,vile vile kuweka wazi orodha ya waombaji hili ni jambo zuri. Malalamiko dhidi ya orodha ya kuwekwa wazi hili ni jambo zuri, pingamizi kwa muombaji hili ni jambo zuri, kuingiza katika daftari hili ni jambo zuri Mhe. Naibu Spika. Kwa mfano kitambulisho kilichopotea au kuharibika, hii sheria ni sheria nzuri ambapo napenda kunukuu katika kifungu cha 24 ukurasa wa 169 Mhe. Naibu Spika, inasema:

"1. Pale ambapo kitambulisho cha mpiga kura ikiwa kimepotea, kimechafuka au kuharibika, mpiga kura anaweza kuomba yeye mwenyewe kwa Afisa Uandikishaji kupatiwa kitambulisho kipya cha kupigia kura.

2. Endapo Afisa wa Uandikishaji ataridhika na maombi yaliyofanywa kulingana na maelekezo ya kifugu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atampatia muombaji kitambulisho kipya cha kupiga kura baada ya muombaji kulipia ada iliyowekwa kwa kukabidhi kitambulisho kilichochafuka au kuharibika.

3. Maombi yaliyofanywa chini ya kifungu hichi yatawasilishwa katika fomu maalum iliyotayarishwa kwa mujibu wa Kanuni zilizotayarishwa."

Mhe. Naibu Spika, sheria hii ni nzuri sana napenda kuipongeza Tume ya Uchaguzi, napenda kuipongeza Serikali kwa sababu sisi wanasiasa mara nyingi tulikuwa tukitumbukia katika malumbano kutokana na tatizo kubwa tulikuwa hatuna sheria. Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, leo tunapoingia kwenye uchaguzi kila mgombea anafahamu kwamba mwenye mamlaka ya kutangaza Mgombea Urais ni Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi, hizi sheria kama vyama vya siasa tunapewa, tunapewa maadili ya uchaguzi, tunapewa sheria za uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, lakini kutokana na kwamba hapakuwa na sheria madhubuti tunajikuta kwamba wagombea wengine tunajitangazia ushindi. Mhe. Naibu Spika, jambo hili ni hatari kwa sababu ikiwa sheria zipo halafu hatuzifuati ni kuifanya nchi yetu kuingia katika msuguano wa kisiasa uliokuwa hauna tija. Kwa hivyo, kilichopo sasa ni kwamba ikipita sheria hii namuomba Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aisaini haraka ili kuiweka nchi yetu katika mazingira mazuri ya uchaguzi wa 2020. Atakapotokezea kiongozi yeyote yule wa kisiasa au mgombea akajitangazia yeye kwamba kashinda kinyume na sheria yetu tunayoitunga hapa, basi vile vyombo husika vifanye wajibu wake ili kuondosha matatizo ya siasa.

Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na matatizo sisi wagombea hususan wa Uwakilishi, Udiwani na Urais pale wakati wa kampeni ambapo huwa Tume ya Uchaguzi inaita vyama vya siasa inakaa navyo, wanajitahidi kutoa elimu ya uchaguzi lakini wakati wa kwenda kubandika picha zile kuna wengine wanakuwa wanapita usiku wa manane kupachua picha za wagombea wa vyama vyengine na kupachika picha zao. Jambo hili sio zuri katika uchaguzi huru na wa haki. Jambo hili ni viashiria vya ugomvi, jambo hili ni viashiria vya kuiweka nchi yetu pabaya, lakini sheria hii sasa itakuwa ni dawa kuondokana na matatizo yale Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii kusema kweli sasa imekuja wakati muafaka kutokana na mikwaruzo mingi sana ya kisiasa. Sisi vyama vya siasa tulitumbukia katika dimbwi baya sana ikaja mazungumzo ya Tume ya Muafaka ile ya CCM na CUF. Mimi napongeza sana wakati ule mambo yalikuwa mazuri lakini sasa ni wakati mwengine inabidi tubadilike tuweke sheria nyengine zinazokwenda na wakati huu. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, nchini Tanzania tuna vyama 18 vya siasa sasa vyenye usajili wa kudumu, tukisema kwamba leo sheria iliyoko kwamba pale kuwa na vyama viwili au vitatu tu katika Tume ya Uchaguzi, hili jambo kwa sasa halileti tija wala halipanui misingi ya demokrasia kwa vyama vyengine vya siasa ndio maana ukaona sasa kunatokezea misuguano ndani ya Tume ya Uchaguzi. Tulizowea hapo siku za nyuma kwamba Tume ya Uchaguzi hakuna wanasiasa, kulikuwa kuna watu wenye sifa za kisheria wanaochaguliwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar.

Lakini Katiba iliyokuja kufanyiwa marekebisho madogo basi ndio tukaamua sasa kwa wakati ule kuwe na wanasiasa, lakini tujiulize tumepata tija gani tulipoamua sasa kuweka viongozi wa kisiasa katika Tume ya Uchaguzi, ndio maana yakatokezea haya yaliyotokezea mivutano isiyokwisha, chuki na uhasama.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika mbili.

Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante Mwenyekiti, mimi nipo katika kusimamia na katika kuonesha kwamba sheria hii ni nzuri, sheria hii itatuondolea misuguano ya kisiasa isiyokwisha katika nchi yetu. Ni aibu kuona kwamba Zanzibar ni nchi

ndogo watu wake ni wamoja, watu wa Unguja na Pemba wote ni wamoja, lakini leo ndani ya familia moja tunalumbana tu kwa sababu ya itikadi za kisiasa hili si jambo zuri. Sisi viongozi wa kisiasa tusiwatie sumu wale wanachama wetu kwa kuwajengea chuki na kuwabagua, sisi kama viongozi wa kisiasa tujaribu kuwaweka Wazanzibari wawe kitu kimoja inapofika wakati wa kampeni tutangaze sera zetu, tunadi ilani zetu ili kuomba kupigiwa kura.

Lakini tukimaliza uchaguzi Mhe. Naibu Spika, tuheshimu matokeo ya Tume ya Uchaguzi na tuheshimu matokeo ya Wazanzibari kwa yule kiongozi waliyemchagua. Kwa hivyo, sisi wengine ikiwa tumeshinda au tumeshindwa tumpe mashirikiano yule kiongozi aliyechaguliwa hususan Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ili kujenga misingi imara na kujenga misingi mizuri ya mustakbali wa taifa letu kwa sababu tumeanza siasa ya mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 pamoja na nia nzuri iliyokuwepo wakati huo.

Mhe. Naibu Spika, nakumbusha jambo moja tu CCM ndio chama kilichokuwepo madarakani lakini wakati ule watu walivyohojiwa asilimia 80 walitaka mfumo wa chama kimoja, asilimia 20 wakataka mfumo wa vyama vingi. Lakini kwa nia njema ya Chama cha Mapinduzi na Serikali zake zote mbili wakaridhia yale maoni ya watu wachache asilimia 20 ikaja mfumo wa vyama vingi. Kwa hivyo na mimi naamini kwamba sheria hizi ni nzuri hasa kwa vyama vyetu ukizingatia kwamba vyama vyote vya siasa viko sawa, isipokuwa mtaji wa chama cha siasa ni kuwa na wanachama wengi, lakini haijalishi wala haipaswi kwamba udharau chama chengine. Kwa hivyo nataka kuwaomba Wawakilishi wenzangu kwa pamoja tushirikiane. Napenda sana kuwashukuru Wawakilishi wa awamu hii ya saba wamekuwa ni Wawakilishi mahiri na wachapakazi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Juma Ali Khatib: Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa kusema wakati tunaingia ndani ya Baraza hili kuna baadhi ya watu wa vyama fulani walifika kubeza Baraza hili. Matokeo yake tumeliona hili ni Baraza lililotukuka na linalofanya kazi vizuri na serikali hii inafanya kazi vizuri. Kwa sababu ndani ya serikali hii kinachokubaliwa basi ndio hicho hicho, hakuna kiongozi yeyote anayetoka ndani ya serikali akakaa kwenye jukwaa akaikosoa serikali. Tumeona serikali ya awamu iliyopita watu walikuwa wanakubaliana lakini baadae wakitoka jioni wanakaa kwenye majukwaa wanaisema serikali yao wakati wao wamo ndani ya serikali.

Kwa hivyo, nawaomba Wawakilishi kwa pamoja sote tuondoe tofauti zetu, humu ndani hakuna chama cha siasa, humu kuna Wawakilishi. Kwa hivyo, tupitishe sheria hii na tukisha kuipitisha Mhe. Naibu Spika, tumuombe Mhe. Rais aisaini kwa haraka ili hatua za utekelezaji ziendelee.

Ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, sasa atachangia Mhe. Rashid Makame Shamsi na baadae ajitayarishe Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia katika Mswada huu wa Sheria ya Uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze sana Wizara inayohusika na kuletwa kwa sheria hii. Lakini vile vile nimpongeze Waziri na watendaji wake wote kwa kuweza kuandaa sheria hii muhimu kwa taifa.

Pia nichukue fursa hii kuwapongeza Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa hotuba yao ya maoni ambayo imesheheni mapendekezo mbali mbali. Lakini kwa uzito wa aina yake niwapongeze Wajumbe wenzangu waliotangulia na hususan Mhe. Juma Ali Khatib Mwakilishi wa Kuteuliwa na Rais kutoka Chama cha *TADEA* kwa msisitizo wake juu ya umuhimu wa kuwepo kwa sheria hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mswada huu kama walivyotangulia kusema wenzangu ni muhimu sana katika mustakbali wa taifa hili, mimi michango yangu naomba iwe kama ifuatavyo.

&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&

Katika Sura ya Kwanza, nakumbusha tu kwa sababu mara kwa mara huwa nakumbusha suala la uwekaji wa *alphabetical order* katika maneno ambayo yametolewa tafsiri. Lakini vile vile katika eneo hilo napendekeza neno “Mzanzibari” litolewa tafsiri na neno “Mzanzibari wa kuzaliwa” litolewa tafsiri kutokana na umuhimu wake na jinsi lilivyozungumzwa katika Sheria hii, ili huko baadaye tusijetukapata utata juu ya maneno haya mawili.

Mhe. Naibu Spika, nikija ukurasa wa 162 katika neno “muangalizi wa ndani”. Napenda nitoe mapendekezo ya marekebisho kidogo baina ya neno “inajumuisha na taasisi”, palikuwa pana maneno ambayo yamekosekana hapo, isomeke kwamba “inajumuisha muangalizi kutoka taasisi za ndani”. Kwa sababu tafsiri inayozungumziwa ni neno “muangalizi wa ndani”. Kwa hivyo isomeke hivyo “inajumuisha muangalizi kutoka taasisi za ndani” na kuendelea.

Mhe. Naibu Spika, katika tafsiri ya neno “uchaguzi”, “uchaguzi maana yake ni”, kuna neno “ni” halipo naomba liwepo. Lakini vile vile kutokana na ile *version* ya Kingereza ningependa Mwanasheria aipitie tena ile tafsiri ambayo imetolewa ili iendane na ile *version* ya Kingereza kwa sababu kuna neno “*rerun*” kuna “*by election”* na kuna “*rerun”* ambayo nafikiri itakuwa kuna mapungufu kidogo ya hiyo tafsiri.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika ukurasa wa 167 katika kifungu cha 17 mstari wa mwisho kabisa limekosekana neno “fomu” ambalo linatakiwa liwe nyuma ya neno “inayoelekeza” na lisomeke “fomu inayoelekeza” kutokana na neno la Kingereza “*prescribe form”* katika *version* ya Kingereza ukurasa wa 221.

Mhe. Naibu Spika, nielekee sasa katika ukurasa wa 170 katika kifungu cha 28(6) mstari wa mwisho, “itakavyoelekezwa” nilikuwa napendekeza pawe na maneno “itakavyoelekezwa katika Kanuni zitakazotayarishwa na Tume”. Lakini tukija ukurasa wa 170 Kifungu cha 31 kifungu 2(a) neno “maswali” lisomeke “masuala ya vizazi na vifo”.

Mhe. Naibu Spika, nikija ukurasa wa 172 katika kifungu cha 33 mstari wa pili neno la tatu nilikuwa napendekeza baada ya kuwekwa neno “sababu ya kuolewa”, kutokana na *version* ya Kingereza imesema *marriage,* mimi napendekeza isomeke "ndoa". Kwa sababu mtu aliyeandikishwa kuwa mpiga kura na jina lake litabadilika kwa sababu za ndoa sio za kuolewa. Kwa sababu jina linaweza likabadilika la mwanamme au jina linaweza likabadilika la mwanamke kutokana na suala la ndoa. Lakini vile vile katika mstari huo huo maneno ambayo yanayosomeka “hajafutwa kupiga kura”, napendekeza yasomeke kwa mujibu wa vifungu vya Sheria yasomeke hajaondolewa katika daftari la kupiga kura na maneno “hajafutwa kupigwa kura” yaondoke.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kutoa michango yetu ya marekebisho ya Mswada huu nije katika ukurasa wa 176 katika kifungu cha 43 ambacho kinazungumzia sifa za mgombea wa Urais. Katika kifungu hichi sifa zimenukuliwa katika Katiba ya Zanzibar Ibara ya 26 (2). Katika kifungu (d) kuna maneno ambayo katika Katiba yamo lakini katika hii sheria hayamo nayo ni ile “vyama vya siasa ya 1992”, haya yamo katika Katiba. Kwa hivyo hiyo *statement* imalizikie hivyo, "...vyama vya siasa vya 1992", kama tumenukuu katika Katiba.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 44 naleta msisitizo tena kwa nafasi ya mgombea au Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, nilikuwa napendekeza kama ilivyo katika sifa ya (a) ya Rais. Mgombea wa nafasi hii awe ni Mzanzibari wa kuzaliwa. Hoja yangu ni kwamba vitambulisho vingi vya Uzanzibari tumevitoa kwa makosa na wakati mwengine vitambulisho hivyo ndivyo ambavyo vinampelekea mtu kufahamika kama ni Mtanzania na anaweza akaingia nafasi ya Uwakilishi akaja akaendelea mpaka tukajatukaona kwamba anatufaa kuwa Rais, lakini kumbe siyo Mzanzibari wa kuzaliwa. Kwa hivyo tuchukue tahadhari hiyo mapema ili vizazi vyetu visije vikakuta misukosuka. Kwa sababu hii Sheria kwa mujibu wa Katiba, kwa nini Rais akawa Mzanzibari wa kuzaliwa ina maana yake. Hivyo tuweke tahadhari mapema kwa nafasi ya Uwakilishi, mimi naomba sana Mzanzibari awe ni wa kuzaliwa yule ambaye atagombea nafasi hiyo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 177 kifungu cha 47 (4) mstari wa mwisho ambapo inazungumzia suala la Kanuni. Napendekeza kwamba kama itakavyoelekezwa katika Kanuni zitakazotayarishwa na Tume.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 186 kifungu cha 71 kwenye vifaa vya kupigia kura nilikuwa napendekeza katika kifungu hicho cha 1 ambacho kinasomeka “Tume kwa madhumuni ya uchaguzi itapanga na kununua vifaa vya kupigia na kuhesabu kura vya kutosha”. Mimi napendekeza baada ya vya kutosha lakini vile vile na vyenye ubora. Kwa tunaweza tukaja tukawa na vifaa vya kutosha lakini kumbe vifaa vyenyewe havina ubora au viwango ambavyo vinavyotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu cha 73(1) ambacho kinasomeka, “Tume itanunua masanduku ya kupigia kura kwa matumizi ya kupigia kura”. Kifungu cha matumizi ya masanduku tayari kimetajwa katika kifungu cha 71, kwa hivyo hakuna ulazima wa kifungu hichi kuwepo kwa sababu huku tayari imeshasemwa itapanga na kununua vifaa vikiwemo hayo masunduku. Kifungu hichi napendekeza kiondoke ili kuondosha *repetition* katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 74 kuna suala la kituturi, hichi kituturi kimeelezwa lakini kituturi mara nyingi kinatembea na kalamu. Kwa hivyo hichi kifungu cha kuweka kalamu katika kituturi lazima kiwekwe hapa ili kuwe na kifaa ambacho kitatumika na mpiga kura katika kuweza kupiga au kufanikisha suala la kupiga kura. Neno katika kifungu cha 2(b) ambacho kinasomeka misingi ya kura ya siri isomeke, "inalindwa" na isiwe kama ilivyo kwamba "inalinda", lakini iwe "inalindwa".

Mhe. Naibu Spika, nikija katika ukurasa wa 199 katika kifungu cha 100 kifungu cha 2(d) Uzoefu wake katika masuala ya uangalizi wa uchaguzi usiopungua miaka 3. Hapa anazungumziwa muangalizi wa uchaguzi yaani awe na uzoefu wa masuala ya uangalizi wa uchaguzi usiopungua miaka mitatu. Napendekeza baada ya kuwekwa miaka mitatu iwe ni vipindi vitatu vya uchaguzi au chaguzi tatu. Nafikiri ndivyo itakavyokaa kimantiki kuliko hivyo ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie katika ukurasa wa 200 sehemu ya elimu ya wapiga kura. Kwanza nirekebishe neno la pembeni ambalo linasomeka "Mtwala" na lisomeke "mtaala". Katika suala zima la elimu kwa wapiga kura Sheria imekaa vizuri sana, lakini tukumbuke tu kwamba katika kipindi cha uchaguzi zinatokea taasisi nyingi kuweza kuleta maombi ya kuweza kutoa elimu kwa wapiga kura na hususan *NGO's* mbali mbali. *NGO's* nyingi mpaka za mifukoni huwa zinazuka katika kipindi hichi kutaka kutoa elimu kwa wapiga kura. Tukumbuke kwamba *NGO's* nyengine zina nia njema, lakini *NGO's* nyengine hazina nia njema na nchi hii. Ningependa sana katika kutoa vibali, kwanza elimu hiyo isitolewe mpaka ihakikishwe kwamba inafuata mtaala wa Tume ya Uchaguzi.

Vile vile pale ambapo wanatoa elimu lazima kuwe na mtumishi wa Tume ili kuhakikisha kwamba mafunzo yanayotolewa ni yale yanayoendana na matakwa yetu. Tukiacha ovyo katika hili basi kuna hatari ya watu wengi kupotoshwa na watu hawa au vikundi hivi wakati mwengine vinafadhiliwa na wahisani mbali mbali katika kutoa elimu. Wakati mwengine wanaelekezwa maeneo maalum ya kwenda kutoa elimu, Sheria hapa inatakiwa isimamie vizuri.

Mhe. Naibu Spika, hata ile adhabu ambayo imewekwa katika kifungu cha 132 ukurasa 210. Ile adhabu iliyowekwa ni ndogo sana kwa watu wa namna hii. Kwa sababu mtu atakapochukua nafasi ya kupotosha halafu unamwambia adhabu yake isizidi milioni tano na isipungue laki mbili, maana yake hiyo ni adhabu ndogo sana. Huyu keshapotosha na anaweza akaleta fujo. Hata hii adhabu ambayo imependekezwa kwa mtu ambaye atakwenda kinyume na taratibu zile za kutoa elimu, basi adhabu hii ndogo na napenda irekerebishwe ili iwe inaendana na hiyo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nimalizie katika hoja ya rushwa. Katika hoja ya rushwa ambayo imepewa adhabu yake kwa yule atakayebainika katika uchaguzi. Suala la rushwa vile vile lina sheria katika ile Mamlaka yetu ya *ZAECA* kwa mfano mtu anayehusika amekamatwa na *ZAECA*, *ZAECA* ina sheria yake sijui hapa Mwanasheria napenda aje atuwekee wazi itakapotokezea hivi kwamba adhabu hii tuliyoiwekwa katika Sheria hii kama itafanya kazi au itaendana kwa mujibu wa Sheria ya *ZAECA*.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, namalizia la mwisho nije katika suala masharti ya fedha, sijaona utaratibu wa matumizi ya fedha za Tume. Ningependekeza lazima hapa pawe na kipengele kinachoonyesha utawala bora katika matumizi ya fedha. Bila ya hivyo fedha hizi ambazo tunawatilia sisi Tume zinaweza zikatumika vibaya.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati kwa kunipa nafasi hii na kuniongezea muda na mimi niwaambie wenzangu wachangie Mswada huu na hatimaye tuupitishe kwa mustakbali mzima wa usalama na maendeleo ya nchi yetu. Naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Rashid Makame Shamsi, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na baada ya hapo atafuata Mhe. Simai Mohamed Said na baadae ajitayarishe Mhe. Mohammedraza Hassanali.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kufika hapa katika Baraza lako Tukufu. Pia nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuchangia Mswada huu muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe. Waziri kwa utendaji wake mzuri kabisa kwa Wizara hii na Naibu Waziri wake na watendaji wake wote. Niipongeze Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kazi yao nzuri na kuweza kutuletea Mswada huu makini na mzuri kabisa. Pia niwapongeze Wajumbe wa Kamati wote kwa kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi yao waliyoifanya nzuri kupitia Mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutoa fursa hii adhimu kwa kuleta Mswada huu wa Kufuta Sheria ya Uchaguzi Nam. 11 ya Mwaka 1984 na kutunga Sheria ya Mwaka 2017. Sheria hii imekuja wakati muafaka, kwani tumeona mapungufu mengi ya Tume katika kuendesha uchaguzi hasa malalamiko yakianza kwa Afisi ya Wilaya ya Uchaguzi badala yake humalizikia Mahakamani au Mahakama Kuu. Utoaji wa matokeo hata adhabu na makosa ya uchaguzi yanaonekana hayapo vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwa Mswada huu mpya tunaamini mambo mengi yatarekebishika kuongeza usimamizi mzuri wenye kuhakikisha kuwa haki, usawa, uwazi unapatikana kuweza kuendesha masuala yote ya uchaguzi hapa Zanzibar. Licha ya Mswada huu kuwa mzuri bado sisi kama Wawakilishi wa wananchi na mimi ni Mwakilishi wa Jimbo la Mtoni tunatakiwa kuboresha ili kutoa demokrasia na usawa wakati wote ili kuuweka Mswada huu uwe mzuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba wakati niliupitia Mswada huu kifungu cha 15(1). Kifungu hiki cha namba 15(1) ya Mswada huo ambacho kinaruhusu uwepo wa Uwakala wa Vyama vya Siasa katika daftari la uandikishaji la wapiga kura.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema kifungu hiki kiondoke kwa sababu uzoefu nilioupata katika chaguzi mbili zilizopita ukitizama kuandikisha hawa wapiga kura wapya wanakuwa vyama vya siasa wanakaa kile chumba ni cha kuandikisha, kile chumba kwanza kinakuwa kidogo Mhe. Naibu Spika halafu unakuwa utashi wa kisiasa akija mtu wa chama fulani labda, yule wa chama fulani anasema huyu kuna ubishani wa fujo fujo mimi naona hiki kifungu hakina umuhimu sana

Mwanasheria Mkuu naomba ukiangalie sana kifungu 15(1) ya Mswada huu hiki kifungu kiondoke.

Lakini Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwa ufahamu wangu kifungu 15(1) kwa Wakala wa Chama cha Siasa wanawakilisha maslahi ya chama chake, huwa kama *agent* au anakuwa huwa *principal* lakini anawakilisha kwa maslahi ya chama chake sio kwa maslahi ya taifa au kwa Wazanzibari wote. Kwa hivyo mimi naona kifungu hiki hasa 15(15) kinakuwa hakina mantiki nzuri na ukitazama tukiwapa hawa Wakala fursa kuingia kwenye undikishaji hata na zile taasisi *NGO's* wanaweza kusema na wao wana haki ya kuingia katika kusimamia uandikishaji wote unaofanyika katika ile chumba cha uchaguzi katika daftari jipya au uandishaji wa zoezi jipya.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme ukiziangali hizi *NGO's* zinapokuwa zinaingia katika hii chaguzi zetu, unakuta *NGO's* fulani inahusika na mambo fulani, tuseme *NGO's* tutowe mfano ya Dini inahusika na mambo ya Dini sana, lakini unakuta wao katika *NGO's* ile kufuatilia lakini unakuta wao ni wafuasi wa chama fulani, sawa wamekuja kwa niaba ya chama. Sasa mimi naona Mheshimiwa hizi *NGO's* tuziangalie vizuri kwa sababu hapa tunakwenda kwenye masuala ya kisiasa zaidi, tuangalie hasa hizi *NGO's* za kidini kuzipa nafasi kuingia. Mimi naona tusichanganyishe Dini na mambo ya siasa. Kwa hiyo mimi naomba tuangalie kifungu hiki ya kuangalia sana Wakala hawa wasiruhusiwe kuingia kifungu hiki namba 15.

Lakini nikija kutizama kifungu namba 7 (1) cha Katiba ya Zanzibar kinaonesha wazi kwamba suala la upigaji kura ni suala kila Mzanzibari ana haki ya Katiba, muhimu awe na *ZID* hii Katiba ya Zanzibar imeshasema na imeshakuwa wazi. Sasa ukitizama kuweka Mawakala kuhakikisha mimi naona pale inakuwa vurugu mechi na inakuwa hekma ya nchi zote, madamu Katiba imeshatoa fursa ya kuhakikisha kila mtu mwenye *ZID* kuandishwa ni mpiga kura halali basi tuende hivyo hivyo. Na ukitizama kifungu 19(1) cha Mswada huu wa sheria tumeweka vizuri kabisa kuna *display* inawekwa pale Mswada huu haukuacha kutoa nafasi ya uwazi kwa kila mdau kuweza kuangalia na kutoa pingamizi kwa wale ambao hawahusiki au hawana sifa za kuandishwa katika daftari la wapiga kura.

Sasa Mhe. Naibu Spika, hii *display* inakaa muda wa siku saba kwa kuhakikisha kwamba wapiga kura wote ni halali ni sawa tunahakikisha na kama sawa wanakuacha na kama kuna malalamiko unapeleka kwenye Tume ya Uchaguzi. Sasa mimi nasema tuwaachie kazi hii Tume tuwape nafasi wafanye kazi kuliko kuwaachia hawa Wakala wa Vyama vya Kisiasa katika sehemu hii ya uandikishaji katika daftari la kudumu la wapiga kura.

Lakini nije kwenye ukurasa wa 87 wa Mswada Kifungu namba 75(1), hapa kinatoa fursa kila chama cha siasa kinaweza kuteuwa kwa kila kituo cha kupigia kura kuhesabu kura, kujumlisha kuweka Wakala wake. Hapa imetoa fursa Mswada huu kuhakiki kabisa kila mgombea atakuwa na fursa ya kuweka Wakala wake kuangalia wale wafuasi wamepiga kura vizuri, wewe ndio msingi kuhakikisha kura inakwenda vizuri.

Kwa hivyo hapa ishaweka kifungu hiki 75(1) kwa kila mgombe atakuwa na Wakala. Mimi nakumbuka kwenye changuzi zangu zote nilikuwa na wakala karibu 160, wakala ninakuwa na fursa ya kuweka siku ile ya upigaji kura wakala atakuwa anashuhudia katika mgombea wa Urais

na katika Ujumbe wa Baraza la Wawakilishi na Diwani. Kwa hivyo kifungu hichi nakipongeza kwa Mswada huu kimeweka vizuri kwa Wakala wa Vyama wataingia siku ya upigaji kura.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu 110(1) malalamiko yanayohoji uhalali wa uchaguzi wa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani yataamuliwa Mahakama Kuu. Mhe. Naibu Spika, hiki kifungu kimewekwa cha Mswada huu. Mimi nasema sawa kimewekwa lakini ukitizama Mheshimiwa mimi mfano wangu mzuri wa uchaguzi wangu wa Jimbo la Bububu nilifanya uchaguzi Tume ya Uchaguzi ikanitangaza nikashinda uchaguzi ule kwa halali na kwa kura zangu halali, lakini wapinzani wakaenda Mahakamani. Matokeo yake tukaenda kwenye kesi karibu miaka miwili kwenye kesi tukapoteza pesa nyingi karibu milioni kadhaa mimi nikapoteza na kule kupoteza. Sasa inakuwa tuwape nguvu na Mswada huu umeweka wazi.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu ukurasa 212 kifungu namba 145 Tume katika kutekeleza majukumu yake ya uchaguzi itakuwa na uwezo wa jukumu ya mamlaka ya kuamua jambo lolote linalohusiana na uchaguzi. Sasa mimi naomba Mhe. Naibu Spika tuwape mamlaka hii Tume ya Uchaguzi iwe na mamlaka ya kuamua kama huyu mgombea kashinda halali na fursa ya kwenda Mahakamani mimi naona isikuwepo kwa sababu unapokwenda Mahakamani ni kupoteza fedha, kupoteza muda tu kwa yule mjumbe au mgombea aliyeshinda na Tume ya Uchaguzi imemtangaza. Kwa hiyo mimi naomba tuwape fursa hawa kwa Mswada huu na Sheria hii hawa ndugu zetu wa Tume ya Uchaguzi kwa kufanya kazi zao kwa uadilifu na bila kuingiliwa na mamlaka yote waweze na kuwa na haki ya kuwamua na kufanya kazi zao vizuri bila kuyumbishwa yumbishwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nije kwenye ukurasa 185 ya Mswada huu kifungu namba 69(h) "Matokeo ya kupiga kura yatabandikwa au kuwekwa nje ya kituo cha kupiga kura baada ya kuhesabiwa". Mheshimiwa mimi naona mimi kifungu hiki tuanza wenyewe kuweka mashaka kwa sababu tumeona uchaguzi uliopita mwaka jana wa 2015 matokeo yakishapandikiwa ukutani pale yakishabandikwa matokeo ya Urais, matokeo ya mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani mtu anachukuwa anapiga picha matokeo yake, akishapiga picha anakwenda anaweza kujumlisha kituo hichi, kituo hichi halafu kuna kutizama hii mitandao hii ya kijamii Mhe. Naibu Spika iko mingi.

Kuna dada mmoja yuko Marekani kule Washington anarusha matokeo mengi ukiangalia mitandao mengi kwenye *instagram*, kwenye *facebook* matokeo mengi yanayofanyika hapa yeye anajua vipi hata hujui kule siri kazipataje. Sasa utakuja uchaguzi huu ushaweka *display* pale tunashajua kura amepata Mhe. Rais ngapi, Mhe. Mwakilishi ngapi, Mhe. Diwani ngapi, mtu anachukuwa anaanza kujumulisha mwenyewe halafu anapeleka nje akipeleka nje kule yule anajumlisha anarusha matokeo tayari huyu kapata kura hizi.

Sasa hii naona *display* hii tunaweka hapa tunanza kujizonga wenyewe. Mimi ningeomba hii *display* kwa nini isiondoshwe wakapewa Tume ya Uchaguzi mamlaka moja kwa moja ikishahesabiwa kura ipelekwe Tume ya Uchaguzi utangaziwe kihalali kwenye vyombo vya habari. Sasa kuweka *display* pale wazi na mtu mwengine anaweza kuja kuchukuwa *display* ile akaibadilisha kwa peni zake au kwa kompyuta akaweka matokeo mengine. Kwa hiyo mimi tunaanza mambo wenyewe kutoa fursa na kutowa mwanya kwa watu ambao hawana nia njema ya nchi hii kwa kutuchafulia uchaguzi wetu.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa Mswada huu ukurusa 160 katika Sura ya Kwanza masharti ya utangulizi. Mheshimiwa maeneo yote yaliyoruhusiwa na mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa madhumuni ya kubandika mabango ya kampeni ambayo hayataruhusiwa maeneo ya hospitali, skuli na majengo ya ibada. Mheshimiwa mimi sina tatizo suala la kubandika hizi kufanya kampeni maeneo ya hospitali, skuli na majengo ya ibada, hili jambo ni muhimu lakini hili eneo la masoko mheshimiwa tuliangalie vizuri hili la masoko, eneo la masoko ni eneo *public area*, mgombea yoyote anayetaka kufanya kampeni zake kwenye eneo la watu au kwenye eneo la masoko au maeneo ya mkusanyiko wa watu kwa sababu kubandika zile *posters* zake au kufanya matangazo yote.

Ukiangalia masoko mheshimia hii Sheria itakuja kutubana mwisho wa siku na sisi pia wadau wa kugombea kwenye uchaguzi huu ukitazama, ukiandika masoko unaweza kusema masoko kama marikiti pale, lakini masoko haya ukiyageuza ukitizama maduka yote ukuanzia pale Darajani mpaka mwisho yale yote masoko ukienda maeneo mengine yote ni masoko. Sasa unakuta ukifanya kampeni lazima upate sehemu zenye watu na sehemu ambazo watu wanajua ujumbe utawafika. Sasa mimi naomba sana hii sehemu ya Hospitali, Skuli, majengo ya ibada hayana tatizo uko isifanye kampeni, lakini eneo la masoko liangaliwe mheshimiwa vizuri kwa sababu sote ni wadau tunahitaji kufanya kampeni. Kwa hiyo, tuangalie hili eneo la masoko kama litakuwa lina umuhimu wake basi tuliwachie tuweze kufanya kampeni eneo ya masoko.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye ukurasa wa 208 kifungu namba 127 (1) "Ni marufuku kwa mgombe wa chama cha siasa au taasisi au mtu mwengine yoyote kutangaza matokeo ya uchaguzi kwa njia yoyote ya mawasiliano kabla ya kutangazwa rasmi na Tume ya Uchaguzi". Mheshimiwa hii nimesema kifungu hiki kizuri lakini kinaanzwa na kule kwenye kubandika yale matokeo ukutani, mtu akisha kuchukuwa yale matokeo akiyajumlisha huwezi kumkamata na hapa tumeona adhabu imewekwa.

Kama kifungu hiki (a) 'ikiwa mgombea atatumikia kifungo cha miaka mitano (5) kama katangaza ikiwa chama cha siasa au taasisi adhabu yake milioni mia (100,000,000) ikiwa mtu mwengine atatumikia kifungo cha miaka...', Lakini mimi nasema Mheshimiwa hizi adhabu ni nzuri lakini huyu mtu atakayetengaza tutamuona wapi na tutamkamata wapi kwa sababu ukiangalia mitandao unakuwa mwengine huwezi kumjua unaona hizi taarifa zinakuja lakini zinatoka nje. Sasa kumkamata mtu nje inakuwa si rahisi kwa mfumo tuliokuwa nao siye sasa hivi kumfatilia hizi taarifa atakazozitoa yeye. Kwa hiyo mimi naomba sana tuangalie haya kuweka matokeo katika kubandika hii *display* yetu.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika moja.

Mhe. Ibrahim Hussein Makungu: Haya ahsanate namalizia mwisho katika ukurasa wa 183 wa Mswada huu wetu kifungu namba 64(4) Chama cha siasa au mgombea atabandika vifaa vya kampeni katika maeneo yanayoruhusiwa baada ya kupata idhini ya mmiliki. Mhe. Naibu Spika, mimi nakata nipongeze huu Mswada wetu na siye tumeupitisha na nawaomba wajumbe muupitishe huu Mswada mzuri. Kwa sababu nimeangalia hili suala hili kwa sababu mtu anaweza akalala asubuhi nyumbani kwake nje kote kumebandikwa picha chama fulani, wakati yeye si

mfuasi wa chama kile. Kwa hivyo inakuwa shida sasa kutaka kuzibandua au kuona mimi nitajulikana kama mimi chama hiki.

Kwa hivyo mimi nimefurahi sana kuwekwa kipengele hiki cha sheria mtu lazima umuombe akubali na umbandikie zile *posters* zako, kama yeye chama fulani anakipenda basi ataweka *posters* za chama fulani tu kwa sababu anajua kama hawa ni wenzangu na mtu kama hapendi usimbandikie *posters* zile. Kwa hiyo mimi naomba hii sheria nzuri na tumeingalia kwa umakini mkubwa na inaleta changamoto kubwa chaguzi zilizopita kutokana na hali ilivyokuwa inakwenda kupandika zile *posters* ovyo ovyo tuu mtu abajibandikia kwa sababu ya kufuata...

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, mimi nasema naunga mkono asilimia mia kwa mia kwa Mswada huu ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Hussein Ibrahim Makungu sasa hivi atafuta Mhe. Simai na baada ya hapo atakuja Mhe. Mohammedraza ajitayarishe Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu leo kuweza kufika hapa sote tukiwa wazima na afya lakini pia nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika kwa jinsi unavyoendesha Baraza letu kwa umahiri wako na umakini wako na pia kutuongoza.

Lakini pia nichukuwe nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu ambao nawakilisha hapa leo, nimefurahi sana leo kumuona kaka yangu, jirani yangu Mhe. Mohammedraza amefika leo Barazani, yeye ni jirani yangu kule Wilaya ya Kati. Jimbo la Tunguu linapakana na Jimbo la Uzini pamoja na Chwaka, kwa hivyo naamini sasa tutakuwa na sisi naye kwa pamoja baada ya kurudi katika matibabu yake kwa hiyo nimefurahi sana.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, niendelee kuwapa pole wapiganaji wetu pamoja na familia katika kipindi hiki kigumu ambapo msiba mkubwa umetupata taifa letu na Inshallah Mwenyezi Mungu atawapa subra na wazidi kuwa na nguvu ya ustahamilivu katika kipindi hiki kigumu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nataka nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hasa kwa Mswada huu leo kufika hapa Barazani. Hili kwanza linaonyesha umahairi wake na jinsi anavyojali utawala bora. Mhe. Naibu Spika, kuna msemo wazungu wanatumia wanasema kwamba "*Democracy is a very expensive tool"* kwamba demokrasia ina gharama zake lakini lazima tuifaye. Kwa hiyo leo sisi humu ndani tunapitisha sheria hii na kutowa mapendekezo yetu ili kuhakikisha kwamba Wazanzibari wote wataweza kushiriki na kuyafanya yale kila miaka mitano hasa katika Mswada huu wa Sheria kufuta Sheria ya Uchaguzi nambari moja ya mwaka 1984 na kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na masuala mengineyo. Lakini Mswada huu nimeupenda sana kwa sababu unakuja kuboresha mengi ambayo mapungufu yake tuliyaona huko nyuma, nataka niseme moja ambalo nataka nisisitize.

Mhe. Naibu Spika, ukienda katika Katiba yetu kwenye kifungu cha namba 120 (4) kinazungumzia masuala la mipaka, hili ni kweli tukiangalia kile kifungu kinasema kwamba Tume itakuwa na mamlaka au madaraka ya kuweza kupanga au kukata mipaka ya majimbo kwa kuangalia sensa kila baada ya muda wa miaka minane.

Mhe. Naibu Spika, nataka nitowe historia kidogo moja hapa ya chaguzi zetu ambazo tumefanya Zanzibar miaka ya nyuma.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 1963 kabla ya mapinduzi palifanyika uchaguzi Zanzibar. Chama cha ASP kilipata majimbo kumi na tatu (13) ambapo ushindi wake ulikuwa sawa sawa na asilimia 54.2, Chama cha ZNP na ZPP walipata majimbo yaliobakia lakini majimbo ya Zanzibar mwaka 1963 yalikuwa majimbo 31, hiyo ni 1963, ukichukuwa *population* ya Zanzibar ambayo wakati huo lablda ilikuwa laki 250,000 na ushee mpaka kwenda laki 300,000.

Hasa kama utachukuwa *issue* ya idadi ya watu kuwa ni hoja ni juu ya ukataji wa mipaka na majimbo basi leo kutakuwa na majimbo Zanzibar *at least* 170 kwa sababu kama kwa kila watu laki 250,000 uwepe majimbo 31 ukiangalia historia, kwa hiyo unachukua laki 250,000 maana leo sisi tuko watu milioni1,400,000. Kwa hiyo Tume kwenye *issue* ya mipaka iendelee kufanya kazi kila inapohitaji ikiwa ni miaka mitano, miaka kumi wawe huru, hivi ni visiwa watu wanazunguka, wanahamia na mambo yanabadilika. Leo ukienda Fuoni siyo Fuoni ya miaka mitano ilopita, leo ukienda Tunguu mji mpya au Jumbi mji mpya, sio ile Tunguu na Jumbi ile ya zamani inayojulikana. Leo ukienda Mtoni sio ile Mtoni kama ile ya zamani inayotambulika, leo ukienda kwa Mhe. Rashid kule Magomeni basi siyo Magomeni ya zamani. Leo ukitoka Mwanakwerekwe unakanya gari pembeni nyumba kulia nyumba mpaka unafika zako kwenye Tunguu *junction* ni nyumba kote zinajengwa, kwa hiyo suala la mipaka Tume iwe huru na iendelee kufanya kazi yake.

La pili nataka nizunguzie kifungu namba 100 ambacho kinazungumza suala la waangalizi. Mhe. Naibu Spika, kifungu namba 100 ni kizuri na ni kizuri kwa sababu gani, ukiangalia katika miaka ya nyuma unamkuta muangalizi anatoa matokeo ya uchaguzi ya Kaskazini Unguja lakini yeye yuko Mjini anakula starehe. Hili nimeliona nimelithibitisha maana wengine humu tunakulia maeneo tofauti. Sasa hawa waangalizi wanapokuja haya masharti yaliyowekwa mara hii ni mazuri sana kwa sababu hichi ndicho kinachohitajika, mtu kama hana uzoefu inakuwaje anakwenda kufanya kazi ambayo haijui.

Mhe. Naibu Spika, tumeona mara hii kila mtu unamkuta mtu sijawahi kumuona hata kampeni hata kushiriki katika chama cha siasa chochote au kuandika jambo lolote ana pasi anajiita yeye muangalizi wa ndani, hasa hawa watu wanatokea wapi, nani anawapa hizi nafasi. Sasa kwa kweli masharti ambayo yamewekwa mara hii kila taasisi ya ndani iliyosajiliwa kabla ya kupatiwa kibali ya waangalizi itawasilisha katika Tume, Katiba ya taasisi, cheti ya usajili, muundo wa uongozi unaotambulika, uzoefu wake. Hili ni jambo zuri sana kwa sababu sio kila mmoja anakuja hapa akasema anahitajia neema kwetu sisi au anatuombea sisi mema kwa Wazanzibari, wengine wanakuja hapa kutuharibu, wanakuja hapa sisi kutuharibia maisha yetu kwa faida zao wenyewe kwa yake mambo wanayoyataka wao. Kwa hiyo suala la uangalizi wanapokuja hapa tuwe makini sana na Tume iendelee kulikamata upande huu katika kutowa elimu suala hili zima la waangalizi ili watu wapate kujua.

Lakini pia katika kifungu cha 127 Mhe. Naibu Spika, hiki kifungu kimezungumziwa sana na hiki kifungu kina historia yake tangu chaguzi za vyama vingi vimeanza hapa Zanzibar. Moja katika katika kifungu namba 127 namba 1 unaposema kutangaza matokeo ya uchaguzi kwa njia yoyote

ya mawasiliano. Mimi nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu kama itampendeza basi neno la mawasiliano liwekwe katika utangulizi tafsiri yake ifahamike vizuri.

Lakini katika hiki kifungu namba 1(2) kinasema kama mgombea chama cha siasa, taasisi ya mtu mwengine yeyote atayetangaza matokeo. Mimi nashauri kiongezwe kifungu namba 3 hapo ili kama Tume au mtu yeyote awe na nafasi ya kutoa taarifa kituo cha Polisi, kwa sababu haya mambo ya kutangaza kuna njia nyingi sasa hivi na lazima fursa iwepo kwa Tume au mtu ili aweze kupeleka taarifa kituo cha Polisi pale ambapo mtu amefanya kosa la kutangaza matokeo ya aina yoyote wakati huku tumeshakubaliana kisheria kwamba Tume ndio yenye mamlaka ya kutangaza matokeo.

Mhe. Naibu Spika, pia kifungu cha 143 ni kizuri ukiangalia uwezo wa mamlaka kwa jumla ya Tume, inaposema kwamba Tume katika kutekeleza majukumu yake ya uchaguzi itakuwa na uwezo, jukumu na mamlaka ya kuamua jambo lolote linalohusiana na uchaguzi ambalo halikuwekewa masharti yake ndani ya sheria hii au sheria nyengine yoyote inayohusiana na uchaguzi.

Mhe. Naibu Spika, hiki ndicho kifungu ambacho katika hii Sheria inaweka uwazi kuwapa Tume nguvu. Mimi niwapongeze sana wanasheria katika miaka yote tangu nilipoanza mimi ndani ya Baraza hili la Wawakilishi, basi Sheria hichi ndicho ninaweza nikasema nikaisifia sana sheria kwa umakini umepitiwa na watu mpaka ile lugha yake ilivyoandikwa. Kwa hiyo, nawapongeza sana.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukiangalia katika vifungu vyengine, kifungu Nam. 24(2) kinapozungumza masuala ya endapo Afisa Uandikishaji ataridhika na maombi hasa ya mtu anapopoteza kitambulisho chake au kuharibika. Sasa Mhe. Naibu Spika, unaposema mtu kwenda kulipia ada, ada inaweza ikapangwa mtu yeyote wakati kupiga kura ni haki ya kila mmoja. Sasa hii ada iangaliwe vizuri sana kwani kuna wanyonge huko, sio unaambiwa kupata kitambulisho kipya mtu akalipe shilingi 20,000 au 15,000 iwe ada ya wastani ambayo kila Mzanzibari ataweza kuhimili na kwenda kuilipia.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia ukiangalia kifungu cha 44(d). Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 44 ukiangalia kinajirudia…

Mhe. Naibu Spika, samahani sio kifungu cha 44 ni kifungu cha 31. Kwenye kifungu hiki cha 31 kinasema kwamba juu ya suala zima la kumuondoa mpiga kura asiyekuwa na sifa. Ukiangalia 31(2) (a) inasema taasisi inayohusika na masuala ya vizazi na vifo halafu ukienda kwenye hiyo 31(d) inasema taasisi inayohusika na usajili wa wakaazi na vitambulisho. Sasa hivi hizi taasisi zote tumeshaziunganisha. Kwa hiyo hapa kidogo Mwanasheria Mkuu ajaribu kuweka mambo sawa ili hizi mbili iweze kuonekana kama ni moja kwa sababu tayari sasa hivi hii inakuja kuwa Wakala. Kwa hiyo, hawa wawili sasa wameshakuwa ndugu mmoja inafaa hapa wakatambulika kama ni mmoja katika kifungu hiki.

Mhe. Naibu Spika, nizungumze suala la wakati wa uchaguzi mambo ambayo yanafanyika mengi, ni suala zima la *access* ya watu ambao wenye ulemavu na watu wazima ili waweze kufika katika vituo vya kupiga kura.

Mhe. Naibu Spika, utaona wakati mwengine katika majimbo yetu au maeneo tofauti watu wanapata tabu sana. Wazee wanafika pale pale mstari unakuta yule mtu ambaye anamleta mzazi wake au mlemavu ili aweze kupiga kura. Sasa wakati mwengine wananchi wanakuwa hawapendi kumuona yule ambaye aliyemleta anapewa nafasi pia ya kupiga kura. Mimi nashauri Tume iendelee kutoa elimu ihakikishe watu wa aina hiyo wanawajua pia kabla ili ile huduma ambayo wanakuja kutimiza ya kupiga kura waweze kutimiza jinsi ambavyo ilivyopangwa na kwa urahisi bila ya tabu yoyote.

Mhe. Naibu Spika, lakini jambo jengine ambalo Mhe. Hussein Ibrahim Makungu amelizungumza limenifurahisha sana ni suala la picha ambazo zinabandikwa. Kwa kweli watu wengine wanapata tabu sana maeneo tofauti kubandikiwa mapicha ambayo wao wenyewe hawataki. Kuna watu wanaumwa na wanavipenda sana vyama vyao vya siasa. Sasa pale unapokwenda kumbandikia mtu kwa kweli Tume iliangalie hili kwa undani kwa sababu wakati mwengine mtu anaweza kutoka ndani kwa hasira akaenda akachana ile picha akaambiwa amefanya kosa, lakini mtu aliyekuja kubandika hajamuomba. Sasa hili liangaliwe kwa undani pia.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala baada ya mtu ameshatimiza haki yake ya kupiga kura katika kituo kubakia mitaani. Hili utalikuta wakati mwengine mtu mmoja anarudi kupiga kura anaishia barazani, baada ya muda panageuka kikundi zogo linaanza, mambo yanaanza kuzungumzwa yule atashinda, yule hivi mambo yanabadilika. Tume izidi kutoa elimu kwamba pale kwa sababu siku ya uchaguzi ni siku moja tu basi, ni kwenda kupiga kura baada ya hapo kurudi nyumbani kwako kula chakula chako cha mchana, cha jioni usubiri matokeo, kwa sababu maeneo yote yanakuwa yamefungwa…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika mbili.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, itatosha hiyo na inapendeza pia.

Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo mtu akishamaliza kupiga kura Tume iendelee kutoa elimu kwamba watu wote wanatakiwa warudi majumbani mwao, wapumzike na wasubiri matokeo. Lakini tabia ya kukaa vikundi kukaa kuzungumza vijana wadogo wadogo wanaingia barazani. Kwa hiyo familia, wazee na niliwahi kuzungumza hapa wakati nachangia katika Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto nikasema suala la *parental guidance* wazazi wachukue wajibu wao katika malezi hasa vijana ambao wamo katika umri wa miaka 15 mpaka kwendea juu kutoka nje nje katika nyakati ambazo hazistahiki.

Kwa hiyo, suala la elimu Tume walete bajeti yao katika suala la elimu waweze kutoa elimu ya kutosha ili wananchi wafahamu haki zao na yapi ambayo wanatakiwa wafanye na yapi ambayo hawatakiwi kufanya.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru sana nimefurahi sana Mswada huu kufika leo hapa, naunga mkono hoja mia juu ya mia kwa niaba ya wananchi wangu

wa Jimbo la Tunguu nawashukuru pia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hili kwa kunisikiliza. Nasema ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mohammedraza baadae atafuata Mhe. Asha Abdalla Mussa na ajitayarishe Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kutupa pumzi na kuhudhuria katika Baraza lako hili tukufu. Lakini nichukue nafasi hii kwa kuwa Mheshimiwa bado sina nguvu ya kuzungumza sana kutokana na afya, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu Alhamdulillah hali yangu inaendelea kuwa ni nzuri.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kwa sababu nilikuwa safarini nimerejea jana, nitoe pongezi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini na kwa niaba yangu na familia yangu kuwapongeza watoto wetu kwa kazi nzuri walioifanya timu yetu ya taifa ya Zanzibar. Mwenyezi Mungu atujaalie kwa sababu timu ya taifa haina wanachama, basi Mwenyezi Mungu *inshaallah* kwa uwezo wake tuombe dua sote ili tuwe na historia ya kupata kikombe hicho na naamini uwezo huo tunao na nia tunayo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, vile vile nichukue nafasi hii kuishukuru hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndugu yangu Mhe. Mohammed Aboud Mohammed pamoja na Kamati nzima ya Katiba na Sheria iliyosomwa kwa niaba ya Kamati na Mhe. Amina Iddi Mabrouk, nitoe pongezi maalum kwa kamati zote.

Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kushukuru Kamati zote hizo pamoja na wizara zilizokaa pamoja kama Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Wanasheria wa ndani ya Baraza la Wawakilishi, Wanasheria wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa uzuri na iliyojaa haiba. Mheshimiwa Mswada huu ulioletwa na mimi nasema naipongeza na naiunga mkono kwa asilimia mia, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa nimeunga mkono naomba nitoe maoni tu kama ni taarifa kwa Tume ya Uchaguzi kusaidia mawazo yangu. Mhe. Naibu Spika, tumeshuhudia miaka nenda miaka rudi wakati wa kampeni tunakuwa na mikutano mikubwa na vyama vinafahamika, lakini kufanya kosa si kosa, kurejea kosa ni kosa, lakini kwa usemi mwengine wanasema "*you learn on mistake to repeat the mistake is the mistake*.

Mhe. Naibu Spika, niiombe Tume pamoja na Kamati zake wakati wa uchaguzi wa kampeni, ningeliomba kutoa tahadhari na mawazo kwamba tunapofanya mikutano ya kampeni ningeomba Tume itizame ushabiki kwa sababu tumeshuhudia vyama vingi, kwa mfano chama kimoja kinafanya mkutano Makunduchi, chama cha pili kinafanya mkutano Nungwi. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika yule wa Makunduchi inabidi aende Nungwi na yule wa Nungwi inabidi aende Makunduchi.

Mhe. Naibu Spika, kwa tumeshuhudia vijana wetu mara nyingi roho zao zilipotea Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema, kunatokea na ajali. Vile vile Mhe. Naibu Spika, kutokana na ushabiki wanachama hawa wanaporejea majumbani yule wa Makunduchi anarudia Nungwi na

yule wa Nungwi anarejea Makunduchi basi hapa kati kati usalama wetu na amani yetu kwa wananchi wetu, kwa vyama vyetu inakuwa ni vigumu sana. Kwa hivyo, naomba kutoa rai kwa Tume ya Uchaguzi wanapotoa ratiba wahakikishe kwamba chama chochote kile kitakachofanya mkutano wawe na mwelekeo wa kufanya kwamba chama kimoja siku ile iwe inafanya mkutano wake.

Mhe. Naibu Spika, *otherwise* tutakuwa tunarejea katika hali ambayo sisi Wazanzibari hatupendi kwa sababu ushabiki ni ushabiki, kuna wengine ni wachochezi, kuna wengine wanatafuta hali ya amani ipotee. Sasa si kila anayepepesuka ni mlevi. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hili linaweza kuhatarisha amani katika hali hii ya makutano. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ningeliiomba Tume ya Uchaguzi wakalitizama kwa ufasaha jambo hili ambalo ni kubwa na gharama zake haziwezi kulipika kwa wananchi wetu wakati wanapopatwa na maafa makubwa sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, vile vile niiombe Tume ya Uchaguzi kupitia vyombo vya usalama kama polisi na *traffic*. Mhe. Naibu Spika, mara nyingi magari yetu yanapokwenda kwenye mikutano utakuta gari la aina ya Fuso linajaza watu wengine wanakaliana juu. Sasa Mhe. Naibu Spika, hakuna kitu usalama, hakuna kitu afya. Mhe. Naibu Spika, dereva anapokuja kupiga breki au panapotokea ajali wale wa juu inabidi wayayuke. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, sote ni watu wa kitu moja lakini kupoteza roho na ushabiki, ningeliiomba Tume ya Uchaguzi kwa kushirikiana na askari iwe imetoa tamko rasmi idadi inayofahamika, *otherwise* Mhe. Naibu Spika katika hali hii watu watakuwa wanaumizana, watu watakuwa hawalali magari yanajaza yanavyojaza, watu wengine wanakaa juu ya magari.

Mimi ningeliomba Tume ya Uchaguzi itoe tamko kwamba lazima haya tunayojadiliana humu ndani katika kufanikisha jambo hili, basi lazima tuwe wa kweli, tusipokuwa wa kweli hili jambo haliwezi kufanikiwa. Kwa hivyo, Tume ya Uchaguzi ina mamlaka ikishirikiana na jeshi itizame siku hizo za mikutano na magari ambayo yanapakia abiria. Wengine wanakwenda kama wanakwenda *pic nic*, kwa hivyo wanajaza abiria kwenye gari ya Fuso moja kuna abiria mia mbili, pengine Fuso linachukua abiria hamsini na wengine wanakaa juu. Kwa hivyo, usalama ni jambo muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa na hayo tu ya kuyaeleza na kuiunga mkono Sheria hii iliyoletwa mbele ya Baraza la Wawakilishi, nasema ahsanteni sana. Nashukuru na naunga mkono kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mohammedraza mchangiaji anayefuata ni Mhe. Asha Abdalla Mussa ajitayarishe Mhe. Suleiman Sarahan Said na baadae atafuta Mhe. Said Soud Said.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili kuweza kuchangia Mswada huu ambao upo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, niungane na Wajumbe wenzangu kwa kuunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja. Mhe. Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana kaka yangu Mhe. Rashid Makame Shamsi kwa kuvielezea vifungu na kutoa ufafanuzi kwa kuuchangia mswada huu kifungu kwa kifungu, kwani Mhe. Rashid yeye kwa kweli ndani ya Baraza hili ndiye anayeweza kutufumbua macho Wajumbe wengine na kuweza na sisi kutoa maoni yetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze na kuipongeza Tume pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuandaa mswada huu na kuuleta hapa Barazani ili na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuweza kuupitisha lakini pia na baadae kuufanyia kazi katika chaguzi zijazo.

Mhe. Naibu Spika, nitaanza kupongeza katika kifungu cha 14(1) katika ukurasa wa 106, kuna kifungu ambacho kinazungumzia Sheha kuwa wakala kwa nafasi yake. Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wengi wamezungumzia kuhusiana na suala la Sheha kuwa wakala. Mhe. Naibu Spika, sote ni mashahidi kwamba tumeona uchaguzi wa mwaka 2015 kulikuwa na changamoto ya kutowatambua wapiga kura ambao wapo katika vituo hivyo. Kuna baadhi ya maeneo kulikuwa na changamoto kubwa na yote haya ni sababu kwamba Sheha hakuwepo katika kituo cha kupigia kura au kituo cha uandikishaji. Mimi niipongeze sana Tume kwa kuona kwamba Sheha ana umuhimu wake katika masuala mazima ya kuwatambua wananchi wake, lakini pia yeye ndiye atakayeongoza wasimamizi wa uchaguzi au wasimamizi wa uandikishaji.

Mhe. Naibu Spika, pia nikija kwenye ukurasa wa 174 kifungu cha 39 ambacho kinazungumzia ubandikaji wa daftari katika eneo la kupigia kura. Mhe. Naibu Spika, hapa pia niwapongeze Tume kwa kukiona kifungu hiki na kukiweka ili kuweza kuondosha matatizo ambayo yanayojitokeza.

Mhe. Naibu Spika, baada ya wananchi kujiandikisha na kuingizwa katika daftari kumetokea changamoto nyingi ambazo zinapelekea uvunjifu wa amani katika maeneo yetu. Changamoto hizo ni kwamba wanapobandika daftari kunatokea watu ambao wasiopenda amani katika nchi yetu wanakwenda kulichana lile daftari na kufanya kwamba wananchi wetu ambao waliojiorodhesha pale wasiweze kutambua orodha zao. Lakini pia kuna changamoto nyengine kwamba mtu amejiorodhesha katika kituo cha Shehia labda ya Kinyasini, lakini utakuta jina lake lipo katika Shehia ya Matemwe.

Mhe. Naibu Spika, nawaomba sana Tume ya Uchaguzi wakati wanapowaingiza watu katika daftari hili la kudumu la wapiga kura, basi wawe makini katika kuweka orodha kamili ya wapiga kura ambao wamejiandikisha katika Shehia husika. Tatizo hili linafikia mpaka wakati wa uchaguzi mkuu mtu amefika pale kwenye kituo anakuta jina lake halipo, inafika pahala anashindwa kupata haki yake kumbe jina lile lipo katika kituo chengine.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika ukurasa wa 184 naunga mkono kifungu cha 67 kinachozungumzia vituo vya kupigia kura. Mhe. Naibu Spika, tunashuhudia kwamba katika ukataji wa majimbo kuna baadhi ya maeneo wananchi wetu wamekuwa wanapata tabu sana katika sehemu ambayo wamepangiwa kwenda kupiga kura. Naiomba sana Tume wakati unapofika wa uchaguzi basi iangalie maeneo yale hatarishi ambayo wananchi wetu wanaweza kupata vikwazo.

Mhe. Naibu Spika, pia nije kwenye ukurasa wa 191 kifungu cha 82(2) kinachozungumzia kura ya mapema. Mhe. Naibu Spika, Tume imeweka utaratibu utakaoruhusu upigaji wa kura wa mapema ambao utafanyika siku moja kabla ya siku ya upigaji kura au siku nyengine yoyote kama itakayoamuliwa na Tume.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwapongeze sana Tume kwa kuona kwamba kuna watu wengi, wapiga kura wananyimwa haki yao kwa kutofika katika kituo ambacho wamejiandikisha na kupiga kura. Hiyo inasababishwa kwamba kunakuwa na ongezeko kubwa la watu ambao wamejiorodhesha kwenye daftari lakini kura nyingi zinakuwa hazijapigwa. Yaani nawapongeza sana, naamini kwamba itakapopitishwa Sheria hii wataandaa utaratibu mzuri ambao wataweza watu hawa kupiga kura bila ya matatizo yoyote.

Pia Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa wa 204 kifungu cha 120000 kinachosema kwamba:-

"Makosa yanayohusiana na kampeni.

Mtu yeyote kuhusiana na kampeni za uchaguzi:

(f) ataendesha kampeni za uchaguzi katika sehemu isiyoruhusiwa kama vile maeneo ya Jeshi, Vituo vya Polisi, Taasisi za Umma na maeneo ya kazi wakati wa saa za kazi kwa taasisi za elimu wakati wa vipindi vya masomo".

Mhe. Naibu Spika, mimi naipongeza sana Tume kwa kuona kifungu hiki au kwa kuweka kifungu hiki ambapo kuna baadhi ya watu ambao wanafanya kazi katika taasisi baadhi yao wanaendesha kampeni katika taasisi zao. Mhe. Naibu Spika, sote ni mashahidi na tunapata malalamiko yanayohusiana na kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi katika taasisi nyengine wanaendesha kampeni katika maeneo ambayo ya kazi.

Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache nisema niungane na Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa maoni yao ambayo wametuletea. Lakini pia niungane na Wajumbe wenzangu waliotangulia mwanzo kuzungumza.

Naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Asha Abdalla Mussa anayefuata ni Mhe. Suleiman Sarahan Said, ajitayarishe Mhe. Said Soud Said (MBM) na nina hakika muda unaweza ukatosha basi ajiandae na Mhe. Suleiman Makame.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa ili kuchangia Mswada huu ambao kwa kweli utaleta zaidi ufafanuzi wa usahihi wa upigaji kura katika siku za mbele.

Mhe. Naibu Spika, mimi awali ya yote kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika jitihada zake za kuleta maendeleo na usawa katika jamii, ili kila mmoja apate haki yake ya kimsingi. Lakini pia nizungumzie kwamba hata kule Tanzania Bara Mheshimiwa wenzetu wengi wenyeviti na viongozi wa vyama vya upinzani ambao wameona umuhimu wa Chama cha Mapinduzi kwamba wameanza kurudi kwenye chama chao. Pia na hapa ningeomba wale wote wanaoona umuhimu wa kurudi warudi kwenye Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nashukuru na mimi nachangia katika ukurasa wa 208 kifungu cha 127 ili tuone umuhimu wake, kwa sababu kwa kweli kuna vitu ambavyo vinachangia uhalisia wa kuleta matatizo kwa udogo wake, lakini baadae vinakuja katika mazingira mazito. Nikichukulia katika kifungu cha 127 pia nimeona katika kifungu cha (b) ikiwa chama cha siasa au taasisi adhabu isiyopungua shilingi milioni moja ambayo itatangaza hizi habari zilizokuwa si za kweli. Lakini katika jumla ya vifungu nimeona hapa kwamba ni taasisi lakini katika chombo ambacho kinaleta madhara makubwa ni vyombo vya habari. Mimi ningeona kwamba hiki chombo cha habari kwa nafasi yake ukiachia taasisi baada ya (c) ingetiwa (d) ikawa vyombo vya habari. Kwa sababu hizi taasisi ni taasisi lakini vyombo vya habari ni katika moja ambayo ni taasisi kubwa inayoleta changamoto sana katika habari hizi.

Pia nizungumzie kwamba katika mazingira mengine hili tatizo limeshakuwa sugu la utangazaji au kutoa matokeo. Sasa ningeomba sana kama walivyosema wenzangu adhabu hizi ndogo ndogo za shilingi laki mbili kwa kuharibu uchaguzi ni ndogo. Kwa hivyo, ningeomba Waziri kidogo atizame umuhimu wa hili neno na pia aangalie shilingi laki mbili ni pesa za nini kwa muda huu. Kwa hivyo, ningeomba hii adhabu nyengine ikaweza kubadilishwa.

Sasa niende katika kifungu cha 128 atakuwa mtu amefanya kosa akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na shilingi milioni tano kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi mwaka mmoja au kifungo, au adhabu zote faini na kifungo.

Mhe. Naibu Spika, bado nazungumzia katika suala zima hili la uchaguzi, mvurugano unaojitokeza kwa makusudi maana yake sio kwamba hatujafikia elimu ya kuelewa, tunajua suala la kutangaza ni suala zito na linaleta mtafaruku mkubwa sana. Lakini kwa utashi na kwa kuangalia kwamba tunafanya kwa makusudi kwa sababu sote wenyewe kwa wenyewe na hakuna mtu anayechukuliwa hatua, bado adhabu za kisheria zingeongezwa ili kutoa mfano kwa watu wengine na jambo hili likawa mwisho wa ukomo wake.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumzie baadhi ya maeneo ambayo mambo mengine yanaleta ushirikishaji mkubwa ili mambo mengine yasiweze kujitokeza. Mheshimiwa tuna kauli tunaambiwa ukishakupiga kura unatakiwa uende nyumbani ukasubiri matokeo yatakavyotokea, lakini tuna kauli nyengine ya Sheria ya kukaa mita 200. Mheshimiwa hizi mita 200 sijui zinapimika vipi, maana yake mita 200 zinakuwa chini ya mlango wa geti ambao mtu anakwenda kupiga kura. Sasa sijui mita 200 baada ya kituo au eneo la kupigia kura. Matokeo yake anakwamba tizama kituo kiliko, yeye anakaa kwenye geti mtu yule hapiti kwenda kupiga kura na hapa ndio panaanza usumbufu na sheria inakwambia mita 200. Ningeomba hapa mita 200 zikafafanuliwa, mita 200 katika eneo, mita 200 kutoka kwenye kituo. Mimi siioni faida yake zaidi kwa sababu tumeambiwa baada ya kupiga kura rudi nyumbani, tukiweka Sheria mita 200 kukusanyika basi itakuwa tumempa uhuru wake mwenyewe na hatuwezi kumlalamikia.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye jambo jengine ambapo mambo mengine yanatuletea usumbufu wakati wa kupiga kura. Mheshimiwa hawa ma-*observes* ambao wanatoka nchi za nje wakija hapa wao sio kama wanakuja kuangalia uchaguzi wanakuja kusimamia uchaguzi. Hili suala linatupa matatizo sana. Ningeomba wizara ikaweza kuweka Sheria ya mtu yeyote ambaye anataka kuja kuangalia uchaguzi kwanza akahakikisha anawasili katika ofisi ambayo ni

muhusika, lakini pia akapewa masharti kwamba asiwe msimamizi yeye awe muangalizi. Mara nyingi wanakosa kufahamu ufahamu wao, sijui kwa lugha zao za Kingereza au wanafanya makusudi. Mara nyengine wanataka wao watusimamie uchaguzi. Kwa hivyo, ningeomba suala hili Mheshimiwa likaangaliwa kwa hali nzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, mambo mengi yanaleta utata kwetu sisi wakati wa uchaguzi, hivyo tunatoa matokeo katika masuala kama Bwawani, lakini tunaruhusu watu kwenda kukusanyika wote kusubiri matokeo, hatuoni kwamba tunakaribisha matatizo maeneo kama yale, wakati ambapo ilikuwa ni kila mtu wahusika wapo, viongozi walioitwa au waliokuwa wanashirikishwa. Lakini tunawaita karibu nusu nzima ya Zanzibar kuja Bwawani kusubiri matokeo, baada ya hapo kazi inakuwa ya askari inakuwa ya kutawanya kitu ambacho kinaleta usumbufu. Ningeomba suala hili likatizamwa vizuri tukatizama vipi ambavyo umuhimu wa kuwalinda raia na mali zao zinaweza kutumika hapa ikasaidia.

Mhe. Naibu Spika, nije katika suala jengine la upigaji kura. Mheshimiwa bado suala la kupiga kura unavyozungumza kwamba mtu apate haki yake kuna sehemu za chini chini ambazo wapigaji kura wanapiga. Mheshimiwa chini hakuna haki, mtu anachukuliwa kwa nguvu kwenda kupiga kura, mtu anachukuliwa na mtu asiyemtaka kwenda kumpigia kura lakini kwa sababu Sheria inamlinda na yeye mwenyewe anakubali kutokana na kutishwa kwake, sasa inabidi afuate masharti ya kwenda kupiga kura. Kwa hivyo, ningeomba mtu anafanya kazi Serikalini, mtu ana uwezo wa kuandika na kusoma anakwenda kupigiwa kura. Hili suala lingetizamwa vizuri sana huyu mtu ni kwamba unajua wazi kuwa hapa ametekwa na anakwenda kupigishwa kura. Kwa hiyo, vitu vidogo vidogo kama hivi vinaanza ushawishi kule chini kwa sababu ya Sheria ambazo tumezipanga wenyewe. Ningeomba mtu mwenye uwezo wa kuwa ana macho na kila kitu basi mtu yule asiruhusiwe kwenda kupigiwa kura, mtu yule akapige mwenyewe na waliokuwa wanataka kupigiwa kura wanajulikana kama hawa hawana uwezo wa kupiga kura.

Mhe. Naibu Spika, nataka nizungumzie pia suala ambalo limejitokeza hapa kwamba upachikaji wa mabango ya matangazo ya kampeni. Mimi ningeishukuru sana Tume au ningeishukuru wizara kwamba maeneo yote husika ambayo ni maeneo yanayotumika katika mambo kama haya ya kijamii basi masuala haya yakawa ni skuli, masoko na maeneo mengine ikawa hivyo hivyo ambavyo imepitishwa na mimi naunga mkono ili kupunguza baadhi ya mambo ambayo yanajitokeza. Kwa sababu wakati ule Mheshimiwa ni wakati wa vichocheo na ni wakati wa kuweza kuangalia vitu ambavyo unaweza ukaona ni vidogo, lakini vinaweza vikaleta tabu.

Niangalie kitu chengine Mheshimiwa ni kwamba niliona humu katika sehemu moja kutoa taarifa kwa njia za mawasiliano. Lakini Mheshimiwa hata za mdomo, za barua, hizi njia zote haidhuru ni za mawasiliano lakini haikubainishwa humu. Humu zimebainishwa njia za mawasiliano zikiwemo mambo ya elektronikia ambayo labda ni simu na vitu vyengine. Sasa hivi vitu vyengine mtu anaweza kukusanya watu akawaambia kwa mdomo tu kwamba jamani fulani kashinda, fulani kashinda, atakwambia mimi sijatumia vyombo vya elektroniki ni mdomo wangu na mdomo haumo kwenye Sheria. Kwa hivyo, ningeomba mtu yeyote atakayetoa malalamiko ambayo yatakuwa yanahusu pia suala hili likaangaliwa.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naangalia sana pengine labda na humu nitaliona sijaliona, kwamba tunapiga kura watu wote na hata vikosi vyetu vyote ni vya kipiga kura, lakini siku ya kupiga kura

mara nyingi sana vikosi vile vinashindwa nafasi ya kupiga kura. Ningeomba kwa nini na hawa vikosi wasingewekewa siku yao maalumu ya kupiga kura baadae wakatusimamia ulinzi na usalama. Kwa hivyo, nilikuwa nafikiria labda eneo hili litakuwemo lakini sijaliona, hivyo na mimi niliona nipendekeze kwamba askari wetu wangepiga siku yao kura ili siku ya pili wakaweza kutulinda na kuondokana na huu mtafaruku wa kuwa hawakupata haki zao za kupiga kura.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana masuala ambayo tunayaona ya kila siku ni kwamba taarifa hizi zinaleta machafuko tunasoma pale tulipofikia na nimefurahi kutokana na mswada huu utapunguza matatizo zaidi.

Mhe. Naibu Spika, lakini bado nizungumzie suala la ulinzi siku ya kupiga kura. Katika mstari tunasema tunamtaka askari mmoja. Mheshimiwa yule ni binadamu, yule ana haja anakwenda, na ana kila kitu lakini tunamuweka askari mmoja badala yake anashindwa kufanya majukumu yake na tunaanza na machafuko yanayojitokeza. Haidhuru baadhi ya askari wanakuwepo katika maeneo ya doria, lakini kama Sheria askari mmoja inawezekana kuwa hatoshi basi hata wawili waongezwe ili kusaidiana katika mazingira ambayo yanaweza yakatusaidia kwa maelekezo kama hayo. Kwa hivyo, Mheshimiwa mimi nilikuwa nichangie masuala yalivyo.

Jengine na mimi naleta mapendekezo yangu. Muundo wa Tume yetu iliyoundwa ni muundo ni muundo wa vyama ambapo kila mmoja anawania chama chake, sio muundo wa kuleta uwiano wa usawa katika kuleta ukweli, ni muundo wa kuvutana. Ningewaomba wahusika Tume ikatafuta watu ambao wana uwiano wa ukweli sio wale wa kuvutana kisiasa, maana yake hapa kama tunakwenda katika muundo wa kisiasa, kuna vyama vyengine havina uwakala. Sasa wale ina maana wao watakuwa hawana haki, kwa sababu Uwakala uliopo hapa ni wa vyama vyengine viwili au vitatu na tuna vyama zaidi ya 14. Kwa hivyo, ningeomba pakachaguliwa watu ambao hawana uwiano na chama ili kuleta usawa wa maendeleo haya, kuliko kuwakusanya watu wanaopendelea vyama na ndio ukakuta watu wanavutana nani amtakae huyu na nani amtakae huyu. Kwa sababu hawana ukweli wa dhamira ya kuweka Tume wana ukweli wa kuvutana na chama chao na ushindi wa chama chao. Ningeomba hili suala likaangaliwa kwa upeo ili kuweza kuondoa matatizo ambayo yanajitokeza.

Mhe. Naibu Spika, mimi nazipongeza Tume, nawapongeza waliotunga huu Mswada wa kauleta hapa na marekebisho yake yote ambayo nimeyaona, yana umuhimu wa hali ya juu. Mimi nilikuwa nichangie tu nione matatizo ambayo yanajitokeza katika siku za kupiga kura. Kwa hivyo, naomba hayo ambayo wenzangu wameshachangia muda mrefu sana na mimi nichangie haya ili tuone tunaboresha zaidi, ili wananchi wetu watakapokuwa wanapiga kura basi wapate nafasi zao za uhakika.

Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono hoja na nashukuru kwa kunipa nafasi hii, ahsante sana Mheshimiwa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahan Said mchangiaji wetu mwengine ni Mhe. Said Soud Said (MBM) na baadae atafuata Mhe. Suleiman Makame Ali.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu ambao umeletwa kwa nia ya kuikuza na kuiboresha demokrasia ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi ya kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwani Dkt. Ali Mohamed Shein ni Rais mtendaji. Unapokuwa na Rais mtendaji basi mara nyingi mambo yanayojitokeza katika utendaji wake yanaboresha maendeleo ya watu anaowaongoza.

Mhe. Rais kwa nia nzuri tu amekubali kuletwa kwa Mswada huu na uletwe katika Baraza si kwa madhumuni mengine yoyote, lengo la Mswada huu ni kuboresha demokrasia ya watu wa Zanzibar, ili waondokane na zile dhana zilizokuwa zinatumiwa na baadhi ya watu kwamba Zanzibar hakuna demokrasi.

Mhe. Naibu Spika, nataka nikwambie kwamba nchi yoyote duniani inayoendeshwa kwa misingi ya Sheria na Katiba basi nchi hiyo inakuwa na Tume huru. Sasa Zanzibar ina Tume huru, akitokea mtu akisema Zanzibar hakuna Tume huru huyo mtu hajui maana ya demokrasi, huyo mtu hajui maana ya Katiba. Sasa Zanzibar imefanikiwa kuwa na Tume huru inayosimamia chaguzi zote na bahati mbaya ikawa bado haijapewa meno, ndio maana wengine wakathubutu mpaka kujitangaza ni kwa sababu Tume ilikuwa haijapewa meno, lakini sasa tumekubali sisi kama serikali kuhakikisha kwamba Tume ya Uchaguzi inakuwa na meno.(*Makofi*).

Kwa mfano kama Said Soud atagombea Uraisi na atajitangaza basi Tume itakuwa na meno ya kumdhibiti Said Soud, hivi ndivyo ilivyo dunia nzima. Sasa leo hii lazima tukubali Wazanzibari kwamba tumepita katika mistari mingi ya kisiasa na tumekumbana na vituko vya aina mbali mbali, lakini sasa umefika wakati muwafaka chini ya uongozi wa Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein anatengeneza Mswada huu au atausaini Mswada huu kwa madhumuni ya kuileta Zanzibar watu wanayoitaka. Wazanzibari wanataka Zanzibar iliyokuwa tulivu na iliyojaa amani na upendo na haitaweza kupatikana kama itakuwa hatuna misingi mizuri ya Tume huru.

Sasa mimi nataka niseme kwamba kilichotusaidia katika mazingira ya kujenga demokarasia mpaka tukafika hatua hii wananchi wa Zanzibar nawapongeza wote kwa uvumilivu na ustahamilivu wa kupelekwa katika mazingira mazuri ndani ya uongozi wa Dkt.. Ali Mohamed Shein. Mhe. Rais ni mmoja katika watu anayependa nchi yake kuona ina amani na utulivu.

Nataka niwaambie Wazanzibari kwamba Mswada huu hauna lengo jengine. Lengo ni kulinda amani ya nchi na utulivu wa nchi ili tuweze kuwa na demokrasia ya kweli. Lengo la Mswada huu si jambo jengine lolote ni kuhakikisha kwamba tunaingia katika uchaguzi tukiwa na maana ya kushinda au kushindwa kwa amani na utulivu.

Sasa ule utaratibu tuliokuwa tumejipangia sisi vyama vya siasa kwamba hatukubali kushindwa ule si utaratibu mzuri. Lazima ukubali kushindwa pale unaposhindwa usiwe tayari kuwa lazima wewe ushinde kwa sababu tu wewe una chama cha siasa na mimi ninawashangaa sana baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa, wanapotangazwa Wabunge na Wawakilishi katika Tume hii wanafurahia Wabunge wao wamepata, Wawakilishi wao wamepata. Lakini hawakubali wanapoambiwa wameshindwa katika kiti cha Urais. Hili jambo la kushangaza hili. Sasa kwa nini

basi husemi na Wawakilishi kwamba na wao hawakushinda au Wabunge wangu hawakushinda una lazima ushinde wewe tu. Hili ni jambo la kushangaza sana. (*Makofi*)

Sasa nasema kwamba mswada huu lengo na madhumuni makubwa kwa Wazanzibari ni kujenga demokrasia ya kweli na kuiweka nchi yetu katika misingi ya amani na utulivu. Natoa wito kwa vyama vya siasa, tena natoa wito kwa uhakika kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Siasa Tanzania. Kwa maana hiyo nchi hii ina vyama 18 na naamini tarehe 21 na 22 vyama hivi vitakutana Dar- es Salaam.

Ninachosema kwa viongozi wa vyama vya siasa wote lazima tuheshimu Sheria na Katiba ya nchi yetu kwa misingi ya kulea demokrasia, kama ukiwa wewe Mbunge wako anatangazwa unafurahi basi ukiwa umeshindwa kiti cha Urais pia ufurahi, haimaanishi kwamba lazima wewe kiti cha Urais upewe tu hata kama umeshindwa. Ki misingi ya demokrasia katika nchi hii ya Zanzibar lazima tukubali kwamba bado naendelea kuwaambia hao viongozi wenzangu wa vyama vya upinzani kwamba CCM haijapata chama mbadala na kwa sababu haijapata chama mbadala CCM itashinda tu uchaguzi ujao itashinda na uchaguzi mwengine itashinda hivi ndivyo itakavyokuwa. (*Makofi*)

Hatuna chama mbadala tunajenga misingi ya ubinafsi ndani ya kuongoza vyama vyetu na hii ndivyo ilivyo. Lau kama ingelikuwa hakuna ubinafsi basi lazima tungehakikisha kwamba kweli wapinzani tunaweza tukaiendesha upinzani wetu katika majimbo tunaweza kuendesha upinzani wetu katika serikali na tukaweza tukafanya maendeleo ya kweli. Lakini leo una lazima wewe unashindana lazima ushinde, wewe nani kwani, wananchi hawataki na tayari una sababu za kukataliwa mara saba ushagombania hushindi, sasa wewe una lazima ushinde tu. (*Makofi*).

Mimi nasema hivi demokrasia ichukuwe nafasi yake. Tume ya Uchaguzi jipangeni bwana mmetuwekea *limit* ya kugombea Urais miaka 40 mtuwekee na *limit* itakayomfanya mtu asigombee japo hawezi. Mtuwekee *limit* ikiwa kuna *limit* ambayo mnaweza kusema mgombea amegombea zaidi ya mara tatu hajapa nafasi huyu hafai (*disqualified*), mumuone kwamba hafai msimuonee huruma. (*Makofi*)

Mnatuletea amani hapa ya kupendelea. Hii Zanzibar ni Afrika na Afrika ni sehemu ya dunia. Zanzibar inahitaji amani sisi hatuwezi kushinda wanayofanya kina Trumph na sisi lazima tufanye, aah. Sisi tutafanya na yale yanayokwenda na mazingira ya maisha yetu. Tunahitaji amani, tunhitaji kupendana, tunahitaji kusaidiana, tunahitaji kuelewana. Lakini leo ukishindwa wewe unawaambia watu wasioane tena, wasisali Msikiti mmoja, wasizikane, wasiwe pamoja, kwa sababu umeshindwa tu, sijui umeshindwa vipi. Zanzibar hakuna chama kimoja tu cha upinzani, Zanzibar kuna vyama 17 vya upinzani na cha 18 CCM. Sasa wengine wameshiriki katika uchaguzi bado tu hujaridhika.(*Makofi*).

Kimsingi bwana Tume ya Uchaguzi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itatoa meno ili muhakikishe kwamba mfanyakazi yenu vizuri. Hatuoni sababu ya kwamba hamna meno tutakupeni meno. Sisi kama serikali tutakupeni meno mfanye kazi kwa uadilifu, mufanye kazi kwa maana ya kuijenga nchi hii iwe nchi ya amani na utulivu, kila mtu anahitaji kuongoza nchi hii kwa amani na utulivu. (*Makofi*)

Kuna vijana wetu wanasoma wanataka kuongoza nchi hii na sisi tunawaambia tutaendelea kuyalinda Mapinduzi ya Zanzibar na tutayalinda Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sababu ndio yaliyotufikisha humu ndani na bila ya kuwepo kwa Mapinduzi nchi hii ingelikuwa haina thamani na kwa nini hatujiulizi wazee wetu hawakusoma kwa nini? mpaka leo ikawa sisi tumesoma tuna uwezo wa kufafanua tuna uwezo wa kuchangua, tuna uwezo wa kuingiza maendeleo katika nchi yetu. Leo kwa nini sasa tusiwe tayari kulinda Mapinduzi. (*Makofi*)

Tunawaambia wale ambao wanabeza Mapinduzi ya Zanzibar ole wao nasema tena Mapinduzi ya Zanzibar ni Mapinduzi ya wananchi wa Zanzibar na tutayalinda kwa gharama yoyote na ndio maana tukawa tayari kusema kwamba Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar sasa ndio kioo cha kuangalia tunakoelekea hatutakubali kuwa mtu ameshindwa akenda akaa na vyombo vya habari akajitangaza, hiyo hatutokubali, hilo jambo halitatokea. Hatutakubali kumuona mtu mchaguzi unaendelea kwenye vituo humo ndani ana kura kura kwenye makoti anatembea nazo hiyo hatutakubali na hayo yametokea. (*Makofi*)

Hatutakubali kumuona kiongozi wa Chama cha Upinzani hata kama ni mimi uchaguzi kesho au keshokutwa leo anasafiri anakwenda Afrika ya Kusini anarudi na kura kwenye maboksi hatutakubali hilo jambo. Kwa hiyo, lazima kila mtu ataingia kwenye uchaguzi kwa misingi ya kisheria na Katiba na Kanuni ya Tume ya Uchaguzi itakavyoelekeza. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wachangiaji ni wengi naomba niseme naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Said Soud Said ulikuwa bado una dakika zako 5 na wala wachangiaji si wengi sijui kwa nini umeacha. Maana makofi hayo yote ni yako. Maana maneno uliokuwa unazungumza mazima, maneno mazuri na mazima uliyokuwa unazungumza. (*Makofi*)

Mhe. Said Soud Said (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu, kwa sababu sijala hasara bado nina uwezo wa kuengeza basi niko tayari kusema kwamba tunakoelekea tunahitaji kuona wapiga kura. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, katika mambo muhimu ambayo Tume ya Uchaguzi tunakubali wafanye na wafanye kwa maslahi ya wao ili kuipeleka nchi hii salama usalimini ni kuwa na siku mbili tafauti, kuwe na siku mbili za kupiga kura walinzi wanaolinda uchaguzi wakisha kupiga kura siku ya pili sasa tuingie uwanjani tukapige sisi raia na nasema hivyo kwa sababu askari wote ni raia ya nchi hii wanayo haki ya kupiga kura kuchagua na hata wao wakiwa watatoka kwenye kazi ile waombe na wao wana haki ya kuchaguliwa. (*Makofi*)

Lakini kwa sasa hivi tumekuwa tukiwanyima sana nafasi ya kupiga kura kuchagua watu wanaowapenda. Kwa hivyo, mimi napendekeza na naomba Tume ya Uchaguzi ipange siku mbili moja kwa askari moja kwa raia. Ili tuweze kuona wenzetu hawa wanapata hati ya kidemokrasia katika kupiga kura ya kuchagua viongozi wanaowataka.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar ni sehemu ya dunia hakuna mtu ambaye duniani anazuiliwa kupiga kura. Lakini ni vigumu kuona kwamba askari wetu baada ya kuwa aende akapige kura Skuli ya Haile Selasie anapangie ende akasimamie Makunduchi wakati kule hana jina lake, hana kituo

chake, hana lolote, matokeo yake anafanyakazi ile hadi usiku wa manane anashindwa kupiga kura huku kura yake hakuweza kuipiga.

Lakini ni vyema Zanzibar ikaanzisha mfumo wa askari kupiga kura kwanza hatimae raia wapige siku ya pili ili wapate ulinzi na usalama watakaoweza kufanya shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, hilo nilikuwa nimeona niliingize ili *hansard* iweze kuwekwa vizuri. Ahsante Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Said Soud mchangiaji anayefuata ni Mhe. Suleiman Makame Ali muda ukitosha atakuja Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Mswada huu ulio mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais pamoja na Tume ya Uchaguzi kwa kutuletea Mswada huu mzuri, muda muafaka ambao kwamba tunauchangia hapa leo. Lakini pia nimpongeze Mhe. Said Soud Said kwa kutoa na kuweka bayana mambo yote mpaka nje huku watu wamefahamu vya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, nende Sura ya Pili kuhusu daftari la kudumu la wapiga kura. Kwenye (i) inasema kwamba kutakuwa na daftari ya kudumu la wapiga kura litakalotayarishwa na Tume, litakuwa na jina kamili, picha ya mpiga kura, tarehe ya kuzaliwa, sehemu ya makaazi, nakusudia kile kitambulisho cha kupigia kura kama ilivyoelezwa hapa.

Lakini Mhe. Naibu Spika, cha kushangaza kuna baadhi ya wapiga kura wengine inapofika siku ya kupiga kura hawaendi na kitambulisho. Sasa Mhe. Naibu Spika, sisi sote humu ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuna vitambulisho hivi hapa tumepewa hatujulikani kama sisi ni Wajumbe, tunajulikana lakini kitambulisho ni muhimu kuweza kumtabua mtu zaidi.

Uchaguzi uliopita Mhe. Naibu Spika, nakuhakikishia kwamba kule Pemba kuna baadhi ya wengine walipiga kura na leseni za magari, lile ni tatizo kubwa wewe umepewa kitambulisho siku nyengine kitambulisho keshauza huko anakwenda kupiga kura. Kwa hiyo, ikiwa kama mtu hana kitambulisho cha kupiga kura basi pawepo na kifungu cha kumzuia mtu huyo haruhusiwi kupiga kura kwa sababu gani akapewa kitambulisho akakiuza halafu akapata kupiga kura. Kwa sababu kama kutatakuwa na haja ya kuwekwa picha pawepo na majina tu hili ni lazima lizingatiwe na lichukuwe na litafakariwe vizuri sana kwamba bila ya kitambulisho mtu asiende kupiga kura, kwa sababu ukiwa na kitambulisho ni ushahidi tosha kamili na kuondosha ule migongano inayotokea.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende ukurasa wa 176 "sifa za ugombea Urais". Mhe. Said Soud Said alisema lakini Mhe. Naibu Spika, na mimi nataka niongezee, mtu anapofika miaka 75, 80 ninavyojua mimi kisheria yule hauzi wala haununuwi, kwa sababu hata akili zake zinakuwa sizo, anaruka zile akili zinakuwa za kitoto. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar ameweka kwamba wale wanaoanzia miaka 70 wameshakuwa wazee wa kujaaliwa ile pencheni. Kwa hiyo, nimuombe kama Mhe. Said Soud Said kama mfano amefikia umri huo basi aende

akachukuwe pencheni kule na awaachie wengine wenye miaka 40 wagombee ile nafasi. Kwa sababu mtu anapofika miaka ile inakuwa tena hajiwezi, yuko hoi yuko taabani hata kwenye majukwaa kusimama inakuwa tena ni tabu Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, niombe sana kwamba na ule ukomo kama alivyosema Mhe. Said Soud Said basi uwepo hapa kwamba anapofikia miaka hiyo asiruhusiwe kugombea kwa sababu hiyo hapo, hata akipata hiyo serikali ataiongoza vipi Mhe. Naibu Spika, hata apate hiyo serikali ana miaka 80 na kuendea mbele ataiongozaje, maana hizo akili tena zinakuwa sizo zinakuwa akili tena za kitoto. Kwa sababu mtu anapokuwa mtoto na anapokuwa mtu mzima miaka mingi akili zake zinarudi zinakwa zile zile za kitoto. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, niombe kwamba hili waliangalie watu wa Tume walichukuwe kuhakikisha kwamba na ule ukomo wa Rais pia wameuweka.

Mhe. Naibu Spika, kwenye Sura ya Nne kwenye masuala ya waangalizi hawa.

Mhe. Naibu Spika, uchaguzi ni gharama na Tume ya Uchaguzi inapata gharama kubwa sana hususan kwa wale waangalizi wa ndani na waangalizi wa nje. Mhe. Naibu Spika, leo kuna waangalizi wanakuja hapa wanaposikia tayari uchaguzi wa ndani ya wa nje wanakuwa kama sisimizi wanajitokeza ili kutaka kusimamia kuangalia uchaguzi unakwendaje.

Lakini Mhe. Naibu Spika, waangalizi wale wengine hawaji kwa ajili ya uchaguzi, wanakuja na mambo yao mfukoni. Kwa hiyo, sasa cha kuomba hapa kwamba wao wale waangalizi basi ni kwamba waweze kuichangia Tume hata kama ni shilingi laki mbili au laki moja ili kuhakikisha kwamba ile gharama ya Tume wanayopewa kwa sababu wanakabidhiwa mambo mengi, wanakabidhiwa Katiba, wanakabidhiwa vitu mbali mbali. Kwa hiyo wanaitia Tume hasara kwa sababu hayo yametokea mpaka Angola.

Mhe. Naibu Spika, Angola kule waangalizi wanapokwenda kuangalia uchaguzi wanaisaidia Tume wanaichangia. Kwa hiyo na hapa niombe kwamba wahakikishe waangalizi hawa watoe waichangie Tume na hiyo iwe imo katika Sheria ya Uchaguzi na iwe ni lazima kuchangia na kama mtu hakuweza hivyo aondoke. Kwa sababu inakuwa msongamano ni mwingi, watu wengi wanataka kuangalia uchaguzi wengine huwa hawana lolote wanakuja kwa maslahi yao tu na mambo yao wanaotaka wenye wao. Kwa hiyo, niombe sana kwamba waangalizi wa Tume ya Uchaguzi wanaotoka nje na wa ndani waweze kuchangia ili kusaidia gharama zile za Tume ya Uchaguzi. Kwa sababu Tume ya Uchaguzi inapata gharama kubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia na pia niipongeze tena Kamati hii ya Mhe. Omar Seif Abeid Kamati ya Viongozi Wakuu na pamoja na serikali kwa ujumla kuhakikisha kwamba wametuletea Mswada huu kwa muda muafaka na *inshaalla* Mhe. Naibu Spika, Mswada huu tutaupitisha kwa moyo mmoja ili kuhakikisha kwamba tunaipa meno Tume ya Uchaguzi kuhakikisha kwamba 2020 tunakwenda kwenye uchaguzi bila ya kukutana na msongamano wowote.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda uliobakia ni mdogo sana na nafahamu kwamba Wajumbe wana mengi ya kuchangia. Kwa hiyo, tumebakiza wachangiaji kama wanne. Kwa hivyo, tukijaaliwa kesho tutaendelea na wachangiaji. (*Makofi*)

Sasa tu niseme kwamba naahirisha kikao hichi hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:37 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 13/12/2017 saa 3:00 asubuhi)